Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Ishirini na Sita - Tarehe 17 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:**

Hotuba ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba katika mwaka uliopita pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2003/2004.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 229

**Kukarabati/Kujenga Barabara ya Babati -Gallapo - Quash Kibaya**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuikarabati/kuijenga barabara ya Babati - Gallapo - Quash hadi Kibaya - Wilaya ya Kiteto ili kuweka mawasiliano ya uhakika na ya njia fupi kati ya maeneo hayo badala ya barabara iliyopo sasa ambayo ni ndefu na inalazimu kupitia Kondoa - Mkoani Dodoma?

(b) Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuimarisha barabara ya Mbuyu wa Jerumani (Mwada) - Magara - Mbulu ili kurahisisha usafiri wa njia fupi kati ya Makao Makuu ya Mkoa (Babati) na Makao Makuu ya Wilaya ya Mbulu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kujenga barabara ya kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara ambayo yapo Babati na Miji ya Kibaya na Orkesumet katika Wilaya ya Kiteto na Simanjiro. Kwa sasa Serikali inakusudia barabara hiyo ipite katika maeneo ya Gallapo na Quash ingawa maeneo yaliyo muafaka kiuchumi na kijamii ya kupitisha barabara hiyo yatafahamika baada ya utafiti wa kina kufanywa na Mhandisi Mshauri. Aidha, barabara hii imetengewa shilingi milioni 15.5 kwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi *(Spot Improvement)* toka Babati hadi Gallapo ambapo ina urefu wa kilometa 31.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango maalum *(Special Project)* wa kuimarisha barabara ya Mbuyu wa Jerumani (Mwada) - Magara - Mbulu, mbali na ile ya barabara ya sasa ya Babati - Dareda - Dongobesh - Mbulu ambayo inatumika na inaendelea kuimarishwa katika Mlima wa Dabil *(Dabil Escarpment).* Hata hivyo, Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo ya kawaida *(Routine Maintenance)* barabara ya Mbuyu wa Jerumani (Mwada) - Magara - Mbulu chini ya Halmashauri husika za Wilaya ya Mbulu na Babati. Barabara hii imetengewa jumla ya shilingi milioni 53.3 kwa mwaka huu wa fedha. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 12.5 ni kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi kati ya Magara na sehemu barabara hiyo inapokutana na barabara kuu itokayo Arusha kwenda Babati kilometa 25, shilingi milioni 11 ni kwa ajili ya matengenezo ya kawaida *(Routine Maintenance)* kati ya Mbulu hadi Magara kilometa 27 na shilingi milioni 30 ni za matengenezo ya madaraja matatu.

Na. 250

**Watumishi Mbalimbali Walioko Vijijini**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna baadhi ya watumishi wa aina mbalimbali walioko Vijijini hasa wa Kata ya Kitunda kama vile walimu, wataalam wa kilimo, wataalam wa afya na kadhalika; na wanafanya kazi mbali na Makao Makuu ya Wilaya yaani Sikonge Mjini; na kwa kuwa kutokana na ubovu wa barabara ya kuunganisha Tarafa ya Sikonge na Tarafa ya Kiwere ambayo nyakati za masika barabara hiyo haipitiki kabisa, hivyo kuwalazimu watumishi hao kusafiri kwa baiskeli kwa siku mbili njiani kufuata mishahara, kusafirisha wagonjwa pamoja na huduma nyingine:-

(a) Je, wafanyakazi wanaoishi na kufanya kazi kwenye mazingira ya aina hiyo Serikali inawapa motisha gani ili waendelee na kazi zao kwenye mazingira hayo bila kinyongo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kufanya mabadiliko ili watumishi hao wapewe vituo vingine vilivyo karibu na huduma muhimu badala ya kuwaacha kwenye vituo hivyo tangu waajiriwe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba bado lipo tatizo la mazingira magumu ya kufanya kazi katika maeneo yetu ya Vijijini ikiwa ni pamoja na Kata ya Kitunda katika Wilaya ya Sikonge. Mazingira hayo ni pamoja na umbali kutoka Makao Makuu ya Wilaya, barabara zisizopitika wakati wote wa mwaka, ukosefu wa usafiri wa kuaminika, uhaba wa mahitaji muhimu na hata sehemu za kuishi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina utaratibu wa kuwapatia motisha maalum ya fedha watumishi mbalimbali wa Halmashauri kwa kufanya kazi kwenye mazingira magumu. Kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Utumishi wa Umma, Serikali imekuwa inapandisha viwango vya mishahara vya

watumishi wake kila mwaka kulingana na uwezo wa fedha ili kuwawezesha watumishi mbalimbali kumudu maisha katika maeneo wanayofanyia kazi.

Vile vile Serikali inaendelea kujenga mazingira bora yatakayowawezesha watumishi popote pale walipo kuweza kufanya kazi kwa ufanisi bila kinyongo. Hatua hizo ni pamoja na watumishi kupatiwa nyumba za kuishi, watumishi kupatiwa vyombo vya usafiri kama vile pikipiki, magari na baiskeli, kuboresha hali ya miundombinu mbalimbali zikiwemo barabara za Vijijini, maji, afya na elimu na kwa Sikonge kwa mwaka huu wa fedha imetengewa shilingi 32,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu kama moja ya hatua ambayo inasaidia.

Mheshimiwa Spika, naomba mwisho basi, nitoe wito kwa wananchi popote pale nchini ili kwa kusaidiana na wahisani na sekta binafsi, waendelee kusaidia kuchangia katika ujenzi wa nyumba za watumishi na miundombinu mbalimbali katika maeneo yao.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekubali kwamba yapo maeneo ambayo kwa kweli ni magumu kwa utendaji wa kazi kwa watumishi wetu, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kwamba je, Serikali inatathmini vipi kazi za watumishi walioko katika maeneo hayo ya Vijijini ambayo watumishi wengi wa Serikali hasa katika maeneo ya Wilaya hawawezi wakafika kwa kipindi cha mwaka mzima? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, upo utaratibu wa Kiserikali ambao unatumika kutathmini kazi za watumishi wote popote pale walipo bila kujali kwamba wapo mbali na Wilaya au wako karibu na Wilaya. Utaratibu huu mara nyingi ni wa kujaza fomu ambao hata kwenye *Local Government Authorities* unapaswa kutumika. Kwa hiyo, kwa kweli utaratibu upo na kwa kiasi kikubwa kabisa umekuwa unazingatiwa.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika swali la msingi imeonekana kwamba watumishi hawa wanasafiri kufuata mishahara yao kwa siku mbili na inatarajiwa pia kwamba wanatumia siku mbili nyingine kurudi katika vituo vyao vya kazi. Sasa katika mazingira haya; je, Serikali haioni kwamba watumishi wa namna hii wanaofanya kazi mbali na Miji au Wilaya, umefika wakati wa kuwafikiria kwa kuwapa posho maalum kwa ajili ya mazingira magumu kabisa ya kufanya kazi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri hata juzi Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni alijaribu kutoa ufafanuzi juu ya jambo hili. Kwa sasa utaratibu kama huo haupo wa kuweza kutoa posho maalum kwa ajili ya watumishi mbalimbali kutokana na sababu hiyo ambayo imeelezwa na Mheshimiwa. Kwa sasa kinachofanyika ni juu ya watumishi katika maeneo waliyoko kutengeneza taratibu zinazowawezesha kukidhi haja hiyo bila ya kuparaganya taratibu zao za kazi na wengi wamekuwa wakishirikiana kwa kumtumia mtumishi mmoja kwenda kufuata mishahara, anawaletea wenzake na wanafanya hivyo zamu kwa zamu. Hiyo ndiyo hali halisi tuliyonayo.

Na. 251

**Barabara ya Kate - Nkundi**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa wafadhili kutoka nje wameisaidia Serikali na Wilaya ya Nkasi kuitengeneza barabara itokayo Namanyere hadi Kijiji cha Kate umbali wa kilometa 50 na kubaki sehemu ya barabara yenye umbali wa kilometa 32 kati ya Kijiji cha Kate hadi Nkundi; je, Serikali ina mpango gani wa kuitengeneza

sehemu iliyobaki au kutafuta wafadhili ili wakamilishe matengenezo ya barabara hiyo ili iweze kuleta maana na manufaa kwa wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nkundi - Kate - Namanyere yenye urefu wa kilometa 75.2 ni barabara ya Mkoa, inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS),* Mkoa wa Rukwa.

Sehemu kubwa ya barabara hii kati ya Namanyere hadi karibu na Kijiji cha Kate umbali wa kilometa 46.7, imefanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe. Matengenezo hayo, yalifanyika kati ya mwezi Oktoba, 2000 na Machi, 2003 na kugharimu kiasi cha shilingi milioni 402.51 kwa fedha kutoka Shirika la Misaada la Marekani *(USAID).*

Mheshimiwa Spika, sehemu iliyobakia kati ya Kate - Nkudi, yenye urefu wa kilometa 28.5 imeendelea kufanyiwa matengenezo ya kawaida na ya maeneo korofi kupitia Wakala wa Barabara ili kuhakikisha barabara hii inapitika katika majira yote ya mwaka.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2002/2003 kiasi cha shilingi milioni 35.72 kilipangwa na kutumika kwa matengenezo ya maeneo korofi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuhakikisha kuwa barabara yote inapitika majira yote ya mwaka, Serikali bado itaendelea na jitihada zake za kutafuta fedha kutoka vyanzo vyake mbalimbali, vikiwemo wafadhili na wahisani ili kuhakikisha sehemu iliyobakia nayo inakarabatiwa.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha ambazo zilitolewa hazikutosha kabisa kutengeneza barabara hiyo ukitilia maanani kwamba ina matuta makubwa matatu; je, Serikali ina mpango gani hata wa dharura kwa ajili ya kuongeza fedha nyingine ukitilia maanani kwamba barabara hiyo inaunganisha barabara nyingi zinazokwenda Ziwani eneo la Ziwa Tanganyika?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa barabara za *TANROADS* mara nyingi huwa ni mbaya sana katika eneo la Nkasi kama vile barabara za Chala - Namanyere - Kirando, - Ryazumbi - Kabwe, Namanyere - Mparamawe ikiwa ni pamoja na barabara hii; je, Serikali itakubali sasa kuhakikisha kwamba katika eneo la Nkasi ambalo limekuwa likisahaulika kwa muda mrefu kutengenezwa barabara zake, inaliangalia kwa namna ya pekee kwa kuliongezea fedha ili kusudi barabara zake zitengenezwe?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la awali nilisema kwamba tunajitahidi kutafuta fedha ili tuweze kuhakikisha kwamba barabara hii ya kutoka Kijiji cha Nkundi kwenda Kate - Namanyere inakarabatiwa yote. Hiyo ni jitihada ya Serikali na bado iko kwenye jitihada yake. Lakini mpango wa dharura wa kuiokoa barabara hiyo haupo kwa sababu tunazo tayari pesa tunapanga kila wakati na itatengenezwa kuhakikisha kwamba inapitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara nyingi mbovu za Wilaya ya Nkasi, naomba nisikubaliane naye sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu mimi mwenyewe nimekwenda huko bahati mbaya sikumkuta yeye lakini nilifika kule na nilipita.

Kwanza, nilitokea Sumbawanga nikaenda mpaka Sitalike na nikarudi mpaka Muze na vile vile nilikwenda upande wake Namanyere mpaka Katangara, kwa kusema kweli *Regional Manager* anajitahidi sana kuhakikisha barabara zile zinapitika. Barabara ni ndefu, ni ghali, ilikuwa mbovu tangu zamani, Serikali inajitahidi kupanga pesa ione kama inaweza kuziokoa barabara hizi. *(Makofi)*

Na. 252

**Barabara za Buhigwe hadi Mvugwe**

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Kisili - Buhigwe ni barabara ya Mkoa ambayo hufanyiwa matengenezo na Serikali Kuu; na kwa kuwa barabara hii zamani ilifika Muyama - Migongo - Mugera mpaka Mvugwe na hivi sasa haijafanyiwa matengenezo; na kwa kuwa barabara hiyo haijafanyiwa matengenezo *(substantial)* tangu uhuru na mpaka hivi sasa haipitiki.

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuitengeneza barabara hiyo ili wananchi waondokane na kero na adha ya usafiri?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama hataridhika na jibu hili kwa sababu ya mabadiliko yake basi alete hilo swali la mabadiliko baadaye.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma una barabara za Mkoa zenye urefu wa kilometa 594 zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)* kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi. Barabara hizo ni pamoja na Kidabwe - Uvinza kilometa 75, Uvinza - *Tabora Border* kilometa 119, Simbo - Ilagala - Kalya kilometa 172, Kibondo - Mabamba kilometa 42, Kakonko - Nyaronga - Nyakahura kilometa 71, Kasulu - Manyovu kilometa 50 na Kisili - Mahembe - Buhigwe kilometa 65. Hizi ndiyo barabara za Mkoa.

Mheshimiwa Spika, barabara hizo alizozitaja Mheshimiwa Mbunge ziko kwenye mtandao wa barabara za Wilaya ambazo ni Buhigwe - Muyama - Migongo - Mugera hadi Makere kupitia Heru Ushingo - Nyarugusu. Sehemu ya barabara ya moja kwa moja toka Nyarugusu hadi Mvugwe haipo.

Aidha, barabara hizi zinahudumiwa na kutunzwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Hivyo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ikishirikiana na Wabunge kupanga utekelezaji wa barabara hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, umelionaje jibu hilo?

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, linafaa faa kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika hotuba yangu niliyoitoa wakati wa mawasilisho ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, iliashiria ya kwamba barabara za Mkoa wa Kigoma zilizoko ndani ya matengenezo ya Serikali Kuu ni chache; je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kwa kuwa barabara hii inayotoka Kisili kwenda Buhigwe - Mvugwe ndiyo barabara ambayo ilikuwa inatumika zamani kusafirisha watu kwa njia ya mabasi na sasa sehemu ya Muyama - Migongo - Mugera mpaka Mvugwe haipitiki tena; je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuiingiza katika utaratibu wa barabara zinazojengwa na Serikali Kuu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru Mheshimiwa Mbunge amekubaliana na jibu la msingi kwamba linafanana na masahihisho, kwa hiyo, hatutegemei tena swali lingine.

**SPIKA:** Ndiyo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, pili, nakubaliana kwamba barabara hiyo ni mbovu lakini naomba na Mheshimiwa Mbunge akubaliane na mimi kungojea wakati tutakapoleta Sheria

Kuu ya barabara kuu, mabadiliko yale ya barabara ambapo tutajadili sote hapa na kukubaliana sote hapa kwamba ni barabara ipi sasa inapanda ngazi na ipi inashuka. *(Makofi)*

Na. 253

**Kuanzisha Hospitali ya Mifupa**

**MHE. USSI YAHAYA HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa hapa nchini ipo Taasisi pekee ya Mifupa *(MOI)* Dar es Salaam; je, Serikali ina mpango gani wa kufikiria kuanzisha hospitali maalum za kushughulikia matatizo ya mifupa kikanda na kuhakikisha kuwepo kwa wataalam wa kutosha wa fani hiyo pamoja na vifaa ambavyo vitakidhi haja ya kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji, Mbunge wa Chaani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya gharama kubwa ya kuanzisha Taasisi kama hiyo, Serikali haina mpango kwa sasa wa kuanzisha Hospitali maalum Kikanda za kushughulikia matatizo ya mifupa na mishipa ya fahamu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa huduma za mifupa na mishipa ya fahamu zinatolewa katika kila Hospitali ya Rufaa kama huduma zozote zile za upasuaji kwa sababu Madaktari Bingwa wa Upasuaji pia nao wanashughulikia mifupa na mishipa ya fahamu.

Mheshimiwa Spika, badala ya kuanzisha Hospitali za Kanda, Wizara yangu imeanzisha mpango maalum wa kuwafundisha Madaktari Bingwa wa Upasuaji toka Mikoani mbinu za msingi za kushughulikia matatizo ya mifupa na mishipa ya fahamu ili waweze kumudu matatizo ya msingi ya mifupa na mishipa ya fahamu huko huko waliko na kuwapa rufani kwenda *MOI* wagonjwa wenye matatizo makubwa. Hatua hii itawezesha hospitali zote za Mikoa kuwa na wataalam hawa kwa hatua za msingi. Mpango huu unaitwa *Satelite Training.*

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara yangu ina mpango wa kupeleka huduma za Madaktari Bingwa Mikoani na hata Wilayani yaani *Outreach Consultancy Services.* Katika mpango huu badala ya wagonjwa kupelekwa kwenye hospitali za rufaa kila mara, Madaktari Bingwa watapanga zamu za kwenda katika Hospitali za Mikoa na kutoa huduma za kibingwa katika hospitali hizo. Hii itawapa nafuu wagonjwa na ndugu kwa kuwapunguzia gharama za usafiri na kadhalika. Kila Hospitali ya Rufaa itapanga ratiba yake ya kutoa huduma hizi katika eneo lake.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu inaanzisha mafunzo ya uzamili ya ubingwa wa mifupa na mishipa ya fahamu *(M.Sc Orthopaedics and Neuro-Surgery)* katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili kwa kutumia Taasisi ya *MOI.*

Hatua zote hizi zitatuwezesha kuwa na wataalam wa mifupa na mishipa ya fahamu Mikoani. Matatizo makubwa ya mifupa na mishipa ya fahamu yataendelea kupelekwa katika Hospitali ya *MOI.*

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, kwa majibu mazuri na yenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba kwa kuwa kumejitokeza tabia kwa baadhi ya Madaktari wanapopangiwa kwenda Hospitali za Mikoani ama Wilayani, wengine hawaendi; je, Serikali itahakikisha kwamba hao wanaopangiwa wote wanafika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya Madaktari ambao wanapangiwa katika Hospitali za Mikoa na Wilaya wanakataa au hawafiki katika maeneo hayo. Sasa utaratibu uliopo ni kwamba kama Daktari atakataa kufika sehemu ya kituo alichopangiwa, basi hatua za kinidhamu zinachukuliwa na hii inaweza ikapelekea kufukuzwa kazi maana zamani ilikuwa wanaweza wakabadilishwa kituo. Jambo hilo sasa limeacha kufanyika na hii inapelekea kuwafanya wale wanaopangiwa maeneo yao wafike katika maeneo husika.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri anakubali kupokea orodha ya Madaktari waliopangiwa kwenda Wilaya ya Ulanga na kwa hiyo mpaka leo hawajaenda, atakuwa tayari kupokea orodha hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, niko tayari kabisa kupokea orodha ya Madaktari waliopangiwa katika Wilaya zetu mbalimbali na si Ulanga peke yake, kama kuna Waheshimiwa Wabunge wengine wana tatizo kama hilo, tutakuwa tayari kuzipokea na tutazifanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 254

**Vipimo vya Ukimwi na Dawa za Kuongeza Uhai kwa Waathirika**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA** aliuliza:-

Kwa kuwa ulimwengu mzima ikiwemo Tanzania upo kwenye vita ya kupambana na ugonjwa hatari wa Ukimwi ambao hauna kinga wala tiba licha ya juhudi mbalimbali zinazofanywa na wataalam duniani kote; na kwa kuwa Serikali inaendelea kuwaelimisha na kuwashawishi wananchi wakapime afya zao ili wawe na uhakika na mwenendo wa afya zao; na kwa kuwa kipimo cha kupima Ukimwi kinachoaminika ni kile cha *CD4* kinachoonyesha hali ya muathirika na kinga halisi iliyosalia katika mwili wake tofauti na kipimo cha *Elisa* kinachotumika sehemu nyingi hata kwenye vituo vya afya nchini:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi kwa kupunguza gharama za kipimo cha *CD4* ambazo zinafikia shilingi 30,000 gharama ambazo mwananchi wa kawaida hawezi kumudu?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kuwadhibiti wanaoagiza dawa za kuongeza nguvu ya waathirika na kuziuza kati ya shilingi 80,000/= hadi shilingi 120,000/= bei ambayo ni kubwa kupita kiasi?

(c) Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya (a) na (b) ya swali hili kwamba ikiwa dawa ya kurefusha maisha ya waathirika inauzwa hadi shilingi 200,000/= kwa dozi kiwango ambacho wananchi walio wengi hawawezi kumudu; je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo hasa ikitiliwa maanani kwamba kuna fedha za wahisani na za Serikali zinazotengwa kwa lengo la kukabiliana na janga hilo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, naomba nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipimo cha *Elisa* ndicho kinachobainisha endapo mtu ameambukizwa virusi vya Ukimwi au la. Hivyo kila mtu hana budi kuanza na kipimo hiki endapo anataka kujua kama ameambukizwa. Kipimo cha *CD4* ni kipimo kinachoonyesha kinga iliyosalia katika mwili wa muathirika na hivyo kinahitajika kwa wale tu waliobainika kuwa wameambukizwa virusi vya Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mashine za kupima *CD4* yaani *FACs-count machine* zinagharama kubwa na mashine moja huuzwa kwa bei ya zaidi ya shilingi milioni 42. Aidha, vifaa vya kupimia *(test kits) CD4* yenye vipimo 50 hugharimu kati ya shilingi 800,000/= hadi shilingi 920,000/=. Kwa sababu hii vituo vingi vimekuwa vikitoza kiasi cha shilingi 30,000/= ili kuchangia gharama. Hata hivyo, hivi sasa gharama imepunguzwa hadi kufikia wastani wa shilingi 15,000/= kwa kipimo kimoja. Inawezekana gharama hii itapungua zaidi siku za usoni kadri mashine hizi zinavyoendelea kuwa nyingi nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, si rahisi kuwadhibiti wanaouza dawa hizi kwa bei kubwa kwa kuwa itakuwa tunaenda kinyume na dhana ya soko huria. Serikali inachofanya ni kuruhusu makampuni mengi zaidi kuleta dawa hizi ili kuwe na ushindani. Aidha, viwanda vya dawa vya humu nchini vimeruhusiwa kutengeneza dawa hizi ili bei ipungue zaidi. Serikali inaendelea kujadiliana na wafadhili mbalimbali ili wasaidie kupatikana kwa dawa hizo kwa gharama nafuu.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la sehemu (b) ni kwamba Serikali inaendelea kuwashawishi makampuni mengi zaidi yaingize dawa hizo nchini na viwanda vya ndani vizalishe kwa madhumuni ya kupunguza bei. Hivi sasa Serikali iko kwenye mazungumzo na Taasisi mbalimbali ikiwemo *Global Fund, Bill Clinton Foundation and Axios International* yenye madhumuni ya kupewa msaada wa dawa hizi ili ziwafikie wananchi wengi kwa gharama nafuu.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali sasa inatenga fedha nyingi za kutosha kwa ajili ya kupambana na tatizo hili la Ukimwi; na kwa kuwa pia Serikali inapata misaada mingi sana kutoka kwa wafadhili mbalimbali kwa ajili ya kukabiliana na janga hili la Ukimwi; na kwa sababu fedha hizi bado zinakwenda tu kwenye warsha, semina na kadhalika; je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu sasa wa kupeleka fedha hizi kama ruzuku kwenye gharama ya madawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba bei za madawa haya ziko juu; na kwamba kwa sababu tuna dhana sasa ya soko huria Serikali haina uwezo wa kuingilia, hivi hata inapofikia pale ambapo wananchi wake wanaweza wakasaidiwa kwa *intervention* ya Serikali kuweza kudhibiti bei za madawa haya pale ambapo Serikali inakuwa na uhakika wa bei hizo, Serikali inashindwaje kufanya hivyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia fedha za wafadhili kwa ajili ya kununulia dawa badala ya kila siku kuendelea na semina, tunapoandika michanganuo ya kuomba fedha, michanganuo ile inaeleza ni mambo gani tunataka kufanya. Sasa unapopeleka mchanganuo uka-*emphasis* kwamba unataka kuweka fedha hizo katika kinga basi lazima fedha hizo ziende kwenye kinga na kinga ni pamoja na elimu ambayo tunaitoa kwa njia ya semina na warsha mbalimbali lakini vile vile vitu kama *condom promotion* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tumepeleka mchanganuo wa kuomba fedha kwa ajili ya madawa katika *Global Fund* fedha hizo ni zaidi ya dola za Kimarekani milioni 800. Bila shaka fedha hizo zikipatikana tutaweza kuingiza katika ununuzi wa dawa na kupunguza gharama za dawa hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, napenda kusema kwamba tunapokuwa na utaratibu au dhana ya soko huria basi tuna wajibu wa kuheshimu dhana hiyo kwa sababu ndiyo Sera ya Serikali. Sasa endapo watu wanapandisha sana bei hizo njia pekee tunayoiona ni kuendelea kuruhusu makampuni mengi zaidi yaagize dawa na kuzungumza na wafadhili wapunguze bei ya dawa hizo. Hiyo ndiyo njia rahisi badala ya kuwalazimisha waagizaji wapunguze bei kwa lazima itakuwa inakwenda kinyume na dhana nzima ya soko huria.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la Ukimwi ni zito tukiliweka katika utaratibu wa soko huria ina maana Serikali inakwepa wajibu wake, kwa nini maduka ya Serikali yasiwekwe rasmi kwa ajili ya kuuza dawa hizi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, jibu ni lile lile tu kwamba Serikali imeamua kujitoa katika biashara, Serikali ina-*promote* sekta binafsi ifanye biashara. Leo tumeshaamua hivyo na tumeanza kufanya hivyo sio rahisi tena kurudi nyuma kuanza kupanga maduka ya Serikali kuuza dawa hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba ushindani katika soko huria ukiendelea bei ya dawa hizi itashuka. Nina mfano wa kutosha kabisa kwamba pale tulipoanza dawa hizi zilikuwa zaidi ya shilingi 500,000/= kwa mwezi, leo tunazungumzia shilingi 80,000/= na bila shaka zitaendelea kupungua kwa hiyo sioni sababu Serikali iingie kwenye biashara hii.

Na. 255

**Wanafunzi Waliofaulu Kuingia Sekondari**

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa Elimu ya Sekondari ni msingi mkubwa wa kuwawezesha wananchi kujikomboa kwenye umaskini na kuliletea Taifa maendeleo:-

(a) Je, ni wanafunzi wangapi waliofaulu mtihani wa Darasa la Saba nchini, Mkoa kwa Mkoa na ni wangapi kati ya hao walipata nafasi ya kujiunga na elimu ya Sekondari za Serikali kwa miaka ya 2000, 2001 na 2002?

(b) Kama zikijumuishwa shule zote za Serikali na za jamii, mashirika na shule binafsi Tanzania; je, ni watoto wangapi waliohudhuria elimu ya sekondari nchini kwenye Vidato vya I, II, III na IV katika miaka ya 2000, 2001, 2002 na 2003?

(c) Je, ni wanafunzi wangapi waliofanya mtihani wa Taifa wa Kidato cha II na ni wangapi walifaulu katika miaka ya 2000, 2001 na 2002?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi wanaofaulu mtihani wa Darasa la Saba Kitaifa na idadi ya wanaochaguliwa kujiunga na masomo katika shule za Sekondari za Serikali imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kama ifuatavyo:-

| Mwaka | Waliofaulu D. VII | % Waliofaulu | Waliojiunga Sekondari za Serikali | % Waliojiunga Sekondari za Serikali |
|---|---|---|---|---|
| 2000 | 85,576 | 22.00 | 48,404 | 12.42 |
| 2001 | 127,351 | 28.60 | 58,159 | 13.10 |
| 2002 | 133,674 | 27.14 | 59,509 | 12.10 |

Idadi ya waliofaulu na idadi ya waliochaguliwa kuingia shule za Sekondari za Serikali katika mwaka 2000, 2001 na 2002 Mkoa kwa Mkoa, imeoneshwa katika jedwali Na.1 ambalo Mheshimiwa Mbunge atapewa sababu ni refu mno kulisoma hapa Bungeni.

(b) Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi wote wa Kidato cha I - IV katika shule zote za Sekondari nchini yaani za Serikali na zisizokuwa za Serikali ilikuwa kama ifuatavyo:-

Mwaka Wanafunzi

| | |
|---|---|
| 2000 | 238,194 |
| 2001 | 264,892 |
| 2002 | 296,529 |
| 2003 | 319,487 |

Mheshimiwa Spika, idadi kwa kila darasa kwa miaka hiyo imeoneshwa kwenye jedwali Na.2 ambalo Mheshimiwa Mbunge atapewa.

(c) Mheshimiwa Spika, wanafunzi waliofanya mtihani wa Taifa wa Kidato cha Pili na kufaulu kwa mwaka 2000, 2001 na 2002 ni kama ifuatavyo:-

| Mwaka K II | Watahiniwa K II | Waliofaulu K II | % Waliofaulu K II | Alama ya kufaulu |
|---|---|---|---|---|
| 2000 | 68,527 | 59,267 | 86.49 | 21 |
| 2001 | 84,781 | 68,057 | 80.27 | 26 |
| 2002 | 105,089 | 75,245 | 71.60 | 30 |

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaweza kusomwa kwa ukamilifu zaidi katika kijitabu kiitwacho *Basic Statistics in Education 1999 - 2003 National Data* kama hiki nilichokishika hapa, kilichogawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na hotuba yangu ya bajeti ya mwaka huu.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa idadi ya wanafunzi waliofaulu Darasa la Saba kuingia Kidato cha Kwanza na kuchaguliwa kuingia Shule za Sekondari katika miaka husika ni nusu ya wale ambao walifanya mtihani je, Serikali itakubaliana nami kwamba wakati umefika tubadilishe shule zetu zote za Sekondari ziweze kuwa na awamu mbili kila siku, awamu ya kwanza asubuhi mpaka mchana na awamu nyingine mchana mpaka jioni ili tuweze kuchukua watoto kiasi cha asilimia 30?

(b) Kwa kuwa shule zetu za Sekondari zina Walimu wachache sana na inaelekea kiwango cha kufeli watoto katika mtihani yao ya Kidato cha Pili inatokana na kutokuwa na Walimu wa kutosha na wenye uwezo je, Serikali itakubaliana nami kwamba kiwango cha kufaulu kwa watoto hawa kingebaki alama 21 mpaka hapo tutakapoweza kuwafundisha au tukafuta kabisa mtihani huu wa *Form II?*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, tukisema tuongeze awamu na katika swali la pili yeye mwenyewe amezungumzia uchache wa Walimu, tutakuwa tunalipanua tatizo. Napenda kukiri kwamba hali ya Walimu katika Shule za Sekondari sio nzuri kwa sababu ile kasi ya upanuaji hatukuioanisha vizuri na ajira ya Walimu wenye sifa za kufundisha katika Shule za Sekondari, kwa hiyo upo uhaba huo. Kwa hiyo, tukifanya uamuzi wa kuwa na awamu mbili jambo hili linaweza kuwa zuri lakini linahitaji maandalizi ya kutosha katika suala la Walimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu alama ya kufaulu kwamba ingebakia 21 ukweli ni kwamba tumekuta hao wanaopata alama 21 ukifanya tathmini wanapofika Kidato cha Nne katika matokeo ya *Form IV* karibu asilimia 90 wanapata *Division Zero* au *Division Four* ya chini sana ambayo haiwafikishi mahali popote. Kwa hiyo, tumeona ni vizuri kuwa na alama ya kufaulu ya asilimia 30 ambayo ni kipimo kizuri na tangu tumeweka alama hii kuwa 30 badala ya 21 kwa kweli Walimu wameongeza jitihada ya kufundisha na wanafunzi wameongeza jitihada ya kujifunza na matokeo wengi zaidi wanafaulu kama takwimu zilivyoonyesha hapa.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na idadi ndogo ya wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na Shule za Serikali hivi sasa ambayo ni chini ya asilimia 10 ambao ni cream kwa nchi nzima, je, Wizara haioni kwamba utaratibu wa sasa wa kuwa na *Special Schools* haujibu swali hili na kwamba kwa kuwa na *Special Schools* kunasababisha wale walio bora zaidi wasiwe mbegu kwa wenzao katika shule nyingine kwa hiyo ni bora ifute utaratibu huo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, tuna utaratibu wa *Special Schools* zinazochukua wanafunzi wanaofaulu kwa alama za juu zaidi. Sasa hivi katika Wizara tuna mjadala mkubwa na tutafurahi kupata mawazo unaoliangalia upya jambo hili kama kweli linatupa faida zilizotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu ukienda kwenye hiyo inayoitwa *Special School* unakuta hali yake kama shule ni ya kawaida na wala haina vifaa vingine maalum. Kwa kweli tulichofanya tumechukua watoto wenye ujuzi, wenye vipaji na wanafaulu kwa hali ya juu tukawaweka peke yao. Sasa tuna mjadala kama hilo kweli ni sahihi au tuwachanganye na wenzao katika shule za kawaida ili waweze kusaidiana vizuri zaidi. Tutakapofikia mwisho wa mjadala huo tutafanya uamuzi na tunafurahi kupata changamoto. *(Makofi)*

Na. 256

**Matumizi ya Maneno Taasisi, Maonyesho na Tahadhari**

**MHE. SALOME J. MBATIA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa zaidi ya miaka 20 tumekuwa tukitumia maneno ya Kiswahili kama vile taasisi, maonyesho, tahadhari na kadhalika ambayo sasa yanatumika kama asasi, maonesho na adhari:-

(a) Je, ni nini tofauti ya maneno hayo?

(b) Je, ni nani mwenye mamlaka ya kuunda maneno ya Kiswahili nchini?

(c) Je, kwa nini maneno hayo yamekuwa yakitumika kwa zaidi ya miaka 20 bila mamlaka husika kusahihisha kasoro hizo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maana na matumizi ya maneno taasisi na asasi, maonyesho na maonesho, tahadhari na hadhari, nadhani neno ni hadhari maana neno adhari alililoliandika Mheshimiwa Mbunge katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu halimo, kwa hiyo, tunadhani alimaanisha neno hadhari. *(Kicheko)*

(i) Mheshimiwa Spika, taasisi na asasi ni maneno mawili tofauti. Taasisi mana yake ni sehemu, Chuo au Idara ya Chuo Kikuu, Wizara au Shirika inayoshughulika na utafiti au mafunzo au mtaala wa jambo mahsusi kwa mfano Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Taasisi ya Elimu Tanzania, Taasisi ya Malaria na Magonjwa ya Tropiki au Taasisi ya Wanyama Pori na tafsiri ya Kiingereza ya neno hili taasisi ni *institute.* Asasi maana yake ni utaratibu, desturi, mila mfumo au kitengo cha mfumo ambao umedumu katika jamii kwa muda mrefu na unakubalika kama sehemu muhimu katika jamii husika. Vile vile asasi ni chombo kinachotoa huduma za ama kielimu, kijamii au kifedha ndani ya jamii husika. Tafsiri ya Kiingereza ya neno asasi ni *institution.*

(ii) Maonyesho na maonesho ni maneno mawili yenye maana moja katika Kiswahili Sanifu na yanakubalika kutumika. Maneno hayo yanatokana na maneno ONA na ONYA ambayo yana maana ya kumwezesha mtu ama aone kwa macho (ONA) au kwa akili (ONYA) au njia zote mbili. Jambo linalopaswa kusisitizwa katika matumizi ya maneno hayo ni kwamba mtumiaji akichagua kutumia moja asichanganye na kutumia la pili katika muktadha ule ule au katika andiko lile lile ukiamua kutumia moja utumie hilo hilo moja.

(iii) Tahadhari na hadhari, tahadhari ni kuepuka jambo la hatari au baya kutokea kwa mfano unaweza kusema Watanzania hawana budi kutahadhari wasiambukizwe Ukimwi kwa kubadili tabia zao. Hadhari ni uangalifu au hatua zinazochukuliwa ili hatari au ubaya usitokee. Kwa mfano unaweza kusema

kubadili tabia ni hadhari muhimu ili kutoambukizwa Ukimwi. Hivyo kutahadhari ni kutenda na hadhari ni hiyo hatua inayochukuliwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na.27 ya mwaka 1967, ndilo lenye mamlaka ya kuandaa istilahi yaani maneno yanayotumika katika nyanja maalum na kuhakikisha kuwa maumbo ya maneno yanayoundwa yanazingatia kanuni za mfumo wa maumbo ya maneno ya lugha ya Kiswahili. Kwa kushirikiana na asasi mbalimbali za ukuzaji Kiswahili pamoja na wataalamu wa nyanja zinazohusika maneno hayo hupitishwa rasmi yaani husanifishwa na kuidhinishwa yaanze kutumika.

(c) Mheshimiwa Spika, Baraza la Kiswahili la Taifa limekuwa likifanya jitihada za kuhimiza matumizi sahihi ya maneno ya Kiswahili kwa njia ya:-

(i) Redio Tanzania Dar es Salaam ambayo hutangaza kipindi cha Lugha ya Taifa kila juma na *Radio One* siku hizi hutangaza kipindi cha Lugha ya Kiswahili kila Jumamosi. *(Makofi)*

(ii) Kuyapatia magazeti mbalimbali ya Kiswahili kwa lengo la kubaini na kuchanganua makosa au matumizi yasiyo sahihi na kuwasiliana na wahariri wa magazeti hayo ili wafanye marekebisho.

(iii) Kuandaa makala mbalimbali kuhusu matumizi sahihi ya maneno na semi na kuchapisha katika magazeti kwa manufaa ya watumiaji wa Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, mbali na jitihada hizi, makosa yanaendelea kufanywa na watumiaji wa Kiswahili kwa sababu kuu mbili:-

(i) Kwanza, watumiaji kuwa wagumu kuacha matumizi yasiyo sahihi kutokana na mazoea hata humu Bungeni. *(Kicheko)*

(ii) Pili, watumiaji kutojielimisha vya kutosha na hivyo kushindwa kwenda bega kwa bega na ukuaji wa Kiswahili katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mathalani baadhi ya watumiaji bado inawawia vigumu kutofautisha matumizi ya maneno kama vile kuwasilisha na kuwakilisha, kudhibiti na kuthibiti au kupambanua kwamba nguvu, nishati na kani yanawakilisha dhana tofauti ingawa dhana hizo zinahusiana.

Mheshimiwa Spika, samahani kwa kutoa mhadhara. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ndiyo, tumepata semina nzuri ya Kiswahili.

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Baraza la Kiswahili ndio lenye mamlaka ya kusimamia Kiswahili nchini na kwa kweli limekuwa liki-*propagate* kwamba Kiswahili kinaweza kutumika katika nyanja yoyote ile na hata kutumiwa shuleni na kwa kuwa Waziri ni mmoja wa watu ambaye anasema kwamba Kiswahili hakijafikia hatua ya kutumika shuleni, je, Waziri anatuambia nini baada ya kufanya utafiti kidogo wa suala hili na kuona kwamba kwa kweli Kiswahili ni kipana na kimekomaa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, suala la Kiswahili kutumika shuleni, kwanza napenda nirekebishe jambo hili kwamba katika miaka ambayo kijana wa Kitanzania anakuwa shuleni ukichukua miaka miwili ya elimu ya awali, miaka saba ya elimu ya msingi inakuwa miaka tisa, miaka minne ya Elimu ya Sekondari ya kawaida jumlisha miwili ya elimu ya juu ni sita na ukiweka ya Chuo Kikuu mitatu ni tisa au kama ni minne Chuo Kikuu kwa *Degree* za miaka nne basi inakuwa kumi. Kwa hiyo, kwa ujumla unaweza kusema watoto wetu kwa miaka tisa ya mwanzo nusu nzima ya safari yao ya kupata elimu wanaifanya kwa lugha ya Kiswahili, lugha ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utumiaji wa Kiingereza katika ngazi ya Sekondari ambayo hivi karibuni imekuwa na mjadala, mimi kama Waziri wa Elimu, Sheria ya Elimu iliyotungwa na Bunge hili

inasema lazima ninapofanya uamuzi wa mambo ya elimu kila wakati nizingatie matakwa ya Watanzania, nawajibika kuzingatia Watanzania wanataka nini.

Mimi sijaona ndani ya jamii ya Watanzania leo kwamba wanataka tubadilishe utumiaji wa lugha ya kufundishia katika ngazi ya Sekondari na Chuo Kikuu iwe ya Kiswahili badala ya Kiingereza ndio maana sithubutu kuamua. Lakini pia mimi kama miongoni mwa jumuiya ya wasomi wa nchi hii kwa sababu nimesoma... *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba pamoja na Kiswahili kuwa lugha ya Taifa lakini Kiingereza ndio Kiswahili cha dunia ya utandawazi. Kwa hiyo, sioni kama itakuwa ni busara kuanza kutumia Kiswahili katika ngazi ya Sekondari na Chuo Kikuu kuelimisha watoto wetu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Nimeshatamka tunaendelea na maswali kwa Wizara nyingine, tafadhali kaeni chini.

Na. 257

**Kupeleka Umeme Ihanja**

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA (k.n.y. MHE. MOHAMED H. MISSANGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipojibu swali Na.84 katika Mkutano wa Bunge wa Januari/Februari, 2001 iliahidi kuwa itawapatia umeme wananchi wa Ihanja kabla ya kumalizika kwa mwaka 2002:-

(a) Je, ni sababu zipi zilizofanya Serikali isitekeleze ahadi yake ya kuwapatia wananchi hao umeme hadi leo hii?

(b) Je, ni lini sasa wananchi hao watapatiwa umeme hasa ikizingatiwa kuwa tangu nguzo za umeme zipelekwe ni takribani miaka 5 sasa lakini hazijachimbiwa na isitoshe baadhi yake zimechukuliwa na kupelekwa Manyoni?

(c) Kwa kuwa shule ya Sekondari ya Ufundi ya Ihanja imepata wafadhili kutoka Marekani ambao wameahidi kuwapatia vifaa kadhaa vya kufundishia masomo ya ufundi ikiwa ni pamoja na kompyuta kwa sharti kuwa lazima shule iwe na umeme; je, Serikali haioni kuwa upo umuhimu wa kuharakisha kupeleka umeme Ihanja ili wafadhili wasikate tamaa kutoa misaada iliyokusudiwa na kwa kufanya hivyo, shule hiyo iweze kunufaika na msaada huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme Shule ya Sekondari ya Ihanja ilikuwa ifanyike wakati wa utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Manyoni na Ihanja ilikuwa inufaike na utekelezaji wa mradi huu sambamba na vijiji vingine vya njiani vinavyopatiwa na njia ya umeme iliyojengwa kwenda Manyoni? Mradi huu ulitekelezwa katika awamu tatu kutokana na ufinyu wa fedha zilizokuwa zimepatikana kama ifuatavyo:-

Awamu ya kwanza ilikuwa ni kufikisha umeme Puma, awamu ya pili kufikisha umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Manyoni na awamu ya tatu ilikuwa kupeleka umeme kwenye mji wa Itigi na vijiji vya njiani. Upelekaji umeme kwenye vijiji vya njiani ulizingatia zaidi ziada ya fedha zilizobaki kwenye fungu lililotengwa wakati wa utekelezaji wa mradi wa umeme kwenda Manyoni.

Wakati wa ujenzi wa njia ya umeme wa awamu ya pili, nguzo zilihifadhiwa Puma, Kaminyanga na Manyoni ili kurahisisha ujenzi. Hata hivyo kabla ya awamu ya tatu kukamilika fedha zilikwisha na hivyo vijiji vingine kikiwepo kijiji chenye Sekondari ya Ihanja havikuweza kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, ni kweli nguzo zilizokuwa zimebaki Puma zimekuwa zikitumiwa kwa shughuli mbalimbali za kuimarisha njia ya umeme iendayo Manyoni ikiwemo ya kubadilisha nguzo zilizochakaa. Hii ni hali ya kawaida kwa kuwa nguzo hizo zililetwa kwa ajili ya mradi wa Manyoni.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kutafuta fedha za kuipatia umeme Shule ya Sekondari Ihanja ili iweze kunufaika pia na vifaa vilivyoahidiwa na mfadhili. Serikali itaendelea kutafuta fedha hizo kiasi cha shilingi milioni 216.7 ili shule hiyo ipate umeme.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwanza naishukuru Wizara ya Nishati na Madini, kwa kuhakikisha umeme umefika katika miji ya Manyoni na Itigi.

Kwa umeme katika miji hii ulifika toka mwaka 1999 na kwa kuwa hivi sasa nguzo nyingine zimeanza kufika na zipo nyingi tu pale Mkoani Singida je, isingekuwa busara Wizara kupitia Shirika lake la *TANESCO* likaanza kusomba nguzo toka pale Singida Mkoani na kuzipeleka kutokea Puma kwenda Ihanja ili shule hii iweze kupata umeme haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 1999 mpaka mwaka 2001 suala hili la umeme Ihanja pamoja na Ikungi liliulizwa na tulijibu hapa Bungeni kwamba tulikuwa tukitafuta fedha. Katika muda huo, tuliweza kupata fedha za kufikisha umeme Ukungi. Kwa hiyo, tumebakiwa na Ihanja. Kama nilivyosema awali, tunaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya Ihanja. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jitihada hizi zitakapofanikiwa tutapeleka umeme kwenye Shule hii ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda niseme kwamba kuwepo kwa nguzo pekee yake hakutoshi kukamilisha mradi huu. Usambazaji wa umeme unahitaji vifaa sio nguzo tu bali nyaya, vikombe na vifaa vingine. Kama nilivyosema gharama nzima ya kupeleka umeme kwenye shule hii ni shilingi milioni 216, tunaendelea kutafuta fedha hizo.

Na. 258

**Matumizi ya Makaa ya Mawe Majumbani**

**MHE. OSCAR T. MLOKA** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu imejaliwa kuwa na machimbo ya makaa ya mawe ambayo ni nishati mbadala inayoweza kulileta Taifa Pato zuri la nje na ndani na kwa kuwa wananchi wengi hasa waishio mijini huhatarisha nchi yetu kugeuka jangwa kutokana na kukata miti ovyo ya kuni na uchomaji wa mkaa kwa matumizi ya majumbani.

Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika wa kuwapa elimu na kuwahamasisha wananchi watumie makaa ya mawe kama nishati mbadala?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Mloka, Mbunge wa Morogoro Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Oscar Mloka, kuwa kasi ya nchi yetu kugeuka kuwa jangwa kwa kiwango fulani inachangiwa na matumizi makubwa ya kuni na mkaa. Pia, kama ambavyo niliwahi kutoa maelezo kupitia jibu la swali Na. 965, katika Bunge lako hili, nakubaliana pia na Mheshimiwa Mbunge kuwa Tanzania inayo hazina kubwa ya makaa ya mawe. Hazina ya makaa ya mawe inakisiwa kuwa zaidi ya tani milioni 330 na iko katika maeneo kadhaa ya nchi ikiwemo Mikoa ya Ruvuma, Iringa, Mbeya na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kutafiti na kuendeleza teknolojia sahihi za kutumia makaa ya mawe zikiwemo za kupikia na matumizi ya viwandani. Teknolojia kadhaa zimejaribiwa na wadau mbalimbali ukiwemo Mgodi wa Kiwira na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hata hivyo, matokeo yameonyesha haja ya kuboresha zaidi teknolojia hizo ili zikubalike zaidi hususan kijamii na kimazingira.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Kampuni binafsi ya *Kyela Valley* kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Nishati na Madini, imefanikiwa kupata majiko 320 na matofali 6,400 ya makaa ya mawe yaliyotengenezwa huko China kwa kutumia makaa ya Kiwira. Majiko na matofali hayo yameanza kufanyiwa maonesho katika baadhi ya maeneo kwa ajili ya kupikia na kukaanga samaki ili kuona kama majiko na vitofali hivyo vinakubalika kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya upembuzi yakinifu kukamilika, hatua muafaka zitachukuliwa ili kuweka utaratibu wa kuzalisha majiko na vitofali vya makaa ya mawe hayo hapa nchini. Endapo utaratibu huu utakamilika, makaa ya mawe hayo yatatoa mchango mkubwa kwa upatikanaji wa nishati mbadala majumbani.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza. Tunafahamu fika kwamba moto wa mkaa wa mawe ni mkali kiasi kwamba hakuna sufuria ambayo inaweza ikahimili joto lake. Lakini nchi za Asia inaelekea zinatumia vumbi la huu mkaa wa mawe kwa matumizi ya majumbani. Je, utaalam huo hauwezi ukaigwa na nchi yetu kama nishati mbadala hasa Mijini ili kunusuru kuangamia kwa misitu yetu kwa kutumia kuni?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kabisa kwanza moto wa makaa ya mawe ni mkali zaidi kuliko moto wa mkaa wa kawaida au moto unaotokana na miti. Pia nakubaliana naye kwamba teknolojia ya kutumia vumbi la makaa ya mawe ambayo sasa hivi inatumika katika baadhi ya nchi hapa duniani hususan Uchina ingeweza kufaa kabisa katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na nishati hii mbadala ya makaa ya mawe. Napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba jana Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia katika hotuba yake ya Bajeti hapa Bungeni alizungumzia katika ukurasa wa 24 suala zima la kufanya utafiti wa matumizi ya teknolojia ya kutumia makaa ya mawe majumbani kwa kutumia vumbi linalopatikana Kiwira.

Mimi napenda kusema kwamba hii inawezekana kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na ndiyo maana Serikali imejizatiti kufanya utafiti katika eneo hili ili kuhakikisha kwamba teknolojia hii inafanikiwa na inatumika hapa nchini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yamejibiwa yote. Matangazo ya vikao kuna tangazo moja tu. Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na kikao leo saa tano na nusu asubuhi katika chumba cha Kamati namba 56.

Vile vile kuna tangazo linasema nakuomba uwatangazie Wabunge wanawake wote wa CCM kuwa leo baada ya kuahirisha Bunge saa saba kutakuwa na kikao. Mwisho wa matangazo. Katibu tuendelee na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004
### Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, ambayo ndiyo inayohusu Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa mwaka wa Fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kuishukuru kwa dhati Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, iliyochambua kwa makini malengo na makusudio ya Bajeti ya Wizara hii na hatimaye kuafiki na kuipitisha kifungu kwa kifungu. Mchango uliotolewa na Kamati kwa ujumla wake pamoja na ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo vimesaidia sana kuiboresha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, majukumu makubwa ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ni kusimamia suala zima la utoaji haki kwa wananchi, kuhakikisha kwamba sheria na taratibu za nchi zinafuatwa, kuishauri Serikali kuhusu masuala ya Sheria kwa lengo la kudumisha utawala bora, amani, utulivu na ustawi wa jamii, hali ambayo ni muhimu kwa maendeleo nchini, kurekebisha sheria ili ziende na wakati, kusajili vizazi, vifo, ndoa na wadhamini, kusimamia suala Katiba na haki za binadamu. Majukumu ya Wizara yamepanuka sana katika miaka ya karibuni baada ya nchi yetu kuingia katika mfumo wa uchumi wa soko huria na utandawazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba imejizatiti kutekeleza majukumu ya Wizara yakiongozwa na Dira ya haki kwa Wote na kwa Wakati. Lengo la Dira hii ni kuleta maendeleo ya Haki ya Kijamii, kudumisha Usawa na Utawala bora, utawala wa Sheria kutokana na kuwepo kwa huduma bora za kisheria zitakazopatikana kwa wote na kwa muda muafaka. Wizara hii imekwishaweka mkakati wa kujenga mfumo wa sheria ambao utakidhi mahitaji mapya ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na maendeleo ya kisayansi ndani ya nchi na kutokana na mahusiano na nchi zingine.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2002/03, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ilijitahidi kutekeleza majukumu yake ya utoaji haki kwa wote na kwa wakati kwa lengo la kudumisha utawala bora. Wizara ilipanga kutekeleza majukumu yake ikizingatia pia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, nilielezea Bunge lako Tukufu mikakati na jiitahada za kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani kwa lengo zima la kupunguza mlundikano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza nchini, tatizo ambalo limekuwa ni sugu na lenye kuathiri haki na kusababisha mzigo kwa Serikali. Katika kushughulikia tatizo hilo, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ilichukua hatua zifuatazo:-

Kuongeza nguvukazi katika Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu ambapo waliteuliwa Majaji wawili wa Mahakama ya Rufani na sita wa Mahakama Kuu. Aidha, Serikali imetoa kibali cha kuajiri Mahakimu Wakazi 75, Mawakili wa Serikali 36 na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 84 na utaratibu wa ajira unaendelea.

Utaratibu wa Kamati za kusukuma kesi *(Case Flow Management)* uliendelea kuimarishwa katika ngazi zote za Mahakama. Kuongeza idadi ya vikao vya Mahakamu Kuu na Mahakama ya Rufani. Vikao vya Mahakama ya Rufani vilifikia saba mwaka 2002/2003 ikilinganishwa na vikao vitano mwaka 2001/2002 na kwa Mahakama Kuu vilifanyika vikao 59 mwaka 2002/2003 ikilinganisihwa na vikao 33 mwaka 2001/2002. Aidha, Mahakama za Mahakimu Wakazi, Wilaya na Mahakama za Mwanzo ziliweza kuendesha shughuli za Kimahakama nyingi zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 2001/2002.

Rasimu ya muundo mpya wa Idara ya Mahakama wenye lengo la kuimarisha utendaji kazi na kudumisha maadili mema ya watumishi wa Mahakama umewasilishwa Serikalini kwa maamuzi.

Katika kuimarisha utoaji haki kwa kundi maalum la watoto, taratibu za kiufundi za ujenzi wa Mahakama za Watoto Mbeya na Mtwara na upanuzi wa Mahakama ya Watoto Kisutu unaendelea kukamilishwa kwa kushirikiana na wafadhili watakaogharamia ujenzi huo.

Pia kuongeza uwezo wa Mahakama za Mahakimu kusikiliza mashauri. Sasa Mahakama za Mahakimu Wakazi zinao uwezo wa kusikiliza mashauri ambayo thamani ya mali husika inafikia shilingi milioni 100 kwa mali inayohamishika kutoka shilingi milioni kumi na shilingi milioni 150 kwa mali isiyohamishika kutoka kiasi cha shilingi milioni 12.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mahakama iliendesha semina kwa Mahakimu Wakazi na wa Wilaya juu ya namna ya kushughulikia suala la kuamua aina ya adhabu zinazotolewa kulingana na makosa ya washtakiwa baada ya kutiwa hatiani. Mafanikio ya semina hiyo yamejitokeza kwa kupungua kidogo misongamano ya wafungwa katika baadhi ya Magereza.

Idara ya Mahakama imewasilisha Serikalini mapendekezo ya kutungwa sheria itakayotamka bayana muda wa maamuzi ya Mahakama kutolewa baada ya taratibu zote za usikilizwaji wa kesi kukamilika.

Mheshimiwa Spika, suala la kuimairisha ubora wa kazi halijafumbiwa macho na Wizara hii. Ukaguzi wa Mahakama umeanza kuimarishwa kwa kuwapatia watendaji vifaa vya kisasa na vyombo vya usafiri ambapo taratibu za ununuzi wa magari 11 ulikuwa unakamilishwa. Magari hayo yatasambazwa kwenye Kanda kwa ajili ya ukaguzi.

Vile vile ofisi zote kumi za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali zilikaguliwa. Ofisi hizo zimepatiwa vitendea kazi vipya ambavyo ni kompyuta na kila Kanda ina gari moja kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake. Kwa ujumla, suala la kuimarisha vitendea kazi limepewa umuhimu mkubwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kupambana na kero ya rushwa ndani ya Idara ya Mahakama, kila Mahakama nchini imeagizwa na Jaji Mkuu kuweka sanduku la maoni au malalamiko kwenye jengo lake kwa matumizi ya wananchi kufikisha maoni au malalamiko yao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, nilieleza juu ya unazishwaji wa Mahakama ya Ardhi ikiwa ni moja ya mikakati ya kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani. Mahakama hii ilianzishwa rasmi kisheria kwa Tangazo la Serikali Na. 64 la tarehe 4 Mei, 2001. Kuanza kazi ya kusikiliza mashauri katika Mahakama hii kunasubiri kukamilishwa kwa taratibu na kanuni za kuendesha na kusimamia usikilizaji wa mashauri ili kuhakikisha kuwa mashauri ya migogoro ya ardhi yanashughulikiwa kwa wakati na katika mazingira ya haki na uwazi.

Napenda kulifahamisha Bunge hili Tukufu kuwa taratibu hizo sasa zimekamilika na zipo katika hatua ya uchapaji. Hivyo, Mahakama hiyo itaweza kuanza kazi zake hivi punde.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mahakama ya Biashara, iliendelea kutekeleza kikamilifu majukumu yake katika kipindi kilichopita cha mwaka 2002/03. Mahakama hii ilisajili jumla ya kesi 351 za biashara ikilinganishwa na kesi 344 kwa mwaka 2001/2002.

Kesi zilizosikilizwa na kumalizika mwaka 2002/2003 zilikuwa 234 ikilinganishwa na kesi 227 zilizomalizika mwaka 2001/2002. Hali hii inaonyesha ongezeko kidogo la kesi zilizofunguliwa na kusikilizwa katika mwaka 2002/2003. Hali kadhalika muda uliotumika kumaliza kesi ulikuwa miezi mitano mwaka 2002/03 ikilinganishwa na miezi mitatu kwa mwaka 2001/2002.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya kuongezeka kwa muda wa wastani wa kumaliza kesi ni kutokana na kurejeshwa kwa kesi za mwaka 2000 na 2001 kuendelea kusikilizwa tena na Mahakama hii wakati idadi ya Majaji iliendelea kubakia ile ile.

Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha sheria mbalimbali kurekebishwa ili ziende na wakati, shughuli za utafiti wa sheria ziliendelea kutekelezwa kwa ufanisi wa kuridhisha. Tume ya Kurekebisha Sheria ilifanya utafiti wa kuchambua na kuainisha sheria na taratibu za sheria na kutoa mapendekezo ya kuzifanyia marekebisho. Tafiti na rejea za sheria hizo ambazo zimefikia hatua ya kuchapishwa na kuwasilishwa Serikalini ni zile zinazohusu usalama barabarani na sheria ya sekta ya utalii. Kazi hiyo imekamilika na kesho tunatarajia kukabidhiwa ripoti hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, sheria nyingine zinahusu sekta ya Madini na ile inayohusu Mtiririko wa Utendaji Haki. Tafiti za sheria zinazoendelea kufanyika katika kipindi hiki ni zile zinazohusu sheria za Majeshi ya Polisi na Magereza, Sheria za Kilimo na Mifugo, Sheria zinazohusu uwakilishi kwa kutumia Wanasheria Wasaidizi katika Mahakama za chini *(para-legal project)* na sheria za sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa sheria za Mirathi, Ndoa na Watoto ulifanywa na Tume ya Kurekebisha Sheria na kisha kuwasilishwa Serikalini. Mapendekezo yaliyotolewa yalifanyiwa kazi na Wizara kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kazi ya uchambuzi imekamilika na hivyo, mara maamuzi yatakapochukuliwa na Serikali tutawasilisha Miswada ya Sheria husika Bungeni hivi karibuni baada ya Serikali kufanya maamuzi ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, Miswada ya Sheria inayotungwa na Bunge iliandaliwa pamoja na sheria ndogo ndogo zinazotungwa na mamlaka mbalimbali za sheria na baadhi zilitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Vile vile katika jitihada za kuhakikisha upatikanaji wa Miswada na Sheria za Serikali kwa wakati muafaka, Wizara ilizingatia mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu kila Wizara kuwa na *Legislative Programme.* Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba inaratibu programu hii kuiwezesha Idara ya Uandishi wa Miswada kuzifahamu *Legislative Programmes* za Wizara zote na hivyo kufanyia kazi Miswada hiyo katika wakati muafaka. Katika kipindi cha mwaka 2002/03, Wizara imeandaa na kuchapisha jumla ya Miswada 22.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kurekebisha sheria na kutoa toleo la vitabu vya sheria zilizofanyiwa marekebisho yote yaliyofanyika hadi kufikia Julai, 2002 ambayo imeendelea kwa muda mrefu sasa karibu inafikia mwisho. Tarehe 30 Juni, wachapaji wa sheria hizo watakuwa tayari kuanza kutoa sura 418 za sheria kwa kuanza na toleo la kwanza hadi la ishirini. Tunategemea sasa kazi ya kuanza kutoa matoleo hayo ya sheria itazinduliwa mwezi Agosti, 2003.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imeendelea kuishauri Serikali katika mashauri ya madai na kuiwakilisha katika kesi zinazoikabili. Pia Wizara iliendelea kuiwakilisha Serikali katika majadiliano na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Mfuko wa *OPEC* katika kupata mikopo nafuu kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Aidha, Wizara iliendelea kushiriki kuiwakilisha Serikali katika Jumuiya za Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Ushirikiano wa Afrika Mashariki *(EAC)* katika vikao vyake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara hii iliendelea kutoa ushauri kwa Serikali, Idara na Taasisi zake ili kuhakikisha kwamba zinazingatia Mikataba ya Kimataifa juu ya haki za binadamu. Vile vile taarifa za utekelezaji wa haki za binadamu ziliaandaliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na kuwasilishwa kwenye Kamati za Haki za Binadamu za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na mageuzi ya kiuchumi na kisiasa yanayoendelea hapa nchini na pia kwa kuzingatia taarifa za Kamati na Tume mbalimbali na bila kusahau maoni ya wananchi katika kongamano, warsha na semina mbalimbali, Wizara imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Katiba ya Nchi ambayo yatawasilishwa Serikalini kwa uamuzi. Kwa upande wa suala la kuboresha na kuimarisha mahusiano baina ya vyombo vya kutoa haki na vya utawala, Wizara ilitekeleza wajibu huu kwa kutoa ushauri wa kisheria katika mambo ya Kikatiba. Hatua hii iliwezesha kuboresha na kuimarisha demokrasia na huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza, kuimarisha na kuboresha Haki za Binadamu na misingi ya utawala bora, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, kwa kupitia Tume ya Haki za binadamu na Utawala Bora, ilichukua hatua mbalimbali zikiwemo kupokea na kufanya uchunguzi wa malalamiko na tuhuma mbalimbali zinazohusu ukiukwaji wa Haki za binadamu na msingi ya utawala bora. Tume imepokea malalamiko zaidi ya 5,000. Kati ya hayo, zaidi ya malalamiko 2000 uchunguzi wake umekamilka na mengine yanafanyiwa kazi. Aidha, hatua nyingine iliyochukuliwa ni kuweka mkakati wa kutoa elimu juu ya haki za binadamu na msingi ya utawala bora kwa viongozi mbalimbali wa Serikali wakiwemo Wenyeviti wa Vijiji, Watendaji wa Kata na Makatibu Tarafa ambao ndio wanaosimamia masuala ya kanuni za utawala bora huko Vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake hayo, Tume ilitembelea Mikoa yote ya Tanzania Bara isipokuwa Dar es Salaam ambako ilikuwa na Sekretariati za Mikoa na viongozi mbalimbali ili kujitambulisha kujenga mahusiano na kuelezea majukumu yake. Hali kadhalika, Tume ilikutana na viongozi na Wawakilishi wa Asasi zisizo za Kiserikali ili kujenga mahusiano na asasi hizo na kutumia mtandao na ujuzi wao kuelimisha wananchi kuhusu masuala ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Aidha, Tume imetembelea Magereza yote ya Mikoa ya Tanzania Bara na baadhi ya Magereza ya Wilaya. Tume pia iliendesha semina kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa lengo hilo hilo. Katika Mkutano huu wa Bunge letu Tukufu Tume imeendesha pia semina kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kwa dhati kuimarisha hadhi ya vyombo vya utoaji haki. Kwa kuelewa umuhimu wa sekta ya sheria, Serikali imekuwa ikiongeza kwa kasi Bajeti ya Wizara na asasi zake. Katika mwaka wa fedha 1997/1998, Serikali iliipatia Wizara jumla ya shilingi 4,622,059,800/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Mwaka huu tunategemea kupatiwa kiasi kinachokaribia shilingi 32 bilioni. Naamini Serikali yetu itaendelea kuongeza Bajeti ya Wizara ili iweze kukidhi kutekeleza majukumu yake kikamilifu hasa baada ya kuwa na matatizo ya fedha kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha hadhi ya vyombo vya utoaji haki nchini, Wizara ilitekeleza na kufanikisha yafuatayo:-

Ujenzi wa jengo la makao ya kudumu kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora pamoja na Tume ya Kurekebisha Sheria ulikamilika na jengo kuhamiwa. Jengo hilo tulilolijenga kwa msaada wa Serikali ya Denmark na kupewa jina la *HAKI HOUSE* lilifunguliwa rasmi na Makamu wa Rais kwa niaba ya Mheshimwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Aprili, 2003.

Jumla ya Mahakimu 600 wa Mahakama za Mwanzo, 300 wa Mahakama za Mahakimu Wakazi na Majaji 34 wa Mahakama Kuu na Mahakama za Rufani walipatiwa mafunzo katika taasisi za elimu hapa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 200/03, nilizungumzia pendekezo la kisera la kuimarisha na kuipanua Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kuondoa uendeshaji wa kesi za jinai kutoka Idara ya Polisi ili Mkurugenzi wa Mashtaka ndiye asimamie jukumu hili moja kwa moja. Utekelezaji wa ahadi hii bado unafanyiwa kazi kuzingatia uwezo wa kifedha wa Serikali.

Aidha, katika suala zima la kuimarisha mipango ya muda mrefu ya Wizara, Idara mpya ya Sera, Mipango na Habari ya Wizara imekwishaanzishwa kwa ajili ya uchambuzi wa sera, upangaji wa mipango na kuratibu shughuli zote za maendeleo ya Wizara na Idara zake kwa kuzingatia sera za mageuzi ya sekta mbalimbali nchini ikiwemo sekta ya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inatekeleza programu ya kurekebisha sekta ya Sheria ambayo inaunganisha nguvu za Serikali, wananchi na wafadhili kwa ajili ya kutatua matatizo sugu yanayoikabili sekta ya sheria nchini pamoja na kuongeza uwezo wa nchi yetu kutoa haki kwa wananchi wote kwa wakati. Katika programu hiyo Wizara imeanzisha mradi wa *Quick start* wenye malengo makuu matatu ambayo ni kuhuisha na kuboresha taratibu na kanuni zinazosimamia sekta ya sheria kwa kuandaa mkakati wa mafunzo ya wafanyakazi ili kuboresha usimamizi wao wa kazi, kuboresha mfumo wa haki wa watoto watukufu na majaribio ya kuboresha Mahakama za Mwanzo, Wilaya na za Hakimu Mkazi zinazotoa haki kwa wananchi walio wengi na makusanyo na matumizi ya sehemu ya mapato inayotengwa kugharamia utoaji huduma *(Retention schemes).*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza malengo hayo, tayari Wizara imekwisha kushughulikia mambo yafuatayo:-

Kukamilisha marekebisho ya mkakati wa muda wa kati ili uzingatie programu nyingine za Kitaifa, kama vile programu ya kurekebisha sekta ya umma, mpango wa kurekebisha Serikali za Mitaa, Mkakati wa kuondoa umaskini na mkakati wa kupambana na rushwa.

Kuajiri washauri kwa ajili ya kuchambua viwango vya elimu ya wafanyakazi, kuainisha mahitaji ya mafunzo, kuandaa mkakati wa kukusanya raslimali kwa ajili ya kujenga miundombinu na uwezo wa kutoa haki sawa kwa wote, kuainisha mfumo wa utawala unaofaa katika sekta ya sheria na kusimamia ujenzi wa Mahakama za watoto Mbeya na Mtwara na ukarabati wa baadhi ya Mahakama za Watoto kama vile Mahakama ya Kisutu.

Katika mwaka wa fedha uliopita, Wizara imepiga hatua kubwa katika kukamilisha mradi wa kuboresha Mahakama ya Mwanzo, Wilaya na za Mahakimu Wakazi. Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tarehe 20 Januari, 2003 Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua mradi wa majaribio katika Mahakama za Mwanzo za Mikoa ya Arusha na Manyara. Kama nilivyoeleza, mradi huu unawashirikisha wadau wengi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwapongeza wananchi wa Mikoa hiyo kwa hatua walizochukua kugawana majukumu mbalimbali ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anafahamu majukumu yake vizuri na kwa ari kubwa walioonyesha na michango wanayoendelea kutoa ya fedha, mchanga, matofali, mawe, kokoto na nguvu zao. Jitihada zitafanyika kuhakikisha kwamba mafanikio yanayopatikana katika Mikoa ya Arusha na Manyara yanasambazwa katika Mikoa mingine.

Aidha, Wizara kwa ushirikiano wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itaitisha kikao cha Wakuu wa Mikoa wote hapa nchini mwaka 2004 ili kutathmini mafanikio hayo na kupeana mkakati wa kusambaza mafanikio hayo nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kadri ya uwezo wa kifedha ulivyoruhusu, tulijielekeza katika kuimarisha hadhi ya Mahakama zetu pamoja na mfumo mzima wa utoaji haki nchini kwa kuyakabili matatizo ya ukosefu wa vitendea kazi, majengo machakavu ya Mahakama, hata ukosefu wa majengo hayo ya Mahakama katika sehemu nyingine, mafunzo yasiyokidhi mahitaji pamoja na mawasiliano hafifu.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kukamilisha maandalizi ya mradi wa *Accountability Transparency and Integrity Project(ATIP)* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuboresha majengo ya Mahakama, kujenga taasisi ya kutoa mafunzo kwa wanasheria wahitimu *(Law School)* na kuongeza ufanisi katika mawasiliano. Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara itaongeza juhudi za kupata ushirikiano wa wabia wa maendeleo na kuwashawishi waongeze msaada wao katika utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara ilifanya juhudi kubwa katika kuhakikisha kuwa mazingira ya kazi yanaboreshwa ili kuongeza ufanisi wa utendaji. Wizara ilinunua vitendea kazi kama vile kompyuta na *printers* zake kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Makao Makuu na Ofisi zote za kanda. Magari yalinunuliwa kwa ajili ya Kanda ya Dar es Salaam na Moshi. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya mafunzo ya muda mfupi ya ndani na nje ya nchi. Jumla ya watumishi 88 wamenufaika na mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na wengine 22 walipata mafunzo ya muda mfupi, Nane mafunzo ya masjala ya Sheria na 49 walipewa mafunzo ya maadili ya kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza ahadi nilizozitoa mwaka 2002/2003, Wizara hii imeendelea kukabiliwa na matatizo ambayo yameendelea kuathiri ufanisi wa utendaji katika shughuli nzima ya utoaji haki. Mengi ya matatizo yanatokana na ufinyu wa bajeti. Baadhi ya matatizo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kushindwa kufanya ukarabati wa Mahakama ya Rufani, zabuni ya ukarabati wa jengo hilo haikutangazwa kutokana na ufinyu wa Bajeti, ingawa kazi za usanifu na ukadiriaji wa gharama za ujenzi zilikamilika. Hali hii imesababisha kuendelea kuwepo tatizo la ofisi na vyumba vya ofisi kwa ajili ya Majaji kwenye jengo la Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa vyombo vya usafiri na vitendea kazi kwa ajili ya watumishi wa Wizara umeendelea kuwepo, uhaba, ubovu na uchakavu wa majengo yanayotumika kwa ajili ya kufanyia shughuli mbalimbali za Wizara na Mahakama uliendelea kuwepo, ukosefu wa majengo kutokana na uwezo mdogo wa fedha kujenga ofisi mpya za kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mahakama ya Mwanzo, upungufu wa Mahakimu katika Mahakama, hasa Mahakama za Mwanzo, Kamati za nidhamu za Mahakama kushindwa kukaa ipasavyo na kushindikana kukamilisha zoezi la usambazaji wa mradi maalum wa usajili wa ndoa, vizazi na vifo chini ya mradi wa *Civil Registration Programme (CRP)* katika Wilaya ambazo hazijafikiwa na mradi huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea mafanikio na matatizo ya Wizara hii katika kipindi cha mwaka 2002/2003, sasa napenda nichukue fursa hii kuelezea mpango na malengo ambayo tunategemea kuyatekeleza katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004. Kwa ujumla, Wizara itaendelea kulenga kutekeleza Dira yake ya Haki kwa Wote na kwa Wakati. Utekelezaji malengo utazingatia utoaji wa haki kwa wote na kwa wakati, ushauri wa kisheria utawala bora, uwazi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuelezea mpango na malengo ya Wizara katika mwaka ujao wa fedha, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu juu ya umuhimu wa sekta ya sheria katika harakati za Serikali kuondoa umaskini. Sekta ya sheria inagusa kila sekta ya kiuchumi na ya jamii. Shughuli zote zinategemea bila kikomo sheria, taratibu za kisheria na utawala bora. Juhudi za kupunguza umaskini hutegemea sana amani, utulivu na uhakika wa usalama wa maisha na mali za wananchi. Upatikanaji ulio endelevu wa mambo hayo sharti uwepo ustawi wa mazingira ya utawala unaotokana na utawala wa sheria. Utekelezaji wa sera zote za kiuchumi na kijamii katika kuleta maendeleo ya nchi zinategemea sekta ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, utekelezaji wa malengo ya Wizara unalenga kuboresha mazingira yatakayowezesha na kupunguza matatizo ya utekelezaji wa sera zingine za kiuchumi na kijamii, hususan uwekezaji na uzalishaji mali ili kupunguza au kuondoa umaskini katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu, sera ya sekta ndiyo mwongozo wa kutekeleza majukumu mbalimbali ya sekta. Kwa msingi huo, mwaka ujao wa fedha Wizara imepanga kuanza maandalizi ya kutayarisha sera ya Taifa ya sekta ya sheria. Katika kutayarisha sera hiyo, Wizara itawahusisha wadau wote kwa lengo la kupata michango yao ya mawazo ambayo yataboresha uandaaji wa sera hiyo. Kutokana na umuhimu wake na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi yanayoendelea dunia kote, uandaaji wa sera hii utapewa umuhimu wa pekee ili ikamilike mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie mpango na maendeleo ya sekta ya sheria katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la mlundikano wa kesi Mahakamani pamoja na mlundikano wa wafungwa na mahabusu magerezani limekuwa kero kubwa kwa Serikali na wananchi kwa ujumla. Wizara hii kupitia Idara ya Mahakama na Idara ya Mkurugenzi wa mashtaka imepanga kufanya vikao nane vya Mahakama ya Rufani, vikao 80 vya Mahakama Kuu, kwenye Kanda 11 na kuendesha vikao vya kila siku vya kusikiliza mashauri kwenye Mahakama Kuu na Mahakama 21 na Mahakimu Wakazi, Mahakama za Wilaya 88 na Mahakama za Mwanzo 1,105.

Aidha Kamati za Kusukuma Kesi zitaimarishwa na zitafanya vikao vinne kwenye kila Kanda ya Mahakama Kuu, Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama ya Wilaya. Hali kadhalika utaratibu wa kumaliza kesi kwa njia ya usuluhishi na utaratibu wa kila Jaji na Hakimu kujipangia kalenda ya kusikiliza kesi kwa wiki, mwezi na mwaka utaendelea kutumika. Aidha, Ofisi mpya ya Kanda ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatarajiwa kufunguliwa Mkoani Kagera katika Mwaka huu wa fedha kwa lengo la kukabiliana na mlundikano wa kesi na kusogeza huduma ya sheria karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zitakazochukuliwa zitakuwa kuongeza wigo wa kazi ya Mahakama ya Biashara hadi Mkoa wa Arusha na Mwanza. Aidha, Mahakama ya Ardhi itaanza kufanya kazi yake ya kushughulikia migogoro ya ardhi nchini mwaka huu wa fedha. Lengo la Wizara ni kuiwezesha Mahakama hii kufanya kazi katika kanda zote za Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutoa msukumo mkubwa katika kuharakisha usilizaji wa kesi kwa lengo la kuondoa kero kwa wananchi na kuendeleza utawala bora, Wizara, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, itaanzisha Kamati ya Kitaifa ya kusukuma kesi ambayo wajumbe wake watatoka katika vyombo vyote vya sheria na usalama. Jukumu kubwa la Kamati hii litakuwa kusimamia kutoa miongozo na ushauri kwa viongozi wakuu wa Idara ya Mahakama, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza na Kamati za kusukuma kesi. Aidha, Idara ya Mahakama itakuwa ikichapisha vipeperushi vyenye maelezo ya masuala ya utawala wa sheria taratibu za ufunguaji upangaji na usikilizaji wa kesi katika Mahakama mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara itatilia mkazo kuandaa taarifa za masuala ya haki za Binadamu na kuziwasilisha kwenye Kamati mbalimbali za Tume ya Haki za Binadamu za ndani na za Kimataifa. Hii inatokana na ukweli kwamba Serikali ya Tanzania imekubali na kuridhia Mikataba ya Kimataifa ya haki za binadamu. Taarifa za utekelezaji wa Mikataba ya haki za binadamu ni njia maridhawa kuhakikisha kwamba masharti yanayowekwa kwenye mikataba hiyo yanatekelezwa na nchi wanachama. Taarifa hiyo ni kipimo cha utekelezaji wa masharti na pia ni njia ya kusahihisha taarifa potofu zinazotolewa na watu wasio na nia njema kwa nchi yetu ili kutuharibia sifa yetu machoni mwa jamii ya Kimataifa. Taarifa hizo zitasaidia kujua ukweli wa hali halisi ilivyo hapa nchini kutokana na jinsi nchi yetu inavyozingatia haki za binadamu.

Aidha, taarifa hizo husaidia kufahamisha umoja wa Mataifa juu ya matatizo ya uhaba wa raslimali, ujuzi, fedha au vitendea kazi tuliyo nayo katika kutekeleza masharti ya Mikataba hiyo. Itawezekana kwa vyombo hivyo kutoa msaada ili kukabiliana na matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyogusia awali, Wizara inatarajia kuandaa mapendekezo ya marekebisho katika Katiba ya nchi katika maeneo kadhaa yanayohusu masuala ya uchaguzi, kuimarisha vifungu vya haki na wajibu wa kila mtu na muundo na uendeshaji wa mhimili wa Mahakama. Kama ilivyo kawaida, baada ya mapendekezo hayo kupitiwa na Serikali kwa ujumla yatafikishwa katika Bunge hili likiwa ni sauti ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine itakuwa ni kufanya mapitio ya sheria mbalimbali za nchi na kuhakikisha kwamba zinawiana na matakwa ya Katiba ya nchi na majukumu ya nchi katika Mikataba ya Kimataifa ya haki za binadamu. Sheria hizo ni pamoja na sheria kuhusu watoto, ndoa na mirathi, kazi tutakayoifanya kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Aidha, Wizara hii kwa kupitia Tume ya Haki za Binadamu na utawala Bora itaongeza kasi ya usikilizaji wa malalamiko ya ukiukwaji wa Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora na kuwaelimisha wananchi wajibu wao. Mkazo utaelekezwa huko Vijijini ambapo ndipo walipo wananchi wengi. Wizara hii itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kueneza elimu hiyo.

Aidha, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itaendelea na ukaguzi wa Magereza katika ngazi zote na vituo vya Polisi na hali za mahabusu na wafungwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara itaendelea na majukumu yake ya uandishi wa Miswada ya Sheria, sheria ndogo ndogo zinazotungwa na mamlaka nyingine na pia kufanya utafiti, uchambuzi na uhuishaji wa sheria mbalimbali. Aidha, Wizara itaanzisha programu ya kuelimisha jamii kuhusu majukumu ya Tume ya kurekebisha jamii kuhusu majukumu ya Tume ya kurekebisha sheria na umuhimu wa kuwashirikisha katika kutunga na kurekebisha sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine tunayotarajia kuichukua ni kuunganisha mitambo ambayo inaitwa *Pre-press Typesetting* hivyo kuwezesha Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria na ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwasiliana kiuchapaji wakati wote - *two way networking* na hivyo kurahisisha na kuboresha kazi. Hata hivyo mitambo hii itanunuliwa hali ya fedha itakaporuhusu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii itaendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya sheria za Kimataifa pamoja na kuiwakilisha katika mashauri mbalimbali ya madai. Vile vile, Wizara itaendelea kushughulikia madai ya fidia na madai mengineyo ya kisheria. Aidha, Wizara itaendesha mafunzo kwa Majaji kuhusu sheria na Mikataba ya Kimataifa inayohusiana na sheria mbalimbali zinazohusiana na mabadiliko ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara itashughulikia Mpango wa Kurekebu Sekta ya Sheria na ukamilishaji kazi za tafiti chini ya mradi wa *Quick Start* kwa lengo la kuhakikisha kuwa utekelezaji wa matokeo ya tafiti hizo unaanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara itaongeza juhudi za kupata ushirikiano wa wabia wa maendeleo na kuwashawishi waongeze msaada wao katika utekelezaji wa miradi

iliyo chini ya Wizara. Jitihada zitafanyika kuhakikisha kwamba mafanikio yatakayopatikana katika Mikoa ya Arusha na Manyara yanasambazwa katika Mikoa mingine. Kama nilivyoeleza awali, kwa ushirikiano na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara inatarajia kuitisha kikao cha Wakuu wa Mikoa wote hapa nchini ili kutathmini mafanikio hayo na kupeana mkakati wa kusambaza mafanikio ya mradi nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara hii imelenga kuendelea na uboreshaji wa hadhi na uimarishaji wa vyombo vya utoaji haki nchini na kuvirudishia hadhi kama kuboresha mazingira ya kazi ya ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kanda zote, kuanzisha mfumo wa kuwa na kada ya maafisa Utawala wa Mahakama *(Court Administrators)* ili Mahakimu Wafawidhi watumie muda wao mwingi kusikiliza mashauri, badala ya kushughulikia masuala ya Utawala na fedha na kulifanyia ukarabati jengo la forodhani kwa ajili ya matumizi ya Ofisi za Mahakama ya Rufani.

Pia kukarabati majengo ya Mahakama Kuu Kanda za Mwanza, Moshi na Iringa, kuendesha ujenzi wa Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba, Mahakama za Wilaya za Kongwa, Ludewa na Mbarali. Aidha kujenga jengo jipya Mahakama ya Mwanzo na Manzese, Mahakama za Mwanzo chache zitakarabatiwa. Aidha, kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya fedha, Wizara inaandaa programu endelevu maalum kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Mahakama hizo katika Mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Spika, pia kuwapatia vyombo vya usafiri Mahakimu wa Wilaya Wafawidhi ishirini na tano kwa lengo la kuimarisha ukaguzi wa Mahakama na kuongeza kasi ya usukumaji kesi. *(Makofi)*

Kuendelea kuboresha mazingira ya Ofisi za Mahakama za Mwanzo kwa kuwapatia vitendea kazi muhimu. Aidha, kuhakikisha fedha zinazifikia Mahakama hizi, ikiwa ni pamoja na kero za Wazee wa Baraza. *(Makofi)*

Kufunga mtandao wa kompyuta ili kuimarisha mawasiliano, upatikanaji na utunzaji wa taarifa na kumbukumbu za shughuli za sekta ya Sheria na sekta nyinginezo, kuendelea kuboresha mazingira ya ofisi mbalimbali za watumishi na kuendeleza jitihada za kuajiri Mahakimu katika ngazi mbalimbali za Idara ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuboresha utoaji huduma na kuongeza ufanisi katika sekta ya Sheria, katika mwaka ujao wa fedha, Wizara imepanga kutekeleza mambo muhimu yafuatayo: -

Kuendeleza zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi wa ngazi mbalimbali pamoja na kuajiri watumishi wapya hasa Mahakimu, Mawakili wa Serikali na watumishi wengine ili kuziba upungufu uliopo, kuendeleza jitihada za kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa sekta na kuwapeleka watumishi kwenye mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kupata ujuzi na mbinu mpya za kitaalam na kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha, Wizara itaendelea na jitihada za kukabiliana na janga la Ukimwi kwa kushirikiana na wadau wengine katika nyanja mbalimbali. Wizara itaendelea kutoa elimu ya Ukimwi kwa watumishi wake katika ngazi zote chini ya Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi. Aidha, kwa kutumia fedha zilizotolewa na Wafadhili Wizara ilikitumia Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania *(TAWLA)* kufanya utafiti juu ya Sheria mbalimbali za nchi ili kuzihuisha ziweze kuwalinda watu wenye virusi vya Ukimwi. Utafiti huo ulilenga kuangalia uwezekano wa kurekebisha baadhi ya Sheria ili waathirika wa Ukimwi wasibaguliwe na watu kuwanyanyapaa. Kuhusu utafiti na wadau, Wizara inaangalia namna ya kufanyia kazi mapendekezo ya utafiti uliofanywa na *TAWLA.* Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria pia imeandaa Mkakati wa Utafiti kuhusu Sheria zinazohusu suala zima la Ukimwi. Utafiti wa Sheria hizi utaanza kufanyika katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa nia ya kudumisha hadhi ya Mahakama na sekta nzima ya Sheria. Wizara itaimarisha ukaguzi wa mara kwa mara kwenye mahakama na ngazi zote za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, vitachapishwa vitabu vya Mwongozo wa Ukaguzi wa Mahakama *(Supervision Manual)* na kuirejesha kada ya Mahakimu Wakaguzi wa Mahakama *(Supervisory Magistrates).* Pia, Wizara imepanga kuandaa mkutano wa Majaji na Mahakimu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha, Wizara itashirikiana na Taasisi zinazoshughulikia masuala ya jinsia kuendesha mafunzo kwa watumishi wa Wizara kwa nia ya kujenga uwezo wa kubuni, kutayarisha, kutekeleza na kutathmini mipango na Bajeti inayozingatia masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Taifa kwa ujumla limepata pigo kubwa la kuondokewa na aliyekuwa Jaji Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Francis L. Nyalali, aliyefariki mwezi Aprili, 2003. Pia Taifa hili limeondokewa na Jaji wa Mahakama ya Rufani akiwa katika utumishi Mheshimiwa Kamugumya Simon Kahwa Rugakingira, aliyefariki mwezi Juni 2003 na Jaji wa Mahakama ya Rufani Mstaafu Mheshimiwa Jaji Ali M. Omar, aliyefariki Aprili, 2003 huko Zanzibar na Mheshimiwa Jaji Mstaafu A. G. Korosso aliyefariki mwezi Aprili, 2003. Aidha, Taifa limeondokewa na Majaji wa Mahakama Kuu wawili wakiwa katika utumishi, Mheshimiwa Jaji Asher A. Kyando, aliyefariki Mwezi Oktoba, 2002 na Mheshimiwa Jaji Kulwa Massaba, aliyefariki mwezi Desemba, 2002. Marehemu Majaji hao walikuwa tegemeo kubwa Kitaifa na watumishi wachapakazi hodari, waadilifu waliotoa mchango mkubwa kiutumishi kwa wananchi wa Tanzania. Napenda kutoa pole kwa familia zao.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa pole kwa familia za wafanyakazi wengine wa Wizara yangu waliotutoka na kutuachia mapengo katika utumishi wa umma. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze mahali pema peponi roho za marehemu wote hao. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya kuendeleza demokrasia ya uwakilishi wa wananchi ndani ya Bunge lako Tukufu, ulifanyika Uchaguzi wa Wabunge katika Majimbo yote ya Kisiwa cha Pemba na baadhi ya Majimbo ya Tanzania Bara baada ya Majimbo hayo kuwa wazi kwa sababu mbalimbali. Napenda kuungana na Mawaziri wenzangu waliotangulia kutoa hotuba zao kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa katika Majimbo yao, wale walioteuliwa kwa viti maalum na waliorudishwa Bungeni baada ya kushinda kesi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Majaji Eusebia N. Munuo na Harold C. Nsekela, walioteuliwa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni kuwa Majaji wa Mahakama ya Rufani na Waheshimiwa Njegafibili M. Mwaikugile, Salome S. Kaganda, Projestus A. Rugazia, Salum A. Massati, Radhiabegum H. Sheikh na Augustine F. Shangwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu. Hali kadhalika, napenda kumpongeza Bwana Augustine Mwarija kwa kuteuliwa kuwa Msajili wa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.

Vile vile, napenda kuwapongeza wafuatao, Mheshimiwa Pius Msekwa na Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Bwana Mohamed Ismail na Bwana Onael Malisa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Makamishna wa Muda (*Part Time*), Bwana William J. M. Mdundo na Jaji Mstaafu Mheshimiwa Edward A. Mwesiumo, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Makamishna wa Kudumu (*Full Time*) wa Tume ya Kurekebisha Sheria.

Naomba nimalizie hotuba yangu kwa kuwashukuru viongozi na watendaji Wakuu na watumishi wote katika Wizara yangu ambao kwa kipindi kirefu wamekuwa wakinipatia msaada mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kuiongoza Wizara. Naomba niwataje kwa majina Jaji Mkuu, Mheshimiwa Barnabas Albert Samatta, Jaji Kiongozi, Mheshimiwa Hamis A. Msumi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew J. Chenge , Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mheshimiwa Jaji Robert H. Kisanga, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Mheshimiwa Jaji Anthony Bahati, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Sheria Tanzania, Bibi Mwanaidi Maajar, Mwenyekiti wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Bwana Paul Rupia na Rais wa Chama cha Wanasheria nchini, Bwana Thomas Mihayo.

Aidha, nawashukuru Watendaji Wakuu wa Vyombo mbalimbali vilivyo chini ya Wizara hususan Bwana Johnson P. M. Mwanyika, Naibu Mwanasheria Mkuu na Katibu Mkuu wa Wizara, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa kuteuliwa kwake. Naamini kwamba Bwana Mwanyika aliyekulia katika Wizara hii ya Sheria atatoa mchango mkubwa katika kusukuma mbele gurudumu la Wizara. Bwana Augustine G. Mwarija, Msajili wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Bi Mary S. Shangali, Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Bwana Gad J. K. Mjemas, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za

Binadamu na Utawala Bora na Bibi Daria Bigeye, Kaimu Mshauri Mkuu wa Shirika la Sheria Tanzania. Msaada wao umenisaidia sana katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa nchi wahisani na Taasisi za Kimataifa ambazo zimeendelea kutoa misaada mbalimbali kwa ajili ya kuiendeleza na kuisaidia sekta ya Sheria nchini. Naomba niwataje kwa majina Serikali ya Canada, Denmark, Ujerumani, Ireland, Marekani, Uingereza, Finland, Norway, Uholanzi, Sweden na Mashirika ya Kimataifa ya Benki ya dunia, *UNDP, USAID, KAF, British Council, CIDA* (Canada) na *SIDA* (Sweden). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza malengo na majukumu yake yaliyoainishwa kulingana na mwelekeo kwa mwaka wa fedha 2003/2004 na kama yalivyochambuliwa katika vitabu vya makisio, naomba Bunge lako Tukufu likubali Wizara yangu ipatiwe jumla ya shilingi 31,846,939,583/= katika mchanganuo ufuatao, Fungu 40, Idara ya Mahakama, Matumizi ya Kawaida shilingi 16,273,736,300/= Matumizi ya Maendeleo shilingi 1,700,000,000/=, jumla ni shilingi 17,973,736,300/=.
Fungu 41, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Matumizi ya Kawaida shilingi 4,578,492,549/=, Matumizi ya Maendeleo shilingi 4,458,241,090/=, jumla ni shilingi 9,036,733,639/=.

Mheshimiwa Spika, Fungu 55, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Matumizi ya Kawaida shilingi 2,007,585,393/=, Matumizi ya Maendeleo shilingi 827,200,000/=, jumla ni shilingi 2,834,785,393/=.

Fungu 59, Tume ya Kurekebisha Sheria, Matumizi ya Kawaida shilingi 482,737,200/=, Matumizi ya Maendeleo shilingi 220,000,000/=, jumla ni shilingi 702,737,200/=.

Mheshimiwa Spika, Fungu 64, Mahakama ya Biashara, matumizi ya kawaida shilingi 587,332,200/=, Matumizi ya Maendeleo shilingi 250,800,000/=, jumla ni shilingi 838,132,200/=. Fungu 90, Mahakama ya Ardhi, Matumizi ya Kawaida shilingi 460,814,800/=, Matumizi ya Maendeleo hakuna, jumla ni shilingi 460,814,800/=.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004 Wizara hii imekisia kukusanya kiasi cha shilingi 1,766,355,000/= kama maduhuli ya Serikali kwa mchanganuo ufuatao: -

Mheshimiwa Spika, Fungu 40, shilingi 482,405,000/=, Fungu 41, shilingi 383,750,000/=, Fungu 55, shilingi 200,000/=, Fungu 59, hakuna, Fungu 64, shilingi 900,000,000/=, jumla ni shilingi 1,766,355,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (k.n.y. MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2003 kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati naomba kuwasilisha Taarifa na Maoni ya Kamati na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.
Mheshimiwa Spika, wajumbe wa Kamati hii ni Mheshimiwa Athumani Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti na wajumbe Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Ramadhan Khalfan, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa George Mlawa,

Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Grace Kiwelu na Makatibu wa Kamati Ndugu Nenelwa Mwihambi na Ndugu Ernest Zulu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 3 Juni, 2003 Kamati yangu ilikutana Jijini Dar es Salaam kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa mwaka 2002/2003 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2003/2004 kwa mafungu yafuatayo:-

Fungu 40 - Idara ya Mahakama, Fungu 41 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Fungu 64 - Mahakama ya Biashara na Fungu 90 - Mahakama ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kikao hiki Kamati yangu ilipata fursa ya kufanya ziara katika Taasisi kadhaa zilizo chini ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Lengo likiwa ni kujifunza shughuli zinazofanywa na kujionea mazingira halisi ya utendaji kazi wa Taasisi hizo. Taasisi zilizotembelewa katika ziara hiyo ni Makao Makuu ya Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu, Mahakama Kuu ya Tanzania, Mahakama za Mwanzo Manzese na Kariakoo, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu pamoja na Mahakama ya Watoto na Mahakama ya Biashara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mengi mazuri ambayo Kamati yangu ilijifunza, tuliweza pia kuelezwa na kujionea matatizo makubwa yanayoikabili Idara ya Mahakama. Kwa ruhusa yako naomba kwa kifupi niyataje matatizo hayo kama ufinyu wa Ofisi katika Makao Makuu ya Wizara, Mahakama Kuu, Tume ya Kurekebisha Sheria na kadhalika, uhaba wa nyumba kwa Majaji na Mahakimu hivyo kulazimisha baadhi yao kuishi hotelini na maeneo yasiyostahili kwa muda mrefu, uchakavu wa majengo ya Mahakama hasa Mahakama za Mwanzo na kucheleweshwa malipo ya Wazee wa Mahakama. Pamoja na kukamilika kwa kesi wanazoshughulikia, bado hawalipwi posho zao kwa wakati. Katika Mahakama mbalimbali kuna madai ya malimbikizo ya miezi kadhaa kwa posho za wazee hawa wa Mahakama

Pia Mahakama hazina usafiri hata kwa ajili ya kupeleka fedha na kuchukua mishahara Benki na uhaba wa vitendea kazi, mfano karatasi, meza, makabati ya vielelezo vya kesi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliopita Kamati yangu ilitoa maagizo katika maeneo kadhaa. Tunaipongeza Wizara kwa hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza maagizo hayo. Pamoja na pongezi hizo, Kamati yangu inasisitiza jitihada zaidi katika kushughulikia maeneo yafuatayo:-

Mahakama ya Ardhi. Kamati inasisitiza ushauri wake kwamba Mahakama hiyo iwaelimishe Watendaji wa Vijiji, Kata na Tarafa juu ya matumizi ya Sheria mpya za Ardhi Na. 4 na Na. 5 za mwaka 1999.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kamati inashauri Tume iandae na kuwasilisha mipango yake ya kuhakikisha elimu juu ya Kanuni za Utawala Bora inawafikia wananchi vijijini hasa watendaji wa Kata.

Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Kamati bado inasisitiza ufanyike uchunguzi (*social study*) kuhusu kiini cha uhalifu hasa kwa vijana. Hii ifanyike kwa ushirikiano na Wizara nyingine kama Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara na nyingine husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa hii iliwasilishwa mbele ya Kamati na Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Mbunge. Kamati yangu ilielezwa kuwa Wizara ilipata mafanikio ya kuridhisha katika kutekeleza mpango wa 2002/2003. Miongoni mwa mafanikio hayo ni haya yafuatayo:-

Kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani. Hii ilitokana na jitihada za kuzipatia vitendea kazi Mahakama mbalimbali, mpango wa kuratibu Kamati za Kusukuma Kesi *(Case Flow Management)* na pia ajira zaidi kwa Mahakimu, Majaji wa Mahakama Kuu na Majaji wa Mahakama ya Rufani.

Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora. Kamati yangu ilielezwa kwamba Wizara, kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ilipokea na kufanya uchunguzi wa malalamiko na tuhuma zinazohusu ukiukwaji wa haki za binadamu na utawala bora. Malalamiko 2,000 kati ya zaidi ya 5,000 yaliyopokelewa kutoka magereza yote ya Mikoa ya Tanzania Bara yameshughulikiwa na kutolewa maamuzi.

Utekelezaji wa majaribio ya uboreshaji Mahakama. Kamati ilifahamishwa kwamba majaribio ya kuboresha Mahakama za Mwanzo na za Wilaya katika Mikoa ya Arusha na Manyara *(Quick Start)* yalitekelezwa baada ya kuzinduliwa mwezi Januari mwaka huu.Pamoja na mafanikio hayo Kamati yangu ilielezwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2002/2003 Wizara ilikabiliwa na matatizo kadhaa yaliyotokana na ufinyu wa Bajeti, kama ifuatavyo:-

Kushindikana kukamilika kwa zabuni ya ukarabati wa jengo la Forodhani ambalo litatumika kama Ofisi za Mahakama ya Rufani, ukosefu wa vyombo vya usafiri kwa watumishi wa Wizara, uhaba na uchakavu wa majengo ya Wizara na Mahakama.

Pia mawakili wa Serikali na Mahakimu kuacha kazi Serikalini kutokana na mishahara midogo na motisha duni na kushindikana kwa zoezi la usambazaji wa mradi maalum wa usajili wa ndoa, vizazi na vifo chini ya mradi wa *Civil Registration Programme (CRP).*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imejulishwa kuwa katika kipindi cha 2003/2004 Wizara imepanga kutekeleza kazi mbalimbali ambazo zinalenga kufanikisha Dira ya Wizara ambayo ni Haki kwa Wote na kwa Wakati. Miongoni mwa kazi hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuendelea kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani kwa kuongeza vikao vya mahakamani, kuimarisha Kamati za kusukuma kesi na utaratibu wa kumaliza kesi kwa njia ya usuluhishi.

Pili, kuandaa taarifa za masuala ya Haki za Binadamu na kufanya marekebisho katika Katiba ya nchi hususan vifungu vinavyohusu masuala ya uchaguzi. Pia kuimarisha vifungu vinavyohusu haki na wajibu wa kila mtu.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuendelea kushughulikia uandishi wa Miswada ya sheria, na sheria ndogo ndogo zinazotungwa na mamlaka nyingine, nne, kukarabati jengo la Forodhani kwa ajili ya Mahakama ya Rufani, kukarabati majengo ya Mahakama Kuu za Mwanza, Moshi na Iringa, kujenga Mahakama Kuu Bukoba na Mahakama za Kongwa na Mbarali na tano, kuboresha utoaji wa huduma na kuongeza ufanisi wa Wizara kwa kupandisha vyeo, kuajiri watumishi wapya, kutoa mafunzo na kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujionea hali halisi ya uchakavu wa majengo ya Mahakama ya Mwanzo ya Manzese Kamati yangu haikuridhishwa na kitendo cha Wizara kutotenga fedha yoyote kwa ajili ya kukarabati au kujenga upya mahakama hiyo na nyingine zenye hali kama hiyo. Kutokana na kutoridhishwa huku, Kamati ilimwita Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Mramba.

Baada ya majadiliano ya kina baina ya Kamati, Waziri wa Fedha na Waziri mhusika, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ilikubali kutoa katika bajeti yake ya mwaka 2003/2004 kiasi cha shilingi 50,000,000/= ili mahakama ya Mwanzo ya Manzese ibomolewe na kujengwa upya. Vilevile Waziri wa Fedha ametoa ahadi kuwa katika mwaka wa fedha ujao Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa Mahakama za mwanzo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inapongeza maamuzi ya busara na kushauri kuwa jitihada zifanyike ili mwaka ujao wa fedha (2004/2005) mahakama zenye hali mbaya zikarabatiwe na nyingine zijengwe. Vile vile Kamati inashauri mahakama zipatiwe vitendea kazi ili kufanikisha na kurahisisha kazi zao, mahakama za Wilaya zipatiwe usafiri ambao pamoja na mambo mengine utawezesha kufanyika ukaguzi wa mahakama za mwanzo mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia inashauri na kusisitiza wazee wa baraza walipwe fedha zao wanazoidai Serikali kutokana na kesi zilizomalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati inashauri mafunzo yaendelee kutolewa hasa kwa Idara ya Uandishi wa Sheria ili miswada ya sheria na mikataba mbalimbali inayoandaliwa na Idara hiyo iwe ubora unaohitajika kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu. Ofisi hii ni muhimu sana katika ukusanyaji na utunzaji wa takwimu zinazohusu Watanzania wote. Lakini majengo yake ni machakavu na watumishi wanafanya kazi katika mazingira magumu mno.

Vile vile Kamati imeona kuwa mfumo wa utendaji kazi ni wa kizamani. Hivyo, Kamati yangu inashauri Wizara itenge fedha kwa ajili ya ukarabati wa Ofisi hii na kununua vifaa vya kisasa ili utendaji kazi uboreshwe na kuleta ufanisi. Aidha, sheria inayotumika katika masuala ya uzazi na vifo ni ya zamani sana na haijafanyiwa marekebisho toka tupate Uhuru. Kamati inashauri sheria hiyo irekebishwe ili kuendana na mabadiliko yanayotokea nchini na duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Kamati yangu inapongeza kuwepo kwa mpango wa kuifanyia marekebisho Katiba ya nchi. Aidha, tunashauri haki ya mtu kushiriki uchaguzi kama mgombea binafsi kwa ngazi ya Ubunge na Udiwani pia iangaliwe na kufanyiwa kazi katika marekebisho hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi fulani tatizo la mlundikano wa mahabusu linasababishwa na sheria zetu zinazohusu mienendo ya kesi za madai na zile za jinai na kutofuatwa kwa taratibu za kutoa vifungo vya nje kwa makosa madogo madogo. Hivyo, Kamati yangu inashauri Wizara itazame uwezekano wa kurekebisha sheria hizo na kusisitiza ufuatiliaji wa taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kamati inashauri Tume isiishie kufanya ziara katika magereza ya Mikoa tu, bali ifike hadi magereza ya Wilaya ambako ukiukwaji wa haki za binadamu unafanyika kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** Kamati yangu pia inashauri kuwa katika suala la matumizi kuwe na utaratibu wa kuheshimu mihimili mitatu ya dola yaani Serikali, Bunge na Mahakama. Mihimili hiyo igawane kutoka Pato la Taifa kwa uwiano mahitaji yao asilimia fulani ya mapato ya Taifa kwa ajili ya utekelezaji wa malengo ya kila mmoja. Kwani hali ilivyo sasa Mahakama inatengewa fedha kidogo sana ikilinganishwa na umuhimu wake katika jukumu la kutoa haki kwa wote. Hili lisipotekelezwa kuna uwezekano wa wananchi kukosa imani na Serikali yao, na hata kuhatarisha amani na utulivu wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inashauri kuwepo ushirikishwaji wa Wabunge na wadau wengine katika hatua za mwanzo za maandalizi ya Bajeti ya Serikali ili wachangie maoni kuhusu maeneo ya kupewa kipaumbele. Utaratibu wa sasa unawashirikisha Wabunge katika hatua ambayo hairuhusu hata kufanya marekebisho katika bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004 Kamati yangu iliombwa iidhinishe jumla ya shilingi 31,846,939,583/= kwa mafungu yote ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii. Kamati yangu imeridhia ombi hili na inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha ombi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** baada ya kusema hayo napenda sasa nikushukuru kwa kunipatia fursa hii ya kusoma taarifa ya Kamati. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Harith Mwapachu, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba na Wataalam wake wote kwa maelezo ya kina na ushirikiano waliouonyesha kwa Kamati yangu.

Aidha, natoa shukrani kwa Ofisi ya Bunge na wote waliohusika katika maandalizi na ufanikishwaji wa ziara za Kamati hii kwani Kamati imejifunza mambo mengi ambayo yamesaidia sana katika uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Kwa namna ya pekee napenda niwashukuru

Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati yangu kwa michango yao mizuri iliyochambua kwa kina Bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda niishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na ndugu Kipenka Msemembo Mussa na wasaidizi wake, hususan Makatibu wa Kamati ndugu Nenelwa Mwihambi na Ernest Zulu kwa kuihudumia vema Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na wajumbe wote wa Kamati hii naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, niwajulishe Waheshimiwa Wabunge wanne watakaochangia sasa hivi kwa kufuatana. Wa kwanza ni Mheshimiwa Asha Ngede, wa pili ni Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, wa tatu ni Mheshimiwa Getrude Mongella na wanne ni Mheshimiwa Rhoda Kahatano, hao ndiyo wasemaji wanne wa kwanza. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa mwaka wa Fedha 2003/2004 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b) na (c) toleo la 2003.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Mbunge, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, na Katibu Mkuu na timu yake yote ya Wataalam kwa kuandaa Bajeti hii, ambayo kimsingi Kambi ya Upinzani haina matatizo nayo. Hata hivyo, Kambi ya upinzani inadhani kuna maeneo ambayo yanahitaji ufafanuzi wa kina kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali niseme ninaunga mkono hoja za Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria kwa vile mimi pia ni Mjumbe wa Kamati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaanza kuidodosa Bajeti hii kwa kutazama kwa kina Hotuba za nyuma za Wizara hii, mathalani, Bajeti za mwaka 2001/2002 na 2002/2003 kwa lengo la kupima tunakotoka na tunakoenda. Maeneo hayo ni kama yafuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka wa Fedha 1999/2000, 2001/2002 na 2002/2003 Mheshimiwa Waziri alieleza dira na lengo Kuu la Wizara yake kuwa ni kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Ripoti ya Kamati ya Mheshimiwa Mark Bomani. Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa Kamati ya Mark Bomani ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sekta nzima ya Sheria pamoja na suala zima la utoaji haki hapa nchini.

Kamati hiyo ilitoa mapendekezo ya jinsi ya kuyatatua matatizo yanayoikabili Sekta hii. Kwa bahati mbaya, ni muda mrefu sasa tangu Kamati hii ilipomaliza kazi yake na kutoa ripoti yake, na ni miaka 4 Mheshimiwa Waziri akielezea Bunge lako Tukufu mikakati ya utekelezaji wa taarifa hiyo bila kuwa na mpango madhubuti na makusudi wa jinsi ya kutekeleza mapendekezo ya Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunatumaini kuanza kwa mradi wa *Quick Start,* utakuwa mwanzo mzuri wa utekelezaji wa ripoti hiyo. Wakati tunaendelea na mikakati, gharama za utekelezaji wa mpango huo zinapanda kila mwaka. Kambi ya Upinzani inadhani kama Serikali haitaweka mpango wa makusudi na kwa kutumia fedha zake za ndani, tutafika mahali mpango huo hautatekelezeka kabisa, hasa kama tutabaki kuwasubiri wahisani.

Kimsingi, kutokutatuliwa matatizo yaliyoainishwa katika Ripoti ya Kamati ya Mark Bomani, ndiyo msingi wa matatizo makubwa yanayoikumba Sekta ya Sheria. Ni hatari sana Programu ya Sekta ya Sheria kuegemea kwa miradi ya Wahisani, kwani Haki ya Mtanzania inapaswa kutolewa na Serikali ya Tanzania, wahisani wanaweza kutuongezea nguvu tu. Tunashukuru kuwa, hata hivyo, Bajeti ya Wizara hii imeendelea kuongezeka mwaka hata mwaka, japo zaidi ni kwa upande wa utawala, kama inavyoonekana kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya mwaka 2003/2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatambua jinsi Serikali ilivyosikiliza kilio cha Wabunge na Watanzania kwa ujumla kuhusu Haki za Binadamu au za Kiraia na hivyo kuunda Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tunapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Jaji Robert Kisanga na Makamishna wake kwa uteuzi huo. Lakini tunawapa pia pole nyingi kwa kazi nzito iliyoko mbele yao.

Mheshimiwa Spika, tumefurahi kuona kuwa Tume imeanza kazi yake, na tunatumaini kuwa kero zinazohusu haki za msingi pamoja na masuala ya Utawala Bora yatashughulikiwa kikamilifu. Tungependa Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili, ni utaratibu gani, Tume hii itafika nchi nzima, hasa vijijini ambako ndiko kuna kero nyingi na wakati huo huo wananchi walio wengi wala hawajui haki zao za msingi, wala maana ya Utawala Bora.

Mara nyingi, hawana uwezo wa kufuatilia haki hizo Dar es Salaam, ambako ndiko kuna Ofisi za Tume na wataalam wa Tume. Tume isipoweka utaratibu makini na kupewa fedha za kutosha kufikisha elimu ya Haki hizo vijijini, na au mitaani waliko wananchi walio wengi tutatumia fedha nyingi bila matunda yeyote. Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi jinsi tunavyopata malalamiko mengi kutoka kwa wananchi mbalimbali walionyanyasika kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, ni imani yetu kuwa Tume hii itakuwa kimbilio la wanyonge, na isiwekewe mizengwe ya aina yeyote ile. Utarabitu ukiwekwa bayana, kero zitapungua sana, hususan vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003 Mheshimiwa Waziri alieleza nia yake ya kuimarisha haki kwa kundi maalum la Watoto. Hii ikiwa ni pamoja na kuimarisha Mahakama ya Watoto Kisutu. Pamoja na kazi na nia hiyo nzuri, Sheria mbalimbali zinazolinda Haki za Watoto hazijafanyiwa marekebisho.

Mathalani, mwaka 1986 Tume ya Kurekebisha Sheria ilisema kuwa Sheria zinazohusiana na Watoto zina dosari na udhaifu mwingi, kiasi kwamba Sheria hizo zinashindikana kutumika mahakamani katika kutetea haki za Watoto.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jaji Lubuva, aliyekuwa Waziri wa Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali alijulishwa juu ya Jambo hilo kwa barua ya Tarehe 5 Julai, 1986. Mwezi Aprili, 1994 Kamati maalum chini ya Mwenyekiti wake Dr. Ringo Tenga, iliwasilisha taarifa yake na mapendekezo mbalimbali kuhusu namna ya kuboresha haki za Watoto.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya, ni miaka 18 tangu Tume ya Kurekebisha Sheria ilipotoa Taarifa yake na miaka 9 tangu Kamati Maalum ilipotoa taarifa yake Wizarani na hakuna hatua yeyote iliyochukuliwa na wala marekebisho husika hayajafanyika.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazohitaji marekebisho haya licha ya zilizotajwa na Mheshimiwa Waziri leo ni pamoja na *Affiliation Ordinance, Cap* 278, ambayo hadi leo inasema kuwa Mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa atalipiwa kiasi kisichozidi shilingi 100 na mhusika aliyempa mimba mwanamke huyo, tena baada ya utaratibu wa kisheria mgumu kweli kweli kuthibitisha ubaba *(fatherhood)* wa huyo mwanaume.

Mheshimiwa Spika, sheria hii ilitungwa mwaka 1949 na wakoloni na imebakia hivyo hivyo, pamoja na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii katika nchi yetu. Leo hii, shillingi 100 wala hainunui pipi, lakini imebakia kwenye Sheria yetu. Kambi ya Upinzani inamtaka Mhe. Waziri awasilishe mara moja Marekebisho ya Sheria hii ambayo ni muhimu sana kwa ustawi wa watoto wetu, na akinamama wanaoathirika na hali hii bila kutegemewa, au wanaotelekezwa kwa sababu moja au nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na Shirika lisilo la Kiserikali la *Legal and Human Right Center (LHRC),* unaonyesha kuwa hivi karibuni kumekuwa na matukio mengi ya kutupwa kwa watoto wachanga, na mathalan, kila baada ya siku 3 mwaka 2002 kulikuwa na matukio kama hayo. Idadi ya watoto wa mitaani nayo imeongezeka maradufu. Isitoshe, watoto waliobahatika kuokoka kutokana na

majanga haya wameendelea kuteseka hata kama wazazi wao ni mamilionea. Hii imetokana na sheria isiyokidhi mahitaji ya nyakati hizi.

Mheshimiwa Spika, sheria zingine zinazohitaji marekebisho ya haraka ni *The Children and Young Persons Ordinance, Cap.13,* ambapo tafsiri ya mtoto chini ya sheria hii inawaondoa watoto walio kati ya miaka 16 na 18, katika tafsiri hiyo na kifungu cha 4(1) kinaondoa kabisa uwezekano wa mtoto kupewa dhamana anaposhtakiwa kwa makosa ambayo adhabu yake ni kifungo cha miaka saba. Isitoshe, kuna mgongano wa sheria, kwani *Penal code* kutokana na marekebisho yaliyotokana na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya 1998, imewanyima watoto hata haki walizokuwa wamepewa chini ya *Children and Young Persons Ordinance.*

Mathalan, wakati kifungu cha 22(1) cha *Ordinance* kinawaondoa watoto wa chini ya miaka 12 kutoka kwenye adhabu ya kifungo, chini ya vifungu vya sasa 131(2)(c); 131(3) na kifungu cha 15(2) na (3) cha *Penal Code* ikisomwa pamoja na kifungu cha 4 na 5 vya *Evidence Act*, 1967 si tu mtoto wa chini ya miaka 12 anaweza kufungwa bali pia kupata kifungo cha maisha kwa makosa ya kubaka. Sheria ya Ndoa, 1971 Kifungu cha 13(2) bado kinaruhusu mtoto wa kike wa miaka 14 kuolewa, japo kifungu cha 13(2) cha *Penal code* kinataja wazi kuwa mtoto huyo hajafikia umri wa kutoa ridhaa *(consent)* kwa masuala ya kujamiiana. Kifungu cha 138(6) kwa tafsiri ya haraka haraka kinaonekana kuruhusu ndoa ya mwanamke katika umri wowote, ni dhahiri kuna mgongano mkubwa wa sheria.

Kambi ya Upinzani inatambua kabisa hitaji la kufanya utafiti na maandalizi ya kutosha kabla ya kufanya marekebisho na kuhuisha sheria, lakini, Kambi inashangaa na kusikitishwa kuona kuwa Serikali inachelewa sana katika kufanya mabadiliko ya sheria kuendana na wakati. Sheria ya Mirathi ni moja ya sheria inayokumbwa na matatizo makubwa. Tunapongeza Shirika Hiari la Mtandao wa Jinsia ambayo sasa imeanza kazi ya kuandaa Muswada wa Marekebisho ya Sheria hii na nyingine zinazofanaa. Tunaamini Mheshimiwa Waziri atatoa ushirikiano wa karibu kusaidia kuleta mabadiliko haya muhimu kama alivyoahidi katika hotuba yake ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya, hata zile nafuu *(reliefs)* ambazo zinatolewa na sheria zilizoko imekuwa vigumu kupatikana. Mfano hai ni pale sheria inapotoa haki ya kusikiliza kesi ya watoto katika chumba tofauti na vyumba tofauti vya rumande, lakini, Mahakama pekee ya watoto iko Kisutu tu kwa Tanzania nzima. Tunaamini Ujenzi wa Mahakama ya Mbeya na Mtwara utaanza mara moja kama Waziri alivyoahidi leo.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonyesha kuwa katika utekelezaji Mahakama na Polisi wamekuwa wakichanganya watoto na watu wazima. Kuna vituo saba tu vya rumande kwa nchi nzima, na utafiti unaonyesha kuwa wakati mwingine watoto hukaa katika vituo vya polisi hadi siku 7, kabla ya kupelekwa Mahakamani au kuachiwa kwa dhamana kutokana na matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mahakimu nao wanakiri kuwa Sheria za Watoto ni vigumu sana kueleweka bila utaalamu wa pekee. Matakwa ya Sheria kuwa watoto wahalifu wapelekwe kwenye shule maalum imebakia kwenye vitabu tu, kwani kwa nchi nzima kuna shule moja tu ya aina hiyo yaani *Irambo Approved School* iliyoko Mbeya na isitoshe nayo ni kwa wavulana tu. Ni imani yetu kuwa MheshimiwaWaziri ataleta mabadiliko yanayotakiwa katika sheria na katika utekelezaji ili kulinda maslahi ya hawa ambao tunawatambua kuwa Taifa la kesho.

Sheria za ajira ya watoto nazo zinahitaji kuangaliwa upya na kwa haraka. Pamoja na matakwa ya *Employment Ordinance* na Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeweka saini na kuridhia, watoto chini ya miaka 15 na wakati mwingine hata 12 wameendelea kuwa katika ajira. Elisa Lwakatare, Mkurugenzi wa Kitengo cha Ajira ya Watoto, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, katika mkutano uliofanyika Karimjee, 23 Juni, 2002 alieleza kuwa watoto milioni 4.2 kati ya watoto milioni 10.2 wa Tanzania kati ya umri wa miaka 5 hadi 14 hawako shuleni kutokana na kujihusisha katika ajira na biashara ndogo ndogo. Utafiti uliofanyika *Kibwela Tea Estate* na Bwana Hosea Rwegoshora wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Kitengo cha *Child Law Unit,* 1997 ilionyesha kuwa watoto 120 wa umri kati ya miaka 12 na 15 walikuwa wakifanya kazi kwenye mashamba hayo kati yao 15% walikuwa hawajaenda na wala hawaendi shule, asilimia 40 walikuwa wameacha shule, asilimia 40 ni watoto wa shule watoro na isitoshe malipo yao yalikuwa madogo sana.

Hali iko hivyo hivyo, katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Machimbo ya Madini, kama vile Chunya, Mererani na hata Machimbo ya kifusi Kunduchi au *Magogoni Ferry* ambapo utafiti wa *LHRC, 2002* ulionyesha watoto 150 wakijihusisha na biashara ya samaki. Kambi ya Upinzani inadhani hii ni hali ya kutisha na Serikali ni lazima ichukue hatua madhubuti kurekebisha sheria husika na kuzisimamia ipasavyo. *(Makofi)*

Kuhusu haki za walemavu, sheria zetu nyingi zimebaki vitabuni na zimeshindikana kutekelezeka. Mathalan, pamoja na kwamba Ibara ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inatambua haki ya walemavu kupata kazi, elimu na huduma za jamii, *The Employment of the Disabled Act, 1982*, kifungu cha 15 inatamka wazi kuwa Waajiri wenye zaidi ya wafanyakazi 50 wanatakiwa waajiri angalau asilimia 2 ya watu hao iwe walemavu.

Kifungu cha 16 cha sheria hiyo inatoa kinga kwa walemavu kutopunguzwa kazini. Lakini haya yote hayakutekelezwa hata katika Taasisi za Serikali yenyewe, ambaye bado ni mwajiri mkuu na pamoja na kuwa walemavu wengi wamehitimu fani mbalimbali, ikiwemo ualimu, *Telephone, Social Welfare* na kadhalika. Sheria ya *Disabled (Care and Maintenance) Act*, nayo ya 1982 inaitaka Serikali za Mitaa kutoa mafunzo maalum kwa ajili ya walemavu na kuunda mfuko maalum kwa ajili ya huduma kwa walemavu.

Lakini wakati Mfuko wa Wanawake na Vijana unazungumziwa kila mara Mfuko wa Walemavu umesahaulika kabisa, japo hawa huhitaji msaada wa pekee. Isitoshe sheria zetu hazikuzingatia mazingira maalum ya walemavu mathalan, hakuna sheria inayowalinda katika usafiri, matumizi ya majengo ikiwemo jengo letu la Bunge ambapo Mbunge mwenzetu Margareth Mkanga, kila siku anahangaika kupanda ngazi za ajabu na hata jana mlimuona anahangaika na hata pamoja na uzoefu huu, bado hatujahamasika kuandaa mazingira husika ya kisheria kutoa huduma hizo. Kambi ya Upinzani inadhani wakati umefika sasa wa kutazama upya sheria hizi zilizolala vitabuni kwa lengo la kutoa huduma inayostahili kwa wanajamii wetu wote, hasa wenye kuhitaji zaidi msaada wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache katika Afrika ambazo zimeweka Haki za Msingi za Binadamu katika Katiba yake. Tunaipongeza kwa hatua hiyo. Pamoja na pongezi hiyo, Tanzania ambayo ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa na kuwa imejitahidi kusaini hati mbalimbali za Umoja huo.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya, Tanzania, kwa taarifa iliyoko katika Mtandao *(Internet)* bado haijasaini wala kuridhia na au kupeleka kwa *Depository* hati muhimu zifuatazo: *The International Convention Against Torture and Other Cruel, Inhuman or Degrading Treatment or Punishment (CAT), The Optional Protocol to the International Covenant on Civil and Political Rights*,1996 *(ICCPR)* na isitoshe nyingi ya hati mbalimbali za Kimataifa ambazo zimesainiwa, zimeridhiwa na kuwa *Deposited* hazijatungiwa sheria za ndani yaani *Domesticated* na hivyo zinashindikana kutumika kama sheria na hivyo hazitekelezeki na au hazijahuishwa na sheria zingine za nchi. Ni vema Mheshimiwa Waziri akatoa ufafanuzi wa kina kuhusu jambo hili wakati wa kutoa ufafanuzi na ni lini sheria hizo zitahuishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 13 inatoa haki ya kila Mtanzania kusikilizwa Mahakamani *(Fair Trial).* Haki inatekelezeka iwapo mwananchi husika anafahamu haki zake, na ni lazima chombo cha haki kitoe haki sawa kwa wote *(Impartial).* Isitoshe mwananchi naye ana haki ya kupewa nafasi ya kusikilizwa. Kwa bahati mbaya haki hii kwa muda mrefu imekumbwa na matatizo mengi.

Baadhi ya matatizo haya ni kama ifuatavyo: Hadi 2002 kulikuwa na *High Court Registries* 11 tu kwa nchi nzima, kwa nchi iliyokuwa na mikoa 20 (Tanzania Bara). Isitoshe, *Registries* zilizokuwepo hazikuwa na Majaji wa kutosha, kwani ukiondoa Dar-es-Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga na Tabora, hakuna Mahakama yenye Jaji wa Kudumu zaidi ya moja, jambo linalofanya utoaji wa haki kuwa wa tatizo na wenye ucheleweshaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo baya zaidi hasa katika masuala ya Haki za Binadamu, kwani Katiba inatoa Mamlaka ya Kusikiliza *(Original Jurisdiction*) kwa *High Court* tu na *Basic Rights and*

*Enforcement Act, 1994* inataka kesi zote za uvunjaji wa Haki za Msingi zisikilizwe na *Full Bench* ya *High Court*, yaani Majaji watatu. Hali hii pamoja na kansa ya ufinyu wa Bajeti, ukosefu wa usafiri na nyenzo kwa Majaji imefanya hali kuwa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa mwaka jana na *LHRC* unaonyesha kuwa kesi nyingi zilizofunguliwa kwenye Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa, 2002 zilibaki bila kushughulikiwa kutokana na upungufu wa Majaji. Hali inaonekana ni mbaya zaidi kadri unavyoshuka katika ngazi ya Mahakama ya Wilaya na Mahakimu Wakazi. Athari ya ucheleweshaji imeonekana dhahiri katika kesi ya Jafari Bakari na Saidi Ibrahim, waliotuhumiwa kwa kesi ya mauaji na kubakia rumande kwa miaka 12 na hatimaye kukutwa hawana hatia, lakini wamekwisha kukaa rumande kwa miaka 12.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa hii ni haki iliyonyimwa kwa mabavu, na mwananchi kunyanyasika bila sababu. Serikali inawajibika kusimamia utekelezaji wa sheria na hasa kulinda misingi ya haki, hasa pale inapopindwa, mathalan, mtu anapobambikiziwa kesi bila sababu na Polisi, Polisi kuchelewesha upelelezi bila sababu, mambo ambayo hivi sasa yamepelekea watuhumiwa waliokuwa rumande kugoma, ikiwa ni pamoja na kugoma kula, kama ilivyotokea kwa watuhumiwa waliokuwa Gereza la Segerea, tarehe 20 Aprili, 2002.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inadhani pamoja na kuundwa kwa Tume ya Haki za Binadamu iwapo hatua za makusudi hazitachukuliwa masuala mengi yatakayoshughulikiwa na Tume hii yatabakia kwenye mashelfu tu. Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Rais, achukue hatua ya kuteua Majaji wa kutosha kadri ya ikama inayotakiwa, kwani kwa bahati nzuri nchi yetu, ina Wanasheria wengi wenye sifa ya kuteuliwa kuwa Majaji akiwemo Dr. Masumbuko Lamwai. *(Makofi)*

Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, ilipotembelea Idara ya Mahakama ilielezwa kwa tatizo kubwa ni nyumba za kukaa Majaji. Tunadhani, kutokana na unyeti wa masuala haya, hoja ya nyumba haina msingi, kwani tunatumia fedha nyingi mathalan, kwenye Takrima ya Serikali kama ilivyo kwenye Bajeti, pamoja na mambo mengine ambayo yanaweza kusubiri, kwa kiwango cha billioni 10 kila mwaka. Ni ajabu iwapo nchi inayojali na kukiri kuwa inaendeshwa kwa Utawala wa Sheria kushindwa kuwa na Majaji wa kutosha kutokana na uhaba wa nyumba. Tunaitaka Serikali ichukue hatua ya haraka kurekebisha jambo hili kwa kuangalia vema vipaumbele vyake katika Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana na hali duni ya maslahi ya watumishi wa Idara ya Mahakama. Hali tuliyoona katika Mahakama ya Kisutu au Manzese ambapo watumishi wa Mahakama wanaenda kujisaidia katika nyumba ya jirani au kutumia vifaa vilivyopelekwa Mahakamani kama *Exhibit* kama nyenzo za kazi ni hali ya kutisha.

Kambi ya Upinzani inaamini kabisa, kama Waziri wa Fedha alivyoatamka mbele ya Kamati, pale Dar es Salaam, atachukua hatua ya makusudi kurekebisha mazingira ya kazi katika Mahakama za Mwanzo katika Bajeti ya 2004/2005. Lakini kwa kuanzia na Mahakama ya Mwanzo ya Manzese na Mbagala na zile zote ambazo zina hali mbaya kama Mahakama ya Manzese hasa kwa kuanzia Bajeti ya mwaka huu. Tunaitaka Serikali iharakishe kufanyia kazi Taarifa ya Jaji Mroso kuhusu maslahi na Mazingira ya Mahakimu, Majaji na watumishi wa Idara ya Mahakama wakiwemo Wanasheria, ambao kwa bahati mbaya tumewapoteza wengi kwa kukimbilia maslahi mazuri katika Sekta binafsi. Ni jambo la kushangaza kuona kuwa Mwanasheria aliyehitimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mwaka moja na wenzake wengine, kiwango kile kile, anashindwa kimaslahi na mwenzake huyo mwingine aliyeko kwenye Idara nyingine ya Serikali kwa zaidi ya mara mbili au tatu.

Pia tunaitaka Serikali irekebishe hali hii mara moja, ili kuondoa kujengeka kwa matabaka katika nchi yetu, jambo ambalo linahatarisha kumomonyoka kwa umoja na mshikamano wa Kitaifa. Katika ngazi ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo mishahara ya Mahakimu ni midogo kiasi cha kutotosheleza mahitaji muhimu ya Mahakimu yenye kulinda hadhi ya Hakimu. Inaelekea kabisa kuwa hali hii ndiyo chanzo kikubwa cha rushwa katika ngazi hii, japo hatuungi mkono hoja hii na wala maadili ya kazi hayaruhusu udogo wa maslahi kuwa sababu ya kupokea rushwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatambua kuwa Mheshimiwa Waziri ametambua tatizo la rushwa katika Idara ya Mahakama kiasi cha kutenga zaidi ya 400 millioni katika Bajeti ya 2003/2004. Pamoja na hatua hiyo nzuri, Kambi ya Upinzani, inatoa tahadhari kuwa tiba ya kweli ya rushwa katika Idara ya Mahakama ni kuwa na Mahakimu na Majaji wa kutosha, mazingira ya kazi yaliyo bora zaidi, vifaa vya kisasa vya kazi. Semina na kubandika vikaratasi *Corruption Free Zone* kwa peke yake haitoshi, kwani makaratasi hayo hubandikwa nje na rushwa hupokelewa kwenye *chamber* na vile vile kutoa masanduku ya maoni kama Waziri alivyosema leo si dawa kwa sababu Watanzania walio wengi hawana utamaduni wa kuandika na wala wengine hawajui kuandika.

Kambi ya Upinzani inamshauri Waziri, afanye zoezi la wateja wa Mahakama kupiga kura ya siri, hasa katika Mahakama za chini, kubaini angalau rushwa katika Utumishi wa Mahakama, kama ilivyofanyika kwenye Idara nyingine hasa vijijini. Ni wazi zoezi hili linahitaji umakini na busara, lakini wateja walioonja joto la kurudi Mahakamani kila wiki 2 kwa muda wa miaka 5 kwa hakika watafunua miujiza iliyoko katika Idara ya Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003 Mheshimiwa Waziri alieleza katika hotuba yake kuwa: "Kuimarisha nidhamu ya maadili ya kazi kwa Mahakimu wetu katika ngazi mbalimbali, kupitia Bodi za Mahakama za Mikoa na Wilaya."

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyoko ni kuwa Bodi hizo hazikufanya kazi zake kutokana na ufinyu wa Bajeti na kutokuwepo utaratibu maalum wa Bodi hizo kupatiwa fedha. Mheshimiwa Waziri alieleza kuwa fedha hizo zingelipatikana kutokana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kambi ya Upinzani ingelipenda kujua nini kimetokea na kwa nini fedha hizo hazikupatikana kama ilivyoelezwa na Waziri. Isitoshe, Kambi ya Upinzani ingelipenda kujua kama kuna *Regulation* maalum zilizotungwa kuendesha Bodi hizo au ni kila Mkoa na Wilaya kujitungia utaratibu wake. Tungependa Waziri afafanue kwa kina jambo hili kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Katika hotuba yake mwaka 2002/2003, Mheshimiwa Waziri alieleza kuwa Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kushirikiana na Mahakama zinaandaa kanuni ambazo zitatoa mwongozo wa uteuzi wa Wazee wa Baraza. Ilielezwa vile vile kuwa kanuni hizo zingeliweka wazi utaratibu mpya wa jinsi ya kuwapata wazee hao, uwiano wa jinsia, muda wao wa kufanya kazi, na udhibiti wa maadili ya kazi yao. Hotuba ya leo ya Waziri haikutamka chochote. Tunataka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu kanuni hizo zimefikia hatua gani mwaka huu na kama ni bado ni kitu gani kimekwamisha kazi hii muhimu isikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na zoezi linaloendelea la kuuza nyumba za Serikali, kwa taarifa tuliyopata wakati Kamati ilipotembelea Idara ya Mahakama, zoezi hili limeathiri kwa sehemu kubwa Idara ya Mahakama, hasa pale wanapochaguliwa Majaji wapya. Hali hii imelazimisha Majaji wapya kupangiwa kukaa Hotelini kwa muda mrefu, hali ambayo inasababisha kiasi kikubwa cha fedha za Idara kulipia gharama za pango badala ya kutumika katika kazi muhimu. Isitoshe, mazingira ya Hoteli, si muafaka kwa Jaji, kutokana na hali halisi ya kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku za karibuni kumekuwa na matumizi mabaya ya vyombo vya dola, au mamlaka za dola kinyume na taratibu kanuni na sheria za nchi. Matukio haya ni kama vile matukio ya kifo cha wananchi 17 mikononi mwa Polisi kule Mbarali 17 Novemba, 2002, tukio la wanachi 6 kufa mikononi mwa Polisi kule Mlimba Morogoro, vijana 6 waliouawa na Polisi kule Mwanza mwaka 2003. Isitoshe, kutokana na taarifa ya *LHRC,* Polisi Magereza mwaka 2002, waliwapiga Makondokta wa Daladala na kuwaumiza vibaya kwa vile tu walivaa unifomu zilizofanana na za Askari wa Magereza.

Mheshimiwa Spika, tarehe 8 Septemba, 2002, askari wa *Mgulani National Service* 12 nao walivamia Kariakoo na kuwavua nguo wanamgambo wa Manispaa ya Ilala na kuwaacha na nguo za ndani, kwa sababu hizo hizo za *uniform.* Tarehe 28, Septemba, 2002, nako askari wa JWTZ nao walivamia Kituo cha Polisi cha Kunduchi kwa lengo la kumtoa mwenzao aliyekuwa kituoni kwa tuhuma ya kufumaniwa. Polisi hao kwa kuzidiwa walikimbia na kuacha kituo. Wanajeshi nao, baada ya kumkosa waliyemhitaji, wakavamia kijiji jirani na kuwapiga wanakijiji na kuharibu mali ikiwa ni pamoja na Gari TZL 7733 na TZM 6853. *LHRC* ilipowahoji wananchi walieleza kuwa matukio hayo yamekuwa kawaida kwao. Kule

Mwanza nako 27 Oktoba, 2002, Bwana Renatus Vedastus, alipigwa vibaya na Polisi akiwa rumande, hadi kulazwa Bugando kwenye *Intensive Care Unit.*

Mheshimiwa Spika, kule Tarime wafungwa na watuhumiwa waliokuwa rumande waliwekwa bila nguo, hali ambayo ilithibitika pia kule Kyabakari Matukio haya yametokea pia kule Zanzibar. Kuna taarifa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, aliamuru nyumba za kijiji cha Nyamuma na kitongoji cha MCH Bomani Mgumu, Wilaya ya Serengeti Mkoa wa Mara zichomwe moto. Matokeo yake ni maghala 696 yaliteketea, nyumba 534 ziliteketea moto, ng'ombe 388 walikufa, mbuzi 1240, kondoo 1,002, kuku 8,421 na mabati 260 yaliteketea, majembe ya plau 100 na minyororo ya ngo'mbe 100, baiskeli 41 na vifaa mbalimbali vya ndani.

Kambi ya Upinzani inataka kupata taarifa kamili Serikali imechukua hatua gani kwa hawa wahalifu wachache ambao licha ya kuchafua jina la Majeshi na Serikali yetu, pia wanachafua rekodi ya Tanzania ya Haki za Binadamu kwa maamuzi yao yasiyofuata sheria. Kambi ya Upinzani imesikitishwa kuona vyombo vya dola, ikiwemo Idara ya Mahakama wakitupiana lawama hasa katika kesi ya Mbarali na tungelipenda Serikali itoe tamko rasmi kuhusu hali hii ili tusiendelee kuona majanga ya aina hii yakitokea katika nchi yetu ambayo inajulikana kote kama kisiwa cha Amani. Katika haya kwa kweli tutapenda jibu la kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria yetu, *Penal Code*, kifungu cha 197 ndicho kinachotoa Adhabu ya kifo kwa makosa yaliyoainishwa. Suala hili, limewakilishwa Mahakama ya Rufaa, katika kesi ya R *vs* Mbushu Dominic, ambapo iliamuliwa kuwa Adhabu ya kifo haiko kinyume cha Katiba ya Jamhuri kwa sababu inaokolewa na kifungu cha 30 cha Katiba na hivyo Mahakama ya Rufaa ilitengua uamuzi wa aliyekuwa Jaji Mwalusanya wa Mahakama kuu aliyeamua kuwa: *"Death penalty is unconstitutional for violating the right to life and provisions against torture, cruel, inhuman or degrading punishments or treatment."*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hukumu hii, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa zimekuwa zikihukumu watuhumiwa wa mashtaka yaliyoanishwa adhabu ya kifo kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, pamoja na hukumu hizo, taarifa zilizoko ni kuwa adhabu hizo daima hazikutekelezwa, isipokuwa chache sana tangu uhuru hadi leo. Rais, ambaye sheria inamtaka kuidhinisha adhabu hiyo, amekuwa akikaa kimya bila kutekeleza amri hiyo ya Mahakama, na au baada ya muda mrefu kupita hupunguza adhabu hiyo, kuwa kifungo cha maisha, mathalani, kati ya 1995 hadi 2002, Mheshimiwa Rais, ameisha kupunguza adhabu za kifo 100 kuwa vifungo vya maisha.

Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, pamoja na nia njema ya Mheshimiwa Rais, kukaa kwa muda mrefu wakati aliyehukumiwa hajui hatima yake, ni kumpa mateso makubwa ya kiakili *(fear and psychological torture),* licha ya adhabu ya kuwa ndani ya gereza. Kambi ya Upinzani, inapendekeza basi, kwa kuwa sheria hii imekuwa haitekelezwi, na ili kupunguza adhabu hiyo ya pili kwa mfungwa ambaye kwa hakika hakuhukumiwa ambayo haiko pia nayo kisheria, Mheshimiwa Waziri alete Bungeni marekebisho ya kifungu hiki cha sheria, ili adhabu ya juu katika Jamhuri ya Muungano iwe Kifungo cha Maisha, ambayo kwa kweli ndiyo adhabu, kwani aliyehukumiwa kifo akisha kufa, haiwi adhabu tena kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani tukitegemea kuwa tutapata majibu ya kina.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, *(Makofi)*

**MHE. ASHA ALI NGEDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa napenda kumpongeza Mwenyekiti wa CCM Taifa, ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuteua Majaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwataja majina Majaji hao, kwanza kabisa ni Mheshimiwa Jaji Mkuu, Barnabas Samatta, ni Majaji watatu ambao walioweza kufanikisha kutoa haki za wanawake waliofukuzwa uanachama na kupoteza Ubunge. *(Makofi)*

Pongezi hizi za Mheshimiwa Barnabas Samatta, zinakwenda sambamba pamoja na Majaji watatu kwa sababu hata kama una Majaji wazuri lakini ikiwa Jaji Mkuu hana ufanisi wa kazi itakuwa kazi bure. Kwa hiyo, pongezi za Mheshimiwa Barnabas Samatta, zinakwenda sambamba na Mheshimiwa Jaji Luanda, Mheshimiwa Ihema, Jaji Kileo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nashindwa kuelewa Mheshimiwa Benjamin Mkapa, anapofanya uteuzi huu sijui huwa ana akili gani. Maana yake ingekuwa vizuri hata viongozi wa Upinzani pia wangekwenda kujifunza kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si kama nasifia tu lakini kwa kweli Mheshimiwa Benjamin Mkapa, angefungua darasa la kufundisha busara na hekima kwa viongozi wa Upinzani hususan Mheshimiwa Katibu Mkuu wangu wa *CUF.* Ikiwa anashindwa na Katiba ya Chama je, akikabidhiwa nchi, Katiba ya Nchi ataiweza? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi katika Wizara hii napenda kuchangia katika Idara ya Mahakama.

**MBUNGE FULANI:** *Hear hear !!!!*

**MHE. ASHA ALI NGEDE:** Mheshimiwa Spika, kutokana na ufanisi wa Majaji wanafanya kazi zao vizuri sana lakini hauendani na vitendea kazi ambavyo vimepitwa na wakati. Jaji anasikiliza kesi vizuri sana, anatoa hukumu vizuri sana, lakini tatizo linakuwepo katika nakala ya hukumu. Hii yote inatokana na uhaba wa vitendea kazi. Mpaka leo Mahakama Kuu bado ina *manual typewriter* ambacho ni kitu cha kichekesho kwa Mahakama Kuu ya Tanzania kuwa na vitendea kazi kama hivyo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri katika Bajeti yake aangalie ununuzi wa kompyuta. Kuna kompyuta lakini hazitoshi. Hivyo basi katika usumbufu huu wananchi wengi hupoteza muda wao kufuatilia nakala za hukumu badala ya kupoteza muda huo kuupeleka katika kuboresha mambo yao na katika ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa sisi kama wanawake unamkuta mwanamke pale anafuatilia nakala ya hukumu mwisho karibu anataka kupewa talaka. Anaaga kwa mume wake anafuatilia nakala ya hukumu. Sasa nakala ya hukumu hii wewe unatoka Kondoa, mwezi mzima nakala ya hukumu hupati kwa nini? Mheshimiwa Waziri naomba uangalie isije nakala ya hukumu ikavunja ndoa za watu. *(Makofi)*

Pia utakuta mtu labda ana kesi ilikuwa ya Mahakama Kuu lakini yeye anakaa Morogoro. Kipato chenyewe cha wananchi wa Tanzania ni cha chini kwa watu wa Vijijini, lakini utakuta anarudi mara tano, sita na kadhalika kwa hiyo hilo pia nilikuwa napenda liangaliwe. Pili kuna kero hii ya Makarani wa Mahakama Kuu. Wale Makarani hujifanya wao wanajua hata Majaji wao wako chini. Unaweza ukamwuliza swali tu pale leo vipi kesi yetu iko *chamber* au *open court,* basi hata kukutazama pia hataki anajifanya yeye ana shughuli nyingi utafikiri karani wa Gavana mafaili tele huku na huku, lakini hana lolote. Anataka tu uzungumze tu vizuri na ndipo atakwambia na faili lako ataliweka juu na Jaji mwenyewe atalikuta faili liko juu. Basi ni mambo ya ajabu ajabu tu. Kwa kweli nilikuwa naiomba Wizara inapoajiri Makarani pia waangalie *background* zao sio mtu tu kwa sababu mjomba wake pale nani nani basi anachukuliwa na pili, nilikuwa napenda semina kwa Makarani. Pale wanafikiri labda wako kwenye *Private Company* kumbe hiyo ni Mahakama ambayo inahudumia wananchi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba wafanyiwe semina mara kwa mara wajue wako pale kwa sababu gani, sio wako pale tu kwa sababu ya kupata mshahara. Halafu pili kwa Makarani hao ni kweli kipato chao hakitoshi, lakini pia ndiyo hivyo hali ya nchi lakini namwomba pia Waziri aangalie marupurupu yao angalau wapate chai na chakula cha mchana. Basi kama watashindwa chakula cha mchana wapatiwe chai, kwa kweli wanatia huruma.

Baada ya hapo kabla sijaunga mkono hoja nilikuwa napenda pia kuzungumzia marupurupu ya Majaji. Ni kweli Majaji wameuziwa nyumba za Serikali. Lakini mimi naona moja hata haitoshi kama kungekuwa na uwezekano Majaji wakauziwa hata mbili mbili. Majaji wanafanya kazi ngumu na vishawishi vingi na kila aina ya rushwa lakini pia wanakwepa. Kwa hiyo kuwauzia nyumba za Serikali ni moja ya kuwafanya akili zao zitulie na imani kwa izidi kuwa na Serikali yao na wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Halafu nilikuwa napenda kuangalia marupurupu pia kwa sababu Jaji hawezi akaenda kama baa ya Bulyaga iliyokuwepo Temeke kutokana na hadhi yake. Kwa mfano ametoka kazini amehukumu kesi ya kifo au amemfunga mtu aende Bulyaga anapishana na ndugu wa yule mtu ambaye amemfunga au amehukumiwa kunyongwa kwa kweli ni hatari. Kwa hiyo inabidi atafute hoteli yenye hadhi ambayo anaweza akaenda pale akapata bia yake, na hoteli yenye hadhi bia tena haiwi kama baa za kawaida. Pia nilikuwa napenda waangalie kuhusu ulinzi. Kazi zao ni nzito. Kazi ya kutoa haki si kazi ya masihara. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kama wana Polisi mmoja anayelinda ikiwezekana basi hata wawili.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Hoja ya Bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Lakini awali ya yote naomba nimpongeze sana mzungumzaji aliyemaliza, Mheshimiwa Asha Ngede, Mbunge wa *CUF* kwa kuonyesha kukomaa kisiasa. Kwa hakika kama ningekuwa sijaoa ningepeleka barua ya uchumba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kusema kwamba, hoja iliyoko mbele yetu naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mihimili mitatu ya Dola, kwa maana ya Mahakama, Bunge na Serikali, tumekuwa tukinyooshewa vidole kuhusu kero hii ya rushwa na eneo ambalo limekuwa likikemewa sana sana kwamba limekuwa likijihusisha na vitendo vya rushwa ni eneo hili la Mahakama. Lakini napenda kutoa pongezi zangu za dhati kabisa bila kigugumizi chochote kwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Barnabas Samatta, kwa jitihada kubwa anazofanya kusafisha rushwa katika Idara hii ya Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kuna mfano wa kupambana na rushwa ambao unaonekana ni katika Idara ya Mahakama, kuanzia Mahakama Kuu mpaka Mahakama za chini, kwa sababu katika Idara ya Mahakama ndipo tunapoona kwamba, watu wanachukuliwa hatua pale wanapokutwa wamejihusisha na vitendo vya rushwa au pale ambapo watumishi wanaonekana kwenda kinyume na Maadili ya Utumishi wa Mahakama. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Jaji Samatta, pamoja na Waheshimiwa Majaji Wasajili na Mahakimu katika Mahakama za Mikoa, Wilaya na Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufanisi huo, bado kuna maamuzi mengi ambayo yanafanywa na Mahakama zetu ambayo ni maamuzi ya kusikitisha sana na ambayo bado yanaonyesha kuna dalili kubwa za rushwa ndani ya Mahakama. Mfano ni maamuzi mbalimbali ambayo yamekuwa yakifanyika kwenye Mahakama Kuu kuhusu umilikishwaji au uuzwaji wa Kiwanda cha Nguo cha *MUTEX.*

Mheshimiwa Spika, kuna uamuzi ambao ulifanywa na Mahakama Kuu Mwanza, kuinyang'anya Serikali kiwanda kupitia *LART,* ili akabidhiwe mtu ambaye alishindwa kukinunua kiwanda kile. Nadhani hilo ni moja kati ya maamuzi ambayo yanaonyesha kulikuwa na mazingira makubwa ya rushwa kwa Jaji huyo wa Mahakama Kuu Mwanza.

Mheshimiwa Spika, binafsi nina imani kubwa sana na Idara hii ya Mahakama, pamoja na hatua ambazo Idara hii inazichukua chini ya Jaji Mkuu, kupiga vita rushwa. Hizo ni hatua nzuri na ambazo nadhani waendelee nazo.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la tatizo la uchakavu wa majengo ya Mahakama. Nadhani suala hili hivi sasa lipo kila sehemu katika nchi yetu. Mazingira ambayo Mahakimu wanafanyia kazi ni mazingira ya kusikitisha sana! Sidhani kama kuna mtu anaweza kufanya kazi yake vizuri na akaweza kutekeleza majukumu yake vizuri kama hajajengewa mazingira ambayo ni mazuri. Kwa mfano, majengo ya Mahakama ya Mkoa wa Mara, majengo ya Mahakama ya Wilaya ya Musoma na jengo la Mahakama ya Mwanzo Musoma Mjini ni majengo ambayo yamechakaa sana na yanahitaji kukarabatiwa, lakini kwa muda mrefu, zaidi ya miaka kumi majengo hayo hayajakarabatiwa na yako kwenye hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, nilibahatika kuwa Mjumbe wa Kamati ya Kisekta ya Utawala, Kamati hizo sasa hivi hazipo na niliwahi kuzungumzia jambo hili, kwamba wakati mwingine inatia aibu kidogo, inafikia mahali hata vyoo tu kwenye Mahakama hakuna! Vile vile, kwenye taarifa hapa ya Msemaji wa Upande wa Upinzani ameeleza wazi kwamba, walipotembelea Mahakama za Manzese, walikuta wafanyakazi hawana sehemu za kujisaidia, kwa hiyo wanatoka kwenda kutafuta huduma hiyo katika nyumba za jirani. Hii ni kuwadhalilisha Watumishi wa Sekta hii ya Mahakama. Wakati mwingine Hakimu anaweza kuwa yuko kwenye kutoa maamuzi, lakini anafikiria, hivi baada ya hapa nitakwenda wapi kujisaidia?

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, wakati atakapokuja kutoa hoja ya kupitisha bajeti yake, anihakikishie kwamba tatizo la kutokuwepo kwa choo kwenye Mahakama ya Mwanzo ya Kitaji Musoma, litapatiwa ufumbuzi. Ni aibu kubwa kwa Mahakama ile, kwa zaidi ya miaka mitatu watumishi, wakiwemo na Mahakimu, hawana sehemu ya kwenda kujisaidia!

Mheshimiwa Spika, nimeangalia kwenye *vote 40, sub vote 2011,* nimeona kuna fedha zimetengwa pale kiasi cha Shilingi milioni 100, lakini haijaelezwa ni Mahakama zipi za Mwanzo ambazo zitanufaika na hizi fedha. Nina imani katika Mahakama ambazo zitanufaika na fedha hizo itakuwemo Mahakama ya Mwanzo ya Musoma, hususan matengenezo ya choo. Pia, Mahakama ya Mkoa na Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda nizungumzie ni kuhusu maslahi ya Watumishi wa Sekta ya Sheria. Kwa kweli Tanzania bado tunawalipa Watumishi wa Sekta ya Sheria mishahara na marupurupu madogo sana ukilinganisha na wenzetu wa Kenya na Uganda, ambao sasa ni *Partner States,* kwa maana ya kuwa ni wenzetu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wakati mwingine tunalalamika kwamba kazi hazifanyiki kwa kiwango cha ufanisi wa kutosha, lakini hivi ni nani anaweza kufanya kazi wakati maslahi yake ni duni na hana uhakika wa kuishi kwa mwezi mzima?

Mheshimiwa Spika, isitoshe fani hiyo ya Sheria hivi sasa ni fani ambayo ina soko kubwa kwenye ajira. Kwa hiyo, tutakuwa tunaajiri Wafanyakazi, Mahakimu na Wanasheria wa Serikali, lakini baada ya kipindi kifupi tutajikuta hatunao kwa sababu wanaingia Serikalini ili waweze kupata uzoefu wa kazi, maana katika sehemu nyingi wataambiwa wawe na sifa za kitaaluma na wawe na ujuzi wa miaka miwili au zaidi. Kwa hiyo, mtu anakuja Serikalini anafanya kazi katika mazingira magumu ili aweze kupata uzoefu na baada ya hapo anaondoka.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba, katika Bajeti inayokuja, Mheshimiwa Waziri, aliangalie sana suala hilo na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, yupo hapa na amekwishatamka kwamba kutakuwa na ongezeko, lakini basi mbali na mishahara tuangalie tunaweza kuwasaidia vipi Wanasheria. Katika nchi za wenzetu wanapewa mikopo ya *furniture,* wanapewa mikopo ya kujenga nyumba, mikopo ya magari na kadhalika na mwajiri anakuwa ndio msimamizi wa mikopo hii ambayo inamuwezesha angalau kuondoa ule ukali wa maisha. Nadhani hii itatusaidia kuweza kuwa na watumishi ambao watakuwa na moyo wa kufanya kazi kwa dhati na kwa ufanisi kabisa. Kwa hiyo, nashauri tuangalie ni jinsi gani tutaboresha maslahi ya hawa wafanyakazi wa Sekta hii ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu malipo ya Wazee wa Mahakama za Mwanzo. Ni kweli kwamba, Serikali imechukua uamuzi mzuri kwa kuongeza posho za Wazee wa Mahakama kutoka Sh.200/= kwa mwezi hadi Sh.1,500/= kwa kesi moja. Hawa Wazee wanaacha shughuli zao na wanashinda Mahakamani kwa muda mrefu sana, lakini pamoja na kwamba wanafanya jitihada na kesi zinamalizika katika wakati unaostahili, tatizo linalojitokeza ni upatikanaji wa malipo yao ya posho kwa wakati. Posho hizi za Wazee wa Mahakama zimekuwa ni kero kwa sababu wakati mwingine inachukua muda mrefu sana wao kuweza kupata malipo yao, wakati wamekwishatekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa hii kero ya posho za Wazee wa Mahakama tunaiondoa kwa sababu baada ya Serikali kuamua posho hiyo kupanda kutoka Sh.200/= hadi Sh.1,500/=, maana yake ni kutokana na uwezo uliopo wa Serikali wa kuweza kuwalipa. Kwa hiyo, hakuna sababu ni kwa nini fedha hizo wasiweze kupatiwa kwa wakati unaostahili. Namwomba Mheshimiwa Waziri, asaidie Wazee wa Mahakama za Mwanzo walipwe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nizungumzie kuhusu tatizo la ucheleweshaji wa kesi. Mheshimiwa Waziri, alifanya ziara kwenye Magereza yetu ya Mkoa wa Mara. Alitembelea pale na alikuta msongamano mkubwa sana wa mahabusu na kulikuwa na kesi za kusikitisha sana. Kuna wengine wana kesi ndogo ndogo mfano mtu kaiba kuku au ameshindwa kuchangia mchango wa shule, wanakamata mali zake, akienda kuzikomboa anakamatwa na Sungusungu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie kwamba, tunapozungumzia dhana ya Utawala Bora, maana yake ni kuhakikisha tunawatendea haki raia wa nchi hii. Inakuwaje mtu aendelee kuwa mahabusu kwa zaidi ya miaka miwili,mitatu, kwa kutopatikana ushahidi? Nashauri pale ambapo ushahidi unakuwa umekosekana kwa kipindi kirefu, hawa mahabusu waachiwe na pindi ushahidi unapopatikana washtakiwe. Kumuweka raia mahabusu kwa zaidi ya miaka miwili, mitatu au minne, nadhani huu ni ukiukwaji mkubwa kabisa wa haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, alipotembelea lile gereza, nadhani alipata fursa ya kuzungumza na baadhi ya mahabusu. Cha ajabu sana unakuta kuna vijana wadogo kabisa wamechanganywa na watu wazima, lakini kesi zenyewe si za msingi. Mfano, unakuta mtu ametuhumiwa labda aliiba samaki, halafu eti hakuna ushahidi kwa miaka miwili, mitatu! Sasa, sijui kama huu ndio Utawala Bora tunaokusudia kujenga kwenye nchi hii. Pia, tunapozungumzia haki za binadamu maana yake tusipotekeleza majukumu yetu upande wa Mahakama, tunaongeza kazi nyingi zaidi kwenye upande wa Tume ya Haki za Binadamu, kwa sababu haya yote yatakwenda kwenye upande mwingine wa malalamiko kwenye hiyo Tume ya Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, namshauri Waziri, aangalie suala hilo kwamba, kwa zile kesi ambazo zimekuwa Mahakamani kwa muda mrefu sana, kuna umuhimu wa kuangalia ili ziondolewe, kwa sababu kesi nyingine ni za kubambikiwa. Wananchi wanabambikizwa kesi ambazo hawakuhusika nazo na nadhani hizi ndio kesi nyingi ambazo zimekuwa zikikaa muda mrefu Mahakamani bila ushahidi kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, kabla sijagongewa kengele ya pili, napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri kuwa, kuna umuhimu sasa wa kujenga mazingira mazuri zaidi kwa watumishi wa Sekta hii ya Sheria na hususan Mahakama kuboresha maeneo wanayofanyia kazi watumishi hao na kuwapatia nyenzo za kutosha ili kuondoa malalamiko madogo madogo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda niwape pole Idara ya Mahakama, kwani kwa muda mfupi wamepoteza Viongozi na Wanasheria mashuhuri, hilo ni pengo kubwa katika Wizara ambayo sasa hivi ina uhaba wa watu wa namna hiyo na inachukua muda mrefu kuwajenga watu kufikia kwa wale ambao wamefariki katika kipindi hiki wasiopungua Majaji sita.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda nichangie kwa kusema kwamba, nadhani Wizara hii inahitaji kuimarisha *training*. Ninapendekeza moja kwa moja kwamba, wafikirie kuanzisha *Law School,* ambayo itakuwa ina mtiririko wa kutoa *certificate* na kutoa *degree.* Kama tumekuwa na *Engineering Departments* zinazopanuliwa kuwa *colleges*, ni kwa nini kusiwe na *college* ambayo inahusika tu na mambo ya Sheria ili tujaribu kupunguza uhaba uliopo katika eneo la Mahakama na utoaji wa haki za kisheria katika nchi hii?

Mheshimiwa Spika, najua kuna *training* katika Chuo Kikuu, lakini idadi ya wale wanaohitimu hawatoshelezi mahitaji na pia wale wa Lushoto hawatoshelezi mahitaji. Kwa hiyo, ni vizuri tufikirie hivyo katika kipindi hiki cha kuimarisha elimu, basi tuwe na *college* ambayo ni *Constituent College* na haitakuwa ajabu kwa sababu Chuo Kikuu chetu kilianza na Sheria pale Lumumba na ndicho kilichozaa maeneo mengine ya *engineering, social sciences* na kadhalika. Nadhani wakati umefika kwa suala hilo kufanyika.

Mheshimiwa Spika, tatu, katika hiyo *training* napenda kuuliza, labda Mheshimiwa Waziri, atanisaidia. Kuna Mahakimu nadhani hasa katika ngazi za Wilaya ambao hawajaonja *training* hata mara moja, sijui yule Hakimu wa Ukerewe bado mnamkumbuka kama yupo? Nadhani yule amesahaulika kwa sababu hajawa *trained* na nina mashaka hata hizi Sheria tunazozitunga kama nakala zake anazo! Sasa kama hana nakala, anahukumu kufuatana na mtiririko upi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kubwa sana, siyo kwetu tu, lakini nadhani katika Wilaya nyingi za pembezoni Mahakimu hawapati Sheria hizi ambazo tunazipitisha hapa. Hata Sheria ya Ardhi ambayo ni muhimu wengi hawana! Kwa hiyo, bado wanaendesha vitu vyao kama walivyozoea! *They are using their common sense, which is never common.* Suala hilo linaleta rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata ukipata hukumu wakati mwingine ukiziangalia kwa kweli hazilingani na mazingira halisi na nitatoa mfano. Kwa sababu ya kukosa *training* huyu anayehukumu anakosa kuoanisha hali ya mazingira na haki kwa sababu haki haiji tu kwa sababu Sheria inasema hivi, nadhani una uwezo wa kuchambua na kuoanisha.

Mheshimiwa Spika, nina mfano uliotokea Ukerewe. Kuna Shule moja inaitwa *Ihebo Primary School*, wakati wamepata fedha za kupanua majengo ya Shule, Wananchi wa Kijiji kile walijitahidi sana kuijenga Shule yao, lakini iko karibu na madhehebu ya Dini fulani. Walipomaliza ile kazi, yale madhehebu yakaenda Mahakamani kusema ardhi ni yao na Shule ile ihamishwe, wakati majengo yameshakamilika zaidi ya madarasa manane!

Mheshimiwa Spika, Jaji yule aliyapa haki yale madhehebu ya Dini! Nilishindwa kuelewa kama Jaji yule tuko pamoja naye katika kuleta maendeleo ama yeye anaelekea wapi? Ninafikiri Sheria inapohukumu ni lazima iende na mazingira. Kama nchi inataka kusomesha watoto haki unampa nani? Unawapa watu wawili/watatu ambao wanaleta fujo na kwa bahati mbaya hawakuwa wote wa dhehebu hilo au kwa sababu tu wamejenga hoja au unawapa watoto na jamii ambayo ndiyo inafanya kazi katika eneo hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii yote inatokana na ufinyu wa ku-*train* watu na kuwaacha waka-*decompose* wakiwa katika maeneo ambayo ni *remote* kama yale ya Ukerewe. Mtu anatafsiri kwa jinsi alivyoamka, kama amekula ugali wa muhogo hukumu ni tofauti, kama kala sato hukumu yake inakuwa ni tofauti. Kwa hiyo, napenda muwasaidie kwa *training*, siwalaumu. Hata kama mie ningekuwa Hakimu, sina kitabu, sina maelekezo, sina semina, siitwi kwenye *training*, nadhani ningefinyanga finyanga hivyo hivyo. Kwa suala hili la *training* muangalie kwa maeneo yote na siyo kwa wale waliopo Dar es Salaam na kwenye Miji tu, nadhani mfanye vizuri kusaidia katika kuleta haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu mlundikano wa kesi. Hili ni suala la kuvunja haki za binadamu na ninadhani hatuhitaji kulisemea zaidi. Kama hatuwezi kumaliza kesi, basi tutunge Sheria ya fidia. Mfano mtu anakaa miaka 10 mahabusu hadi kasahaulika, halafu anakuja kuambiwa huna kosa! Ameumia yeye, wameumia watoto wake na wote wanaomhusu, ametengwa kutoka katika jamii na kuleta maendeleo katika jamii, ni nani anayemfidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine linalohusiana na mlundikano wa kesi ni kwamba, katika Sheria za Mahakimu nadhani wanaruhusiwa kwenda kutembelea magerezani, wakikuta kuna watu wenye kesi ndogo ndogo, kwa mfano, mtu kaiba kuku au kaiba muhogo, wanaweza mara moja wakazi-*clear* zile kesi na zikaisha watu wakaanza shughuli nyingine. Nadhani hiyo kazi haifanyiki, hawatembelei magereza, kwa hiyo, hawajui ni watu wangapi wamelundikana humo mpaka watakapoletewa mafaili. Naomba Majaji na Mahakimu wajitahidi angalau mara moja kwa wiki wapite ku-*assess* kilichopo huko magerezani na watumie nafasi hiyo kuwasaidia wale wachache ambao wamelundikana mle bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachonishangaza zaidi ni kwamba, ukipita magereza kuna rangi nyingine sizioni huko. Swali langu ni kwamba, je, watu hao hawafanyi makosa? Rangi unayoiona ni kama hii yangu tu, unafikiri tuko *South Africa* wakati wa *apartheid*, unapoangalia ule mtiririko wa nani yuko mahabusu. Naomba kwa suala hilo niishie hapo, nadhani Mheshimiwa Waziri, ameelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ni zito zaidi ni hili la mirathi. Kuhusu mirathi Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba linashughulikiwa. Nimeingia ndani ya Bunge toka mwaka 1980, tumeendelea kusema hivyo hivyo, tunalishughulikia, lakini baada ya kuwa Mbunge wa Jimbo, ndiyo nimeona uzito wake na suala hili linahusiana na Mahakama kwa sababu utaratibu uliopo unahusisha mirathi na uthibitishwaji wa mrithi na Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wanahangaika wanatoka Vijijini, lakini kinachoumiza zaidi mtu amemaliza kupiga picha zote, amepata maandishi yote na kila kitu anapopeleka kwa Hakimu, Hakimu anasema nitapeleka Mwanza. Hapa nitatumia mfano wa Ukerewe. Huko Mwanza faili halifiki, Ukerewe faili halipo! Anaanza *process* upya! Mtu huyu anachoka mpaka anafariki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo mifano ambayo kumekuwa na ngazi mbili au tatu za watu wanoshughulikia mirathi ya mtu huyo huyo na ikiwa labda ni mzazi yaani mtu mzee atoke Kijijini, atafute picha aangalie urithi ampelekee Hakimu, halafu Hakimu huyo apoteze faili, kwa kweli mtu huyo haelewi.

Nadhani Mheshimiwa Waziri, atakubaliana nami nikachukue hiyo mifano na hao Mahakimu wawajibishwe. Haiwezekani kutesa watu namna hii! Wakati mwingine ni akina mama na watoto, wengine watoto wao wameachishwa Shule kwa sababu wamezungushwa mpaka imefika mahali mtoto anafukuzwa Shule wakati pesa ambazo zinatokana na mirathi zipo na angeweza kuendelea na Shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani nitamsaidia Mheshimiwa Waziri, nitaorodhesha wale wote ambao wamehangaishwa kwa namna hii, nimletee halafu atusaidie, labda tuko sehemu za mbali mno na mahali ambapo haki zinatolewa. Akinamama wameteseka, wazazi wa vijana waliofariki wameteseka na watoto wa wale marehemu wameteseka bila haki kupatikana. Kwa hiyo, ucheleweshaji wa Sheria hii ni ile Wanasheria wanasema: *"Justice delayed is justice denied"*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, kwa kuangalia mazingira yetu sasa hivi suala la ushirikina limeonekana kutawala sana katika jamii yetu na kuendelea kulipuuza ni kutowatendea haki Watanzania. Ni vema tuiangalie Sheria ya mwaka 1923 ambayo imetokana na *Indian Law* ya kuhusu uchawi.

Mheshimiwa Spika, ninataka ku-*declare* hapa kwamba, bahati nzuri nilipokuwa kwenye Makao Makuu ya Chama, niliteuliwa kuongoza ujumbe uliokwenda kuangalia mauaji yanayotokana na uchawi katika Kanda ya Ziwa. Kitu cha kwanza nilichotafuta ni hiyo Sheria, Sheria hiyo imeandikwa Kiingereza, lakini mchawi hajaenda Shule! Sasa unampa mtu aitumie, mazingira yenyewe ni ya kiajabu ajabu na Sheria yenyewe iko katika Kiingereza na imetokana na *Indian Law*!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri katika Sheria ambazo zinahitaji kutazamwa sasa hivi kwa haraka ni Sheria ya uchawi. Uchawi na ushirikina umeanza kututawala kiasi kwamba, ita-*erode* hata mafanikio ya sayansi na teknolojia ambayo tumeyapata. Sheria yenyewe kwanza kuipata ni matatizo, nadhani hata Waziri nikimwomba hiyo Sheria atatafuta kweli kweli. Nina nakala yangu sikupi, sitampa. Sheria hiyo haipatikani kwa urahisi na matatizo yale yamesambaa katika jamii na ndio yanatuletea migongano ya kila aina katika jamii. Napenda kusema kwamba, Wizara hii ichukulie mambo kwa haraka kuliko inavyofanya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kusema kwamba, Mikataba tunayopambana nayo katika uwekezaji ni kutokana na Wanasheria wetu kutotusaidia kama wazalendo kuisoma. Mfano ni Mikataba ya Madini na Mikataba ya Ardhi na hasa hiyo ya ardhi ni lazima wanasheria wakae chini waisome. Hao watu tunaotaka kuwaleta huku, ambao wanatoka Zimbabwe na kadhalika, kwa sababu kule wamepambana na Sheria kali za ardhi wanataka kuingia hapa, suala hilo tulisome sana na ikibidi tuoanishe Mikataba ya Kimataifa na Sheria zetu ili na sisi twende na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wataalam wenzake, kwa maandalizi ya hotuba hii. Lakini nawapongeza zaidi Idara ya Mahakama, kwa jinsi wanavyojitahidi kupunguza kesi na kupambana na rushwa ambayo inatupaka matope katika nchi yetu. Naomba waendelee na waweze kutumia haki kabisa katika kutoa haki kwa Wananchi na vile vile, katika kuleta sura nzuri ya nchi yetu kama tulivyojijengea Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, ninaipongeza dira ya Wizara hii, naona kwamba kwa jinsi walivyoainisha dira katika kitabu hiki, kama mambo yaliyoainishwa humu yatatekelezwa, nina matumaini makubwa ya mafanikio ya kazi kwenye Wizara hii katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo napenda kulizungumza moja kwa moja ni haya maandalizi ya Sheria ya Mirathi. Ninaona Wizara imepania kubadilisha Sheria nyingi, nawapongeza kwa hilo, lakini suala la mirathi ni suala ambalo linahusu binadamu na maendeleo yake na jinsi alivyoishi katika kujijengea mambo ya kumsaidia akiwa katika ulimwengu huu. Lakini kwa sababu pengine sababu ya kifo cha mmojawao huyu, mtu anapunguziwa maandalizi yake aliyojiwekea kuishi katika ulimwengu wa mwili kwa sababu Sheria haimsaidii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, ametueleza kwamba, Sheria inaandaliwa na kwamba italetwa, ninaomba jambo hili liletwe haraka. Pengine wale ambao hawajaonja tabu ya kunyang'anywa mali zao baada ya mmojawao kufariki hasa mume, hawaoni uchungu. Au wale ambao wanaona kwamba suala hili litaingilia Sheria za Dini, naomba waelimishwe kwa sababu Serikali haina dini, watu wake ndio wana dini. Sasa yule ambaye atafuata Dini yake kama ni Muumini halisi, hatakwenda kwenye hiyo sheria, atakwenda kwenye Mirathi ya Dini, bila shaka ataona ametendewa haki hata kama hakutendewa haki. Kwa sababu suala la imani ni la roho ya mtu na Mungu, mtu anaandaa safari yake ya kwenda Mbinguni kwa hiyo, hatapenda kutumia Sheria ya Serikali. Hiyo isiwatie hofu watu.

Mimi ni Mkristo, tunagombezwa sana kwenda kwenye ushirikiana na siendi, sijawahi kukanyaga huko kwa sababu ninaandaa safari yangu ya kwenda Mbinguni, nikienda kule kwenye ushirikina sitafika Mbinguni. Basi na Muumini wa Dini, ambaye ataona akienda kutumia Sheria ya Nchi ya Mirathi hatafika Mbinguni, hatakwenda huko. Lakini yule atakayependa kuitumia hii sheria ataitumia. Kwa sababu mambo ya imani na mambo ya haki ya mtu ya Kikatiba, naomba tusiyachanganye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Sheria na Mambo ya Katiba, anapendwa katika Bunge hili, wewe mwenyewe ni shahidi, atuletee hiyo sheria tuipitishe ili wananchi waitumie wanavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la Wazee wa Baraza limezungumzwa sana, tulifurahi tulipopandisha kutoka Sh. 200/= kwenda Sh. 1,500/=. Lakini kesi zinachukua muda mrefu, ingawa katika dira amesema tutapunguza kuondoa mlundikano wa kesi. Kesi moja nilivyoangalia huko vijijini kwetu inaweza kuchukua hata mwezi mzima au miezi miwili. Sasa Sh. 1,500/= kwa mzee yule, anayeacha nyumba yake kwenda kushinda Mahakamani, naona bado haitoshi. Basi naomba Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, labda katika Bajeti ijayo, aongeze fedha kidogo zaidi kwa Wazee wa Baraza kwa sababu kesi zinachukua muda mrefu. Kesi moja shilingi 1,500/=, ambayo inachukua mwezi mmoja au miezi miwili. Sasa ulinganifu wake hapo uko wapi? Naomba hilo aweze kuliangalia kwa sababu tunapozungumza haki, siyo haki kwa wale waliokosa tu, ni haki pia kwa watendaji ambao wanasaidia haki hiyo ipatikane kwa wahitaji wa haki. Basi naomba akalilete hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nimefurahi kuliona katika Bajeti hii ni Mahakama ya Ardhi. Mahakama ya Ardhi anasema haijaanza kufanya kazi. Naomba aharakishe ili Mahakama ya Ardhi ianze kufanya kazi ili watu waweze kupata haki zao. Lakini vile vile wananchi wapewe elimu. Wananchi waelimishwe kutumia hizi Mahakama. Kule kwetu Bukoba tuna matatizo sana ya Ardhi na kesi ni nyingi zipo wengine wanapata haki, lakini inachukua muda mrefu. Sasa tukiwa na miongozo huenda itatusaidia. Kwa hiyo, ombi langu maalum, Mheshimiwa Waziri, atufanyie upendeleo maalum, Mahakama hii itakapoanza kufanya kazi, basi ianzie Bukoba. Ni ombi maalum kwa sababu tunahangaika sana kwenda Mwanza, tunahangaika kuja Dar es Salaam, safari ni ndefu, usafiri wenyewe ni wa shida, meli yenyewe ni moja, ikikwama basi na wakati mwingine inakwama majini.

Mheshimiwa Spika, mimi nakumbuka masuala ya ardhi, sheria ipo inaweza kuwasaidia, lakini watu wenyewe hawajaelimishwa. Nakumbuku kuna mtu ambaye ameweka mfano mzuri katika kesi za mirathi na ardhi. Alikuwa mama mmoja anaitwa Spesioza kule Muleba, yeye kesi yake aliisukuma yeye mwenyewe kwa sababu alikuwa mtoto wa kike pekee na ardhi yake akanyang'anywa na baba zake wadogo. Lakini nakumbuka Mahakama Kuu, ilimrudishia ardhi hiyo baada ya miaka 10 au 12 kwa sababu alisema alikumbuka ardhi ile alianza kulima yeye na mama yake na baba wala siyo ya urithi. Ardhi za urithi ndiyo zinazosumbua. Watuwekee sheria wazi ili tuweze kujua kwamba inakuwaje.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni watoto ambao wanahukumu. Sasa amesema wanajenga Mahakama Mbeya na ile nyingine tuliyokuwa nayo Ilambo ya watoto watukutu. Pale Ilambo - Mbeya, nafasi ni ndogo kama alivyosema yeye mwenyewe anapanua. Lakini pia wakati mwingine ni mbali kuwapeleka watoto watukutu. Wazazi wengine wanakuwa na wasiwasi kwa sababu hata kama mtoto wako ni mtukutuku ni wako yuko Mahakamani, unapenda kuona maendeleo ya mtoto yanaendeleaje. Basi ningemwomba Mheshimiwa Waziri, Bajeti yake atakapoleta labda wakati mwingine tutakapokuwa tumeshasafiri na sisi ahakikishe kwamba Mahakama hizo ziwe katika Kanda, badala ya kuwa mbali sana. Zijengwe katika Kanda ili wananchi wengi wapate huduma na watoto wengi wapate kuangaliwa vizuri.

Napenda kumwomba Waziri ashirikiane pia na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa mfano, watoto wale waliokuwa wanafungwa Gereza la Vijana Wami, wanatunzwa vizuri sana. Mimi nimetembelea lile Gereza nikiwa Afisa Elimu wa Mkoa, tulikwenda kuangalia mitaala yao wanayotumia ikoje. Wanatunzwa vizuri na wanafundishwa vizuri. Sijui kama ni sheria ilikuwa kwamba mtoto atakayefaulu mtihani wa darasa la saba kifungo chake kinaisha anakwenda shule za kawaida za sekondari. Sasa mambo kama haya pengine kwa watoto ambao wako kwenye vituo kama hivi vya kuwarudisha katika tabia nzuri na pengine wasingojee hukumu kwa sababu watoto walioko pale wengi wana hukumu ambazo zingine zilikuwa za kutisha.

Mtoto mmoja nilimwuliza wewe kwa nini umefungwa hapa? Akasema mimi niliua, nikamwuliza uliua namna gani? Wakati tunazunguka naye akasema mimi nilitumwa na wale. Nikamwuliza wale akina nani? Akasema wale majambazi, walinoa panga wakasema mkate baba huyo kichwa. Kwa hiyo, mimi kwa nguvu zangu zote nilimkata kichwa. Nilimwuliza nyumbani kwenu wapi? Akasema Nyamanoro - Mwanza na hiyo kesi mimi nilikuwepo Mwanza wakati nakaa, wakawa wanasema mzee mmoja wa Kigoma amekatwa panga huko Nyamanoro na huyo mtoto akaniambia mimi ndiyo niliyemkata. Sasa akasema ninakazana nifaulu mtihani niondokane na kesi hii kwa sababu najua kwamba nilifanya vibaya nimetubu.

Sasa swali hilo la kwamba ametubu mtoto wa miaka 14, niliona kwamba ni huduma nzuri kwa kesi za watoto kama hawa wadogo wafundishwe, waendelee kufundishwa na kurudishwa katika maadili ya jamii kwa sababu tutakuwa tunamsaidia aweze kuishi vizuri baadaye. Kwa hiyo, ushirikiano huu nilikuwa nafikiri labda utatusaidia na hata Mahakimu wenyewe wawe na nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni Chuo cha Lushoto. Mimi nashukuru Chuo cha Lushoto kimeanzishwa. Ninashukuru kitatufundishia Mahakimu wengi na bila shaka tuna walimu wazuri ambao watawasaidia vijana wetu au wenzetu wanaokwenda kujiendeleza. Lakini nadhani nafasi zilizopo pale ni chache labda kama 120 hazitoshi. Naomba Waziri aongeze, wafikirie namna ya kupanua na walete maombi hapa ili waweze kupanua kile chuo kiweze kuhudumia Mahakimu wengi, kwa sababu kesi zinazolundikana ambazo amezitaja kwenye dira, kama hazina Mahakimu ambao wanaelewa kwa sababu hawawezi kufanya kazi kama hawajui, wengine ndiyo maana wanazichelewesha hizo kesi. Pengine ni namna ya kupoteza muda, lakini kama watakuwa *systematic,* wamefundishwa, wataweza kumaliza kesi haraka iwezekanavyo. Kwa hiyo, naomba Waziri, afikirie kuongeza *in-take* ya Chuo cha Lushoto wawe wanafunzi wengi ambao wataweza kurudi na kuhudumia *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, elimu ya sheria katika Idara ya Sheria naomba iwepo. Sheria zitafsiriwe Kiswahili, sheria ziwe na mahali pa kufundishwa hata katika kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni kwenye Elimu wa Watu Wazima, kwa sababu tunapitisha fedha kila siku za elimu ya watu wazima, basi watafsilieni vitabu wapeni hawa wafundishwe, watu waelewe na Mahakimu wenyewe waelewe. Mimi naona uchungu sana ninapoona Mahakimu wakati mwingine wanahukumu kesi ambayo

hata mimi ambaye sijui sheria hata moja, ningeweza kuhukumu vizuri zaidi kuliko ambaye anaitwa Hakimu. Kwa hiyo, naomba Sheria ziwe katika lugha inayoeleweka na ziwe sheria ambazo zinawasaidia wananchi waelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku moja mimi niliona kitu cha ajabu. Kuna mama mmoja nyumba yake na shamba lake viliuzwa akiwa ndani na watoto. Mahakamani mama yule alipoambiwa nyumba yako iliuzwa kihalali kwa sababu alishtaki kwamba mume wangu ameniuza na watoto nikiwa ndani ya nyumba na hatujatalikiana, sasa alipoambiwa kwamba mume alikuwa na haki ya kuuza shamba akiwemo ndani, akalia mama wee, hakimu akamfunga miezi sita amepiga kelele Mahakamani. Huyu Hakimu kweli? Kwa kweli Waziri ana kazi na Mahakama zina kazi na tunahitaji Mahakimu waadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa tena nafasi ya kuchangia katika hoja ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Naomba nianze kwa kusema kwamba, mimi ni Mjumbe katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa hiyo, mawazo yaliyotolewa kwenye ripoti ya hii Kamati ni sehemu ya mchango wangu. Nayakubali yote kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza mchango wangu, naomba nichukue fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba na Mheshimiwa Jaji Mkuu, kwa vifo ambavyo vimetokea vya Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa katika kipindi hiki. Tumepata pigo kubwa sana hasa ukizingatia uzoefu na uadilifu waliokuwa nao wale Marehemu Majaji. Pia nawapa pole kwa vifo vya watumishi wengine wote vilivyotokea katika hii Wizara. Naomba Mungu awapumzishe kwa amani mahali pema peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwa matayarisho mazuri ya hii Bajeti katika *constraint* walizokuwa nazo na ninawaomba waendelee kufanya kazi hivyo.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo kubwa la kutoelewa shughuli za hii Wizara. Tumeona hata wakati tukijadili katika Kamati, ilipofika wakati ambapo tulihoji kwa nini Mahakama za Mwanzo zisitengewe fedha. Jibu lililotolewa ni kwamba, haziwezi kutengewa fedha zaidi kwa sababu kuna *ceiling* iliyowekwa. Tulipouliza kwa nini hii *ceiling* imekuwa ndogo hivi, tukaambiwa hii Wizara ni Wizara ya Huduma siyo *(productive)* haizalishi, ndiyo jibu tulilopewa. Mimi nafikiri jibu kama hilo halistahili kutolewa na Kiongozi wa Serikali. *(Makofi)*

Hakuna mtu ambaye haguswi na sheria katika nchi yoyote. Maisha ya raia katika nchi yanatawaliwa na Katiba, sheria mama. Mikataba yote ni sheria, uhusiano wa raia na dola ni sheria, uhusiano wa raia na raia ni sheria. Mahusiano kati ya dola yetu na dola nyingine ni sheria, shughuli zote za uchumi, huduma za jamii, mali na kadhalika, uhai wetu, hata kuabudu kwetu kuna sheria ndani. Hata Mussa alishushiwa Kitabu cha Taurati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, siyo kweli kwamba, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ni *service ministry only.* Pasipokuwa na sheria na zikasimamiwa vizuri, hakuna amani. Kinyume cha sheria ni *anarchy* na kukiwa na *anarchy* hakuna uzalishaji. Hata mwenzangu Mheshimiwa Mudhihir, atashindwa ku-*organize* michezo ambayo pia kuna sheria. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba hii dhana ya kuwa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, inashughulika na huduma kwa hiyo siyo *productive,* iondolewa na wapewe hadhi ambayo wanastahili kuwa nayo na wepewe *ceiling* ambayo ni ya juu ili waweze kutupangia mipango mizuri zaidi.

Katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wajibu wao mkubwa wa kutoa ushauri juu ya Sheria, wajibu wao mkubwa wa kutoa ushauri juu ya Mikataba ambayo tumeingia na nchi nyingine na Mashirika mengine, hauwezi kufanyika katika mazingira ya shida shida. Ofisi ya Tume za Haki za Binadamu tunawapa kutetea haki za binadamu katika mazingira magumu. Tume ya Kurekebisha Sheria, utafiti wanaofanya, wanaufanya katika mazingira magumu, hawawezi katika hali hii kutupendekezea marekebisho mazuri, tunapiga kelele juu ya marekebisho ya sheria za urithi, sheria za watoto na kadhalika.

Lakini *resources* za utafiti hazipo. Kabidhi Wasii Mkuu, anahusika na ndoa, anahusika na vifo, anahusika na vizazi, tusipojua wamekufa wangapi na wamezaliwa wangapi, hatuwezi kupanga maendeleo. Lakini tulishangaa tulipotembelea hata jengo lao tukakuta rekodi za vizazi na vifo zimewekwa kwenye makabati ya ajabu ajabu. Lile jengo pakitokea cheche za moto, rekodi za Taifa zima zitapotea. Lakini tunaona sehemu nyingine zinazoitwa sehemu ambazo ni *productive* zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mahakama Kuu na Mahakama zote nyingine zinajitahidi kuzuia watu kuji-*engage* kwenye *self help*, maana ukiondoa hukumu za mahakama, watu tutachukua mikuki na mishale kama zamani na kuumizana. Sasa katika jitihada za ku-*maintain* amani katika nchi hii, wako pia katika mazingira magumu. *Rate* ya watumishi wa Mahakama kupata *stroke* imekuwa kubwa sana siku za karibuni. Sababu ni kazi wanazofanya. Jaji anakaa anaandika tangu asubuhi mpaka akitoka kazini anaandika hata vitu ambavyo hatakiwi kuandika. Wenzake huko nje wanasikiliza wakati inakuwa *recorded* na baaadaye anakuja kutoa hukumu. Hawa wa kwetu ni *stenographers*, ni Majaji, kila mtu anafanya kazi zote. Vitendea kazi vyao ni vya shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ni Wizara nyeti sana, haistahili kudharauliwa kwa jinsi ambavyo inadharauliwa sasa. Kuna malalamiko ambayo yanatolewa juu ya ucheleweshaji wa kesi, lakini ukichukua mazingira ya mahakama na mazingira ya sheria zetu, inabidi kesi zichelewe. Wanasema haki ikicheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa, lakini haki inayoharakishwa pia inaweza ikawa haki iliyopotoshwa. Lakini ziko sheria kweli ambazo zinasaidia katika kuchelewesha hii haki. Kwa mfano, *Criminal Procedure Act,* inaweza ikatafsiriwa vibaya na inatafsiriwa vibaya sana kwamba polisi wanafikiriwa na madaraka ya kukamata kabla ya kuchunguza halafu waendelee kuchunguza. Mimi nafikiri hili zaidi siyo ubaya wa sheria lakini ni ufahamu na elimu kwa wale ambao wana uhusiano na utekelezaji wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala dogo la ajira. Tulipokuwa tunatembelea Idara ya Mahakama, Mheshimiwa Jaji Mkuu, aliieleza Kamati kwamba, mkakati uliopo sasa ni kwamba Chuo cha Lushoto kiweze kutoa watumishi wa ngazi za kati wa Mahakama. Hilo ni jambo zuri sana na alitoa mfano kwamba hata Mapadri wanasomeshwa kwenye semina katika maadili ya Kipadri Padri, lakini kuna uwezekano kwamba, pamoja na Mapadri kusoma kwenye semina hizo kuna Mapadri wengine ambao wanajitokeza wanakuwa na tabia mbaya.

Tunachosema ni kwamba, kule ku-*train* watu kwenye Chuo cha Lushoto tu hakutoshelezi kuwa na kada ya katikati ya watumishi wazuri. Mimi nafikiri kwamba, uamuzi huo unakatisha tamaa *contribution* ya vyuo vingine vinavyosaidia ku-*train* katika nyanja za sheria. *(Makofi)*

Viko vyuo kwa mfano Chuo Kikuu cha Mzumbe, ambacho kinatoa diploma ya sheria, kuna Chuo Kikuu Huria nacho kinatoa diploma ya sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatoa *certificate* ya sheria, swali ikiwa *consumers* wa hawa watu ambao wamekuwa *trained* kwenye sheria, ni Wizara ya Sheria tu, *mostly* hivi vyuo vingine vinaambiwa vifunge hiyo *discipline? (Makofi)*

Mimi nilikuwa nafikiria kwamba, kuna njia ya ku-*monitor* hawa watu wanaokuwa *trained* kwenye vyuo vingine waweze kuwa *absorbed* kwenye Mahakama na kwenye Wizara ya Sheria. Sikutegemea niseme kwa muda wote, lakini naomba nivumiliwe kwa sababu ni *interested party* kwenye hii Wizara. *(Makofi)*

Mahakimu wetu na hata Majaji wetu wanaishi katika mazingira magumu. Hivyo kwa mfano juzi huu Mradi wa Viwanja 20,000 Dar es Salaam, kuna kitu gani ambacho kimezuia pasitengwe *estate* ya Watumishi wa Mahakama, kuhakikisha kwamba wanapewa mikopo wajenge nyumba zao pale na wanaishi kwa njia ambayo wanaweza wakalindwa zaidi kuliko kuwa- *expose* katika sehemu hatari, huku wanakatalia watu dhamana, huku wanafunga watu vipindi virefu ambavyo tunavitungia sheria sisi hapa? Hali yao ya maisha ni ngumu sana. Tumewaongezea mamlaka ya kuamua kesi lakini hatukuwaongezea marupurupu yoyote. Wanaishi maisha yale yale ambayo walikuwa wanaishi. Kuna hatari ya kuwapigia kelele kwamba wanapokea rushwa kumbe hawapokei rushwa lakini wana *disillusionment.* Wanafanya kazi shingo upande kwa sababu hawaoni faida ya ile kazi. Kuwa Hakimu siyo kuwa Mtume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninaomba nimalizie kwa kusema niko *concerned* kwamba, kuna kesi nyingi sana dhidi ya Serikali katika Mahakama zetu. Serikali inatakiwa iwe inatawala,

haitakiwi iwe inagombana. Naomba uchunguzi ufanywe pamoja na nia nzuri ya *Government Proceedings Act* ya kuruhusu wananchi waishtaki Serikali, kwa nini Serikali ijiingize kwenye ugomvi na wananchi ili wananchi wawe wanaishtaki kila wakati? Wale ma-*State Attorney* wakae washauri Serikali juu ya uendeshaji bora wa Serikali siyo wakae wangojee kuja Mahakamani kama Mawakili binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, niliyosema naomba nirudie kusema kwamba, naiunga mkono hii hoja. Nampa pole Waziri, pamoja na timu yake na naomba waendelee kutusaidia kuboresha hii Wizara. Pia nampongeza Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ijapokuwa hakuombwa ampigie mtu yeyote debe katika Bunge hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba. Kwanza, nampongeza kwa hotuba yake nzuri, ambayo baada ya kufuata kidogo maelekezo au maboresho ambayo hotuba ya Kiongozi wetu wa Upinzani imemwelekeza, nadhani atakuwa na dira nzuri ya kumsaidia katika kazi yake hii ngumu ya kututafutia haki Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili napenda kuelekeza mchango wangu wa kwanza kwa jinsi haki za binadamu zinavyovunjwa katika magereza na Mahakama zetu. Nina mfano mmoja wa watu ambao ni watuhumiwa. Kabla ya kukamatwa kwamba wao ni watuhumiwa wa kesi au shutuma fulani, wanapopelekwa magerezeni au katika mahabusu ili kuhifadhiwa kwa ajili ya kutafuta ushahidi au upelelezi wa polisi, watu hawa huchukuliwa kama wafungwa na hawapewi nafasi nzuri ya kufanya shughuli kama wao wako nje na wao bado hawajakumbwa na sheria au kosa lile.

Kwa hiyo, namwomba sana Waziri, watu hawa wachukuliwe kama ni watuhumiwa na wapewe nafasi ya kufanya shughuli zote ambazo walikuwa wakizifanya walipokuwa huru nje mpaka itakapothibitika kwamba, kosa walilolifanya ni la kweli na Mahakama itachukua mkondo wake hapo ndiyo itabidi wao wapewe adhabu kama inavyostahili. Lakini vinginevyo ni kuwavunjia haki za binadamu. Waweze kupewa magazeti, kutazama *television*, kuvuta sigara na kama ni wanywa pombe vile vile waruhusiwe kwa sababu wao mkondo wa sheria haujawachukua. Nayasema hayo kwa ushahidi wa kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba, ningependa Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa vijana wetu hawa wa polisi kwamba watuhumiwa hata kama watawakuta na kosa, walinzi wasijaribu kutumia nguvu za ziada wakati mtu yule ambaye wanaye chini ya ulinzi hajafanya tatizo lolote labda kukataa amri zao au kutumia nguvu ya aina yoyote. Mimi binafsi niliwahi kumwona kijana mmoja ambaye alipelekwa polisi, alikamatwa na chupa mbili za gongo, askari akamchukua hadi Kituo cha Polisi, alipofika naye pale akaulizwa huyu ana kosa gani?

Akasema tumemkamata na chupa mbili za gongo. Askari mmoja ambaye ni Mkuu wake alimwambia hebu mpe chai kwanza huyu. Askari aliyefuatana na yule kijana alimpiga kibao kimoja kikubwa sana na akaanguka chini. Yule kijana mlevi akamwuliza Kamanda wa Polisi, hivi Mheshimiwa naomba umwulize huyu kijana wako tokea aliponikamata mpaka hapa tulipo nimefanya kitu gani ambacho hakikuwa chini ya amri yake? Kijana alijibu hapana hajafanya kosa lolote. Je, hivi mimi kupigwa kibao kama hiki ni haki yangu? Alimwambia hapana haki hapa! Lakini kweli kafanya vibaya, mara ya pili usirudie. Baada ya kijana kuambiwa vile alichokifanya ni kwamba alimnyemelea askari na yeye akampiga kibao kimoja kikubwa. Alipoulizwa kwa nini umefanya hivi? Alijibu yeye alinipa chai na mimi nikawajibika nimpe mkate. Sasa kukawa na mabishano pale askari walikuwa wengi maskini wakampiga vibaya sana kwamba kwa nini hakutulia alipopewa chai? Kwa nini alirudisha mkate? *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, ujitahidi kushirikiana na Waziri wa Mambo ya Ndani, ili Maaskari wetu hawa watumie nguvu pale mahali ambapo panastahili na mahali ambapo hapastahili, basi wasitumie nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Waziri, alipokuwa akijibu swali Bungeni hapa la Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, kuhusu nafasi hizi za asilimia 30 za Wabunge wa Viti Maalum kuingia katika Bunge letu, mimi nadhani labda Waziri alilijibu kwa masihara kwa sababu yeye ni mtu ambaye ni

mcheshi ni wa masihara, lakini jawabu lake alijibu kwamba, sababu yake kubwa ni kwamba Bunge letu, nyumba yetu hii ni ndogo, haitoshi kuwaingiza na kuikamilisha ile asilimia 30. Mimi binafsi, kwa mapenzi makubwa ya ndugu zetu hawa wanawake, ambao kwa kweli wamejitahidi, tumekuwa pamoja nao tokea tupiganie uhuru mpaka leo na ikawa wakitaka kujinyanyua tunawakandamiza hawapati nafasi. Kwa hiyo, napendekeza na namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, kama ni sababu ya ufinyu wa nafasi, mimi binafsi pamoja na wenzangu, tutakuwa tayari tuwekewe benchi kule nyuma tukakae ili wenzetu hawa asilimia hii 30 itimie na waingie humu tushirikiane kwa sababu hawa tumeanza nao zamani. *(Makofi)*

Jana nilikuwa nikipitia gazeti hili hapa la Tanganyika. Gazeti hili lilitolewa Desemba 17, 1960. Kuna ushahidi hapa wa kwamba hawa wenzetu tumeshirikiana nao kikamilifu katika kuikomboa nchi hii. Kuna mama jina lake Bi Lucy Lameck, ni Mjumbe wa *LEGICO* Tanganyika na Katibu wa *TANU* ahusikaye na mambo ya wanawake, aliliambia Taifa katika hili gazeti kwamba, mapema mwezi ujao ataanza safari ya kwenda Tanganyika nzima kuwatembelea na kuwakagua wanawake wengi kama vile atakavyoweza. Sitamaliza yote aliyozungumza, lakini katika gazeti hili la tarehe 17 Desemba, 1960, aliyoyaeleza hapa ni kwamba, lazima mtu aheshimu. Tumeshirikiana kikamilifu katika kuikomboa hii nchi. Sasa kwa nini wasipatiwe nafasi hizi? Kwa kweli mahali popote ambapo ndugu zetu hawa watakabidhiwa nafasi, basi ikiwa kuna mwanya wa rushwa, huondoka. Hawa ni watu wanaofanya kazi bila ya kukubali kupokea rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku moja niliingia kwenye gari moja, daladala, nikawakuta makondakta wanahadithiana pale. Mmoja anasema kwamba mimi nimekamatwa bwana. Nimepigwa mbungo leo. Anaulizwa imekuwaje? Anasema, nimekamatwa na Askari. Askari huyo nani huyo? Akasema Askari mwanamke. Akaambiwa umekwisha! Kwa sababu Askari mwanamke huwezi kumwendea na chochote. Alichonacho yeye ni Mahakamani tu. Kama angekuwa Askari yeyote mwanaume, basi nakuhakikishia kwamba, tungekwenda na hiyo kesi isingekwenda Mahakamani. Hii ni alama ya ukweli ya wenzetu hawa. Kwa hiyo, kwa nini wasiingie katika Bunge letu? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumzia kuhusu suala la Utawala Bora. Ili tufikie katika demokrasia ya kweli, napendekeza Tume ya Uchaguzi iwe moja katika mihimili minne ya dola ili tukamilishe hasa demokrasia ya kweli na Tume hiyo ya Uchaguzi iwe huru. Tume hiyo ya Uchaguzi isimamie chaguzi zote za kiserikali kuanzia Taifa hadi ngazi za chini na Vitongoji. Kusiwe na Wizara au Idara yoyote yenye Mamlaka ya kusimamia masuala ya uchaguzi. Hapa ndio kweli tutakuwa tuko tayari kuingia katika demokrasia ya kweli. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, amwombe Mheshimiwa Rais, aunde hii Tume ya Uchaguzi angalau ifanane na ile ya Zanzibar, iwe na Wajumbe kutoka kila Chama. Hii nairudia tena, iwe na Wajumbe kutoka kila Chama na kwa sababu hapa labda Vyama ni vingi, angalau hivi vilivyoleta uwakilishi katika Bunge, wakae pamoja, hiyo ndiyo iwe Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Lakini ikisemekana kwamba Rais achague Tume ya Uchaguzi yake mwenyewe, Tume ya Uchaguzi itawajibika kwa yule aliyeichagua. Hawataweza kufanya haki. Rais akiona uchaguzi unakwenda vibaya, atasema, naomba masanduku ya kura yacheleweshwe kupelekwa. Hapa badilisha asilimia hii iwe hii, fanya hivi. Lazima wale watawajibika kwa yule ambaye amewachagua. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, umwombe Mheshimiwa Rais, atuchagulie Tume ya Uchaguzi iliyo huru na ya haki.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kwamba, kama Tume hii ya Uchaguzi haitakuwepo na kama daftari hili la uchaguzi litachelewa na halitatumika katika uchaguzi ujao, nashindwa kutabiri kwamba uchaguzi huu utakuwepo au la.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie machache katika Wizara hii. Kwanza, natangulia kusema kwamba, naunga mkono hotuba ya Waziri na ningependa kumpongeza Waziri, pamoja na timu yake, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Lakini nisisahau kumpongeza ndugu yangu aliyekaa sasa hivi, kwa kuweka kumbukumu ya gazeti la mwaka 1960 mpaka leo na kukumbuka kwamba kuna mama mmoja Mwana-*TANU*, wakati huo alifanya mambo mazuri. Lakini ningemwomba akumbuke mambo mengi sana yaliyofanywa na *TANU* na

*ASP* kwamba, wamefanya mambo mengi, kama ana magazeti mengine ya *TANU* sio mbaya akienda kurejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ningependa nizungumzie suala la ucheleweshaji wa kesi. Jambo hili kwa kweli limekuwa kero kwa wananchi kwa sababu kuna ambo mengine ya wazi ambayo yanacheleweshwa mpaka wananchi wanashindwa kujua nini kinachoendelea. Nikitoa mfano, siku moja majambazi walivamia nyumba Longido, wakachukua shilingi laki nane. Hao majambazi walikwenda Kijiji kingine wakakamatwa na baada ya kundoka mwenye nyumba alikwenda kutoa taarifa kwamba, majambazi walimvamia wakachukua shilingi laki nane na aliandika *statement* yake. Siku hiyo hiyo usiku majambazi hao wakakamatwa wakapelekwa polisi na zile fedha. Ilikuwa mwaka 2002.

Sasa mwenye pesa hajapewa hizo pesa ziko Mahakamani mpaka leo, eti upelelezi unaendelea. Mwaka 2002 mpaka leo? Kabla ya majambazi kukamatwa amekwishatoa taarifa Polisi. Hivi mtu yeyote akisikia kwamba hizo fedha hazijapatikana mpaka leo ziko Mahakamani kwa ajili ya upelelezi, hivi kweli ataona kwamba ni haki? Ningependa kusema kwamba, jamani haki ikinyimwa kwa mtu yeyote, kwa kweli anaona kwamba ni dhuluma kubwa sana na wananchi walioko Vijijini, wanapata dhuluma kubwa sana. Kwanza kukosa Mahakama ya kukimbilia, hiyo ni dhuluma mojawapo kubwa sana. *(Makofi)*

Katika Jimbo langu tuna Mahakama ya Mwanzo. Hiyo Mahakama ilijengwa na Wajerumani, sio Waingereza. Ni chumba kidogo sana, hakijawahi kukarabatiwa kuanzia wakati ule mpaka leo. Mwananchi aliyeko mwisho wa Jimbo langu, Kamwanga kuja Mahakama ya Longido ni Kilometa 170. Aliyeko Natron kuja Mahakama ya Longido ni Kilometa 150. Kwanza aje kutoka kule mpaka Mahakama, apigwe tarehe, bado uchunguzi, wananachi wakakimbia Mahakama kabisa wakaenda kufanya Mahakama ya kimila ndio inatumika kule. Hizi sheria wao wameziacha kwa ajili ya ugumu wa kufuata haki. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba, kila Tarafa wawe na Mahakama ya Mwanzo ili wananchi wapate huduma hii. Ni huduma! Wapate huduma hii kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mahakama, wakiambiwa wananchi wachangie ni tofauti na kuchangia Shule, madarasa, kuchangia nyumba za Walimu, kuchangia Zahanati, ni tofauti kabisa. Wanaona kwamba sio kazi yao. Katika maeno mengine ambayo wamezoea hizo Mahakama za kimila kutatua matatizo yao, wenyewe wanasema afadhali tutatue matatizo yetu wenyewe kuliko kujenga Mahakama. Kwa hiyo, ningependa Serikali isaidie sana pamoja na wanasiasa, sisi nasi tusaidie sana kuhamasisha wananchi, wachangie hii huduma ipatikane.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia, kuna sheria nyingine kama mwenzangu aliyetangulia alivyosema kwamba, zimepitwa na wakati. Kuna sheria moja ya mimba, yaani wanafunzi wa Shule kupata mimba. Mimi napata uchungu sana kwa adhabu ya mimba. Mtoto wa Shule anapewa mimba, kesi ikienda Mahakamani mhusika anapigwa faini Sh.10,000/=. Hivi Sh.10,000/= na huyo mtoto ambaye wamemharibia maisha yake, amekosa elimu, hivi kweli Sh.10,000/= ni adhabu ya kumpa mhalifu kama huyo? Kwa sababu huyo mtu mimi namhesabu ni kama mbakaji. Ni mbakaji kabisa! Kama mbakaji anafungwa miaka 30, kwa nini huyu apigwe faini Sh.10,000/=? Hiyo Sheria irekebishwe kabisa, kwa sababu kwetu watu ambao bado tunasoma kwa lazima, bado hatutaki elimu, huo uharibifu unatumika sana ili watoto watoke mashuleni. Unatoza faini Sh.10,000/=! Katika maeneo hayo, bado mtu anauza dume lake la ng'ombe la Sh.200,000/= ampe mtoto atoke Shuleni, sasa atashindwa kutoa Sh.10,000/=? Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba hiyo sheria iangaliwe sana kwa sababu inatuumiza na inaturudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni rushwa. Rushwa Mahakamani inatokea kwa sababu nyingi sana. Kwanza nikichukulia Mahakimu walioko kule, ni watu wanaopata shida sana. Kwanza hata ukiangalia usafiri wa Hakimu wa Wilaya, kwanza yeye mwenyewe hana gari, akitaka kutembelea Mahakama za Mwanzo, mpaka aingie kwenye basi, aende huko. Ni shida, ni matatizo makubwa sana. Yaani mimi naona Serikali imeacha chombo hiki kana kwamba ni chombo kinachojiendesha na wanafahamu kwamba hakina mapato. Yaani kimeachwa, ndio maana hakuna fedha za kukarabati majengo, hakuna fedha za ujenzi, hata katika kitabu chao mnaona fedha walizopangiwa na mwaka huu ndio tunasema kwamba ni afadhali. Mimi sijui Serikali inaangaliaje Mahakama. Kwa kweli

ukinyimwa chakula au usipopata mahitaji, lazima utakwenda kuiba na lazima hao nao watadai rushwa ili waweze kuishi. Kwa hiyo, nasema kwamba hebu jamani tuwawezeshe tuwape mshahara mzuri, tuwape marupurupu mengine wanayopata Maafisa wengine. *(Makofi)*

Kuna mwenzangu aliyesema kwamba hata semina hawapati, ni kweli na mnajua wengine siku hizi wanafanya semina kama ajira wapate mapato, kuna wengine wanaopata mapato kwa ajili semina na safari kuliko mshahara. Ningependa kusema kwamba na hawa watu wa Mahakama nao wasaidiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la vitendea kazi. Siku moja Jaji alikuja kutembelea Mahakama ya Mwanzo pale kwetu. Alinikuta, lakini Hakimu alipompeleka kule Mahakamani, aliniambia hebu tuelekee huko, mimi nikakataa. Kilichonisababisha nisiende ni aibu. Kwa sababu nafahamu Mahakama ilivyo, hakuna hata kabati. Ni kale kachumba kalikojengwa mwaka 1905. Hakuna waliozaliwa wakati huo hapa. Hakuna mafaili. Kwanza nilishukuru kwa sababu amekuja ili aende kuona, lakini sitaki na mimi kwenda kuona aibu hiyo nikamsubiri, nikamwambia nendeni kwanza mtanikuta. Hayo ningependa kusema kwamba, kwa kweli hebu tujali tena maeneo ya Mahakama. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kwamba, hii haki inayokosekana ndio maana watu wanajinyonga, ndio maana watu wanauana na ndio maana watu wanachukua sheria mikononi. Kwa sababu ukinyimwa haki... Hakuna kitu kibaya kama kupakaziwa kosa ambalo linatendeka sana Vijijini. Unapakaziwa na tena kwa sababu hujui kinachozungumzwa. Watu wengi hawajui Kiswahili. Kwa mfano, Mwanasheria anajua kuna mtu aliyefungwa Gereza la Dodoma hapa. Amefungwa miaka 40.

Mtu huyu alikamatwa wakati hakuna mtu anayejua Kimasai, akaambiwa ameiba. Hakuna mkalimani na amefungwa miaka 40 yuko hapo. Mwanasheria tumemweleza, mpaka leo. Wakati mmoja tulikwenda kumwona, alivyotueleza mazingira ya kukamatwa mpaka akafungwa, tulisikitika sana. Anatumikia kifungo cha miaka 40 sijui atamaliza lini au atafia kule, lakini hakuna mkalimani anayemwambia kwamba umeambiwa hivi, umetenda hiki na hiki na hiki au anayeeleza yeye anachoeleza. Atafungwa tu! Walifungwa wakiwa wawili anasema sijui mwenzangu kapelekwa wapi mpaka leo. Kwa sababu na wazazi wake hawajui sheria wala pa kwenda, nao wakanyamaza mpaka leo.

Kwanza ni Mheshimiwa Timan, ndiye alikwenda kuulizia ndio akasikia kwamba yuko hapa ndio akaenda kuwaambia wazazi wake kwa sababu ni mtu wa Jimbo lake. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba, hata panya, ukimfukuza akakosa pa kupita, atakurudia pamoja na udogo wake, atakurudia kwa sababu amekosa pa kukimbilia. Sasa watu wanaanza kukosa pa kukimbilia Mahakamani, watafanya fujo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndio tumefikia mwisho wa wasemaji waliopangwa kwa kipindi cha asubuhi. Waliopangwa kipindi cha mchana ni Kama ifuatavyo: Mheshimiwa Zamda Bozzen, Mheshimiwa Ali Said Salim na Mheshimiwa Said Nkumba. Baada ya wazungumzaji hao watatu, watoa hoja watahitimisha hoja yao tukianza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. ZAMDA S. BOZZEN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii adimu kwa mara yangu ya kwanza ili na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu. Awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa kuweza kuwatangazia wananchi kurejea kwangu Bungeni kwa mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kazi zake nzuri, zenye kujaa hekima na ufanisi ambao umetuwezesha kuishi kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuwapongeza Waheshimiwa Majaji wote walioshiriki kuweza kuitoa haki kwa misingi ya Sheria ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano bila kujali jinsia wala itikadi yoyote. Kwa kweli nawapongeza sana, kitendo walichokifanya wametumia Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kwa huzuni kubwa, kuchukua nafasi ya kutoa pole kwa familia za Marehemu Majaji wote kwa ujumla waliopoteza uhai wao, Mwenyezi Mungu, awaweke mahali pema Peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile bila kuwasahau Mawakili wetu waliotusimamia kututetea katika kesi hii ngumu iliyokuwa imetuvunjia heshima ya kutuvua Ubunge bila kumsahau Mheshimiwa Marando na mwenzie Wakili Mnyele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, napenda kuanza kuchangia. Napenda kuchangia upande wa Sheria. Kinachonishangaza na kunisikitisha ni upande wa Sheria hizi ni sheria gani au ni kifungu gani kinachompa mamlaka kiongozi wa Chama cha kisiasa kumfukuza Mbunge, kumvua uanachama na kumfukuza Ubunge Bungeni, halafu kumvua uanachama na kumkosesha haki za Ubunge na kama hiyo sheria ipo, mimi binafsi kama Zamda, nitawasilisha hoja binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ikiwa umechaguliwa na wananchi, wewe ni mwakilishi wa wananchi. Wewe siyo mwakilishi wa chama. Wewe umechaguliwa na wananchi, aidha kama ni kuteuliwa, umeteuliwa na wananchi ukawawakilishe. Unapokuwa umefukuzwa kwenye uanachama na ukanyimwa haki za Bunge ina maana moja kwa moja ni kuwanyang'anya haki wawakilishi wako ambao ni wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa kama hii sheria ipo na kama haitafanyiwa marekebisho, itakuwa ni mchezo wa lelemama. Kila siku watakuwa watu wakikaa wakilala, wakiamka, hata saa sita za usiku wanakaa tu Bunge kesho nimfukuze Mheshimiwa Asha, keshokutwa nimfukuze Mheshimiwa Mwananzila, labda keshokutwa nimfukuze Mheshimiwa Marwa, kwa sababu tu nina chuki naye binafsi na kwa sababu tu niliyekuwa nikimtaka mimi hakuteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba kwa niaba yangu na kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wangeweza kuomba hii Sheria ya kumpa mamlaka kiongozi yeyote wa chama cha kisiasa ibadilishwe. Kwa sababu, ukiangalia hii Sheria imekuwa sasa kama ndio mwenendo na mwelekeo wa kuwa kama mtu akikosana na mtu kwa sababu zao binafsi, anaamua mtu kutoa amri ya kufukuzwa. Hapo hatutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nilikuwa naomba kama kuna uwezekano wa kupitisha Sheria iwapo kama Mbunge atanyimwa haki za Ubunge akafukuzwa na akaweza ku-*appeal* Mahakamani na Mahakama ikamrejeshea uanachama wake na Ubunge wake, kwa kweli nilikuwa naomba Sheria itolewe kwamba viongozi wahusika wenyewe walipe zile gharama za kesi pamoja na mishahara yote ya nyuma iliyolimbikizwa wakati ukiwa nje ya Bunge kwa kipindi chote. Kwa kufanya hivyo, Mwenyekiti nina maana ya kwamba, watakoma kabisa tabia za kufanya mchezo wa kazi kwenye Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nina lingine ambalo linanikera sana rohoni kwangu. Hivi ni kifungu gani kwa kuwa mimi sijasoma Sheria, samahani. Ila naomba tu niseme kama nitakosea, nitakosolewa baadaye. Kuna kifungu gani ambacho kinawapa mamlaka viongozi wa vyama vya siasa, wanapokuwa kwenye mikutano yao ya hadhara na kuanza kuadhiriana kwa njia ya kutumia lugha ya matusi kumtukana kiongozi wa chama kingine chochote kile, chama chochote ni sheria ya kifungu gani? Kama Sheria hiyo ipo lakini sidhani kama kuna sheria hiyo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba wanapopanda juu ya majukwaa hushindwa kusema hoja zao huanza kutukana viongozi wenzao. Ni jambo la aibu na linatia fedheha katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema hivyo nina uhakika na nina ushahidi nilisikia kabisa mtu kapanda juu ya jukwaa kwa kuwa tu yeye amenyimwa nafasi ya Ubunge kwa sababu hakuchaguliwa kwamba alionekana hafai. Anaamua kumtukana Mbunge mwenzie kwa sababu kapita. Hiyo siyo Sheria na kama ni sheria ipo tutaiomba vile vile ibadilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulisema, ni kuhusu masuala ya Sheria ya kunyanyaswa sisi wanawake. Sheria ya kunyanyaswa sisi wanawake inaonekana wazi kwa sababu hamuwezi mkawa mmetenda kosa moja wakaadhibiwa wanawake peke yao. Hii ni kutunyanyasa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi nimekaa nje ya Bunge kwa mwaka mmoja na miezi sita bila sababu yoyote. Haki zipo za msingi, lakini ni kwa sababu tu mtu ameamua kwa mapenzi yake simtaki Bozzen, namtaka fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili vile vile naomba walione. La mwisho ni kwamba, mimi nilikuwa sina mengi sana ya kuchangia. Nilikuwa napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wamenipa ushirikiano wakati wa kipindi changu kigumu cha kesi katika mwaka mmoja na miezi sita. *(Makofi)*

Nasema kwa lugha kwamba sina cha kuwalipa, isipokuwa Mwenyezi Mungu ndiye atakaye walipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema kwamba, nampongeza Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Mwapachu, kwa kazi yake nzuri na Watendaji wote wa Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nasema naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nitakuwa na machache ya kuchangia. Kwanza kabisa, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Wataalam wake. Nimesoma kitabu cha hotuba kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wataalam wake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi vile vile kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi ambavyo amekuwa kivutio kikubwa cha namna ya kujibu maswali kwa Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tunaridhishwa sana na kujibu kwake maswali kwa unyenyekevu mkubwa sana kwa Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze la kwanza, sote tunafahamu kwamba, Mahakama ndicho chombo pekee ambacho kisheria kinatoa haki kwa raia. Sasa mimi bado naona mapungufu katika suala zima la Utawala Bora, kama Mahakama bado zinakuwa mbali sana na wananchi kwa kweli tunawanyima haki yao ya kisheria katika misingi ya haki wananchi ambao kwa kweli wanashindwa kuzifikia Mahakama zilizo mbali sana, wengi wahalifu wanaweza aidha kufungua kesi kwenye Mahakama za mbali ili wananchi waweze kushindwa aidha kupeleka ushahidi wao au wao wenyewe kufika. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana mtandao wa Mahakama hasa za Mwanzo, uende mpaka karibu na wananchi kwa ajili ya misingi kwa raia wote.

La pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nizungumze tu kwamba, ni wananchi wachache sana wanaofahamu kwamba Mahakama ni chombo pekee kinachojitegemea, kwa maana ya kwamba mihimili hii mitatu ya Mahakama, Bunge na Serikali, haitambuliki sana kwa wananchi. Kwa hiyo, chochote kinachofanyika kama kikifanywa na Serikali, kama kikifanywa na Bunge, vyote kwa wananchi wa kawaida kule vijijini vinaonekana ni vitu vya Serikali. Kwa hiyo, hapa nilikuwa nataka niseme kwanza napongeza sana kazi nzuri zinazofanywa na Majaji na kazi nzuri zinazofanywa na Mahakimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nilieleweshe Bunge kwamba, wapo baadhi ya Mahakimu wachache wanaweza wakachafua kazi nzuri inayofanywa na Mahakama zetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mfano nimekwisha wasiliana na Mheshimiwa Waziri, lakini nataka nitoe mfano wa baadhi ya dosari ambazo baadhi ya Mahakimu wanataka kupaka matope kazi nzuri inayofanywa na Mahakama za aina zote, Mahakama ya Rufaa, Mahakama Kuu na Mahakama za Mwanzo na za Mikoa. Nataka nitoe kama mfano, tarehe 20 Machi, 2002 nilifanya mkutano wa hadhara Sikonge Mjini. Mkutano huo ulikusanya wananchi wengi na baadhi ya Viongozi wa Serikali. Katika mkutano huu nilizungumza mambo mengi lakini nilipomaliza mkutano Mwenyekiti wa kile kikao, ambaye ni Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, alisimama, kulikuwa na mgogoro kwa siku za nyuma kati ya Kijiji kama Serikali na mwananchi mmoja ambaye aling'ang'ania kukaa kwenye nyumba ya Kijiji kwa kutumia Mahakama. Mwisho baadaye Mahakama ikatoa uamuzi na yule mwananchi akaondoka.

Kwa hiyo, chuki ile akaendelea nayo dhidi ya Viongozi wa Serikali, akashtaki baada ya ule mkutano kwamba, kupitia kwenye Mkutano wa Mheshimiwa Mbunge, Mwenyekiti pamoja na baadhi ya Viongozi, baada ya mkutano huo walichukua *microphone* ya Mheshimiwa Mbunge, wakanitukana mbele ya hadhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hili kwa masikitiko makubwa sana. Nimpongeze kwanza Hakimu wa kwanza pamoja na kwamba alikuwa ni Hakimu mwanamke, alihukumu kesi ile kwa kutupilia mbali kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, Hakimu ni Hakimu. Unaweza kufuta maneno yako? *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta hii. Nia yangu ilikuwa kumsifia huyu mama, kwa kazi nzuri aliyoifanya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, alihukumu kesi ile kwa kufutilia mbali shitaka lile. Baadaye yule mwananchi kwa sababu anapenda sana kesi, akaenda kwenye Mahakama ya Rufaa ya Wilaya, akakata rufaa akaenda kwenye Mahakama ya Wilaya, kwenye Mahakama ya Wilaya Mheshimiwa Hakimu mwingine mwanaume kama mimi, akawahukumu wale viongozi kifungo cha miezi mitano jela, bila kujali ushahidi uliokuwepo, kwa sababu mazingira yaliyokuwepo ya ushahidi yalikuwa mapana sana. Lakini alimchukua mama wa mlalamikaji, mtoto wa mlalamikaji na mume wa mlalamikaji kwamba hawa ndiyo mashahidi wa kutosha. Akaacha mazingira mengine yote yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasikitika sana kwamba vitendo vya namna hii kwa wananchi vinawapa picha mbaya sana dhidi ya Serikali kama nilivyosema, kwamba wananchi hawatambui kama Mahakama ni chombo kinachojitegemea. Kwa hiyo, lawama zote zinakwenda kwenye Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mfano nautoa na nikimaliza hapa nitamkabidhi Mheshimiwa Waziri, nimekwishapata viambatanisho vyote vya hukumu, nitamkabidhi kwa kweli kwa ufuatiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho lakini siyo kwa umuhimu, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Bozzen, kwa mchango wake mzuri alioutoa jioni hii. Lakini nataka kusema tu kwamba, sheria hii ni sheria mzuri kwamba, mwanachama yoyote lazima aheshimu chama chake. Sasa inategemea haya aliyoyasema Mheshimiwa Bozzen, inategemea unajiunga na chama gani. *(Makofi)*

Sisi tunamaliza miaka mitano hatujasikia Mheshimiwa Mbunge, amefukuzwa. Sasa natoa wito kwamba, unapokuwa wewe umefika mahali ni mwanasiasa, unahitaji chama cha kukitumikia kwa utaratibu, wewe ukitumikie chama na uwatumikie wananchi, ajiunge na chama ambacho hakina mizengwe lakini vile vile hakina uongozi wa mfukoni kwamba uko mikononi mwa mtu mmoja. Kwa hiyo na vyama hivi vinajulikana vipo. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa nataka niseme leo asubuhi kuna mchango wa Mheshimiwa Mbunge mmoja wa *CUF*, alisema kwamba, wanaweza wakawapisha baadhi ya Waheshimiwa Wabunge Wanawake, katika azma ya kufikia asilimia 30. Mimi nasema haya maneno hayatoki rohoni kwa Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha *CUF*. *(Makofi)*

Kwa sababu kama kweli wangekuwa wanawathamini wanawake, wasingewafukuza wanawake wanne ambao walikuwa wanawawakilisha wanawake wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utaratibu wa baadhi ya vyama sasa hivi kurukia Sera sahihi za Chama cha Mapinduzi. Sera za kuwathamini wanawake zimeainishwa vizuri sana katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000 na Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nataka nitoe wito kupitia kwenye Bunge hili Tukufu, kwa wanawake wote nchini kwamba, Chama ambacho kwa kweli kinawathamini wanawake kwa asilimia kubwa ni Chama Cha Mapinduzi peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, wengine wananiambia hapa kwamba ni mazito. Basi nachukua nafasi hii kwa kweli kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kumtakia kheri na fanaka Mheshimiwa Waziri katika kazi zake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuweza kufanya shughuli zetu za Bunge jioni hii tukiwa katika hali ya uzima. Lakini pili, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, hata wakati ambapo sikuwepo uliweza kunirudishia. Hilo nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni mfupi tu. La kwanza ambalo nataka kulizungumzia ni suala la rushwa hasa katika Idara ya Mahakama, ambayo inaonekana kwamba hii habari ya rushwa imeenea mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika na tukitaka tushtaki kwamba hili ni tatizo zito la rushwa na bado pamoja na jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika kutafuta ufumbuzi wa suala hili, bado dawa haijapatikana na niseme kwamba kuna sababu nyingi tu zinazopelekea rushwa, lakini yote hayo bado hayajawa ni siri ya kuweza kusababisha rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka niishauri Serikali katika kutafuta ufumbuzi wa suala hili, asubuhi tunakuwa tunasoma dua kila tukifika hapa, kuna haja kubwa. Nilikuwa nashauri katika kutafuta njia moja ya kutafuta ufumbuzi wa hili suala la rushwa, hasa katika Mahakama, kuanzia wafanyakazi wake wa chini mpaka hao Majaji wote kwa ujumla, basi tungelianzisha utaratibu maalum, tukawa tuna dua maalum, maneno maalum, ambayo yatakuwa yanasemwa kila siku asubuhi kwa wafanyakazi wote kuanzia wa chini hadi wa juu na maneno haya au dua hii isomwe na kila Mahakama atafutwe Sheikh mmoja na Padri mmoja, wakusanye wafanyakazi wote kila asubuhi kama tunavyofanya hapa, patolewe dua ya nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dua hii ni ya maangamizi kwa yeyote atakayeweza kuchukua rushwa, asubuhi hii ya leo mpaka jioni katika Mahakama hii basi Mungu amhukumu. Naamini Serikali ina uwezo wa kutafuta katika kila Mahakama, Sheikh mmoja, na Padri mmoja. Sheikh atatoa baraka zake, dua kali sana ya maangamizi, hali kadhalika na Padri naye atatoa dua kali ya maangamizi na hawa wahusika wawe wanaitikia. Naamini hili huenda likawastua kidogo wakasema kwamba looh hii dua kali. *(Kicheko)*

Sasa kila mtu atakapofikia hatua ya kuchukua rushwa, atasema looh ile dua, nadhani hii itaweza kusaidia. Mnaweza kuona ni mchezo lakini kwa kweli ina faida kubwa na naomba Mheshimiwa Waziri, hili ulitazame na uweze kulifikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba, ametoa Semina mbalimbali za haki za binadamu kwa vyombo mbalimbali na Taasisi mbalimbali. Lakini nataka niseme wazi kwamba, asilimia kubwa ya Watanzania ambao ndiyo waathirika katika hili suala zima la haki za binadamu, hawajui hizo haki zenyewe za binadamu ni zipi. Kwa hiyo, mtu anaweza akavunjiwa haki

yake ya msingi lakini kwa sababu hajui, anaweza asiweze kujua ni hatua gani ya kuchukua. Sasa ni vyema basi kwanza paweze kutolewa taaluma kwa hawa wananchi wa kawaida wa chini ili kila mwananchi ajue haki yake ya msingi ili pale itakapovunjwa ajue kwamba sasa hapa haki yangu imevunjwa na hatua gani niweze kuchukua. Lakini kuwapa tu viongozi wa juu hii semina na pengine hao ndiyo wavunjaji wakubwa wa haki za binadamu, bila kuwafikishia wadau wenyewe wa hali ya chini, kwa kweli bado tutakuwa hatujafanya jambo la maana na la msingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ambayo nataka nichangie ni suala la uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Vitongoji. Napata matatizo sana kwamba chaguzi zote za Rais, Wabunge na Madiwani, zinakuwa chini ya uratibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, isipokuwa chaguzi za Vitongozi, Serikali za Mitaa, zitakuwa chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Hapa napata wasi wasi kwamba, haki haiwezi kupatikana. Kwa sababu wasimamizi wakubwa wa chaguzi hizi ni Wakurugenzi wa Wilaya pamoja na Maafisa Watendaji, ambao asilimia kubwa ya watu hao ni watu kutoka Chama kimoja, Chama Cha Mapinduzi.

Sasa kama tunataka kufanya haki kweli, katika Serikali za Mitaa, Vitongoji na Vijiji, basi ni vyema suala zima la uchaguzi kuhamishiwa kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili chaguzi zetu ziweze kufanywa chini ya usimamizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nimesoma katika ripoti yako kwamba unafikiria kuleta marekebisho ya Katiba. Naomba hili nalo ulifikirie kuhamisha chaguzi za Serikali za Mitaa kwenda moja kwa moja kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi tunasema kwamba, Tanzania tunakusudia kufanya uchaguzi huru na wa haki. Sasa kwa kupanga Tume ya Taifa ya Uchaguzi, niliomba Mheshimiwa Waziri, ufikirie kubadilisha utaratibu wa uchapishaji wa karatasi za kura. Kwa sababu mtu anatakiwa asijulikane nani kamchagua nani, ili aweze kuwa huru bila kuwa na mashaka, kuwa nimemchagua fulani, nikijulikana nitafukuzwa kazi au nitafanya nini. Basi ni vyema uchapishaji wa makaratasi ya kura usibakie kishina katika kura. *(Makofi)*

Kwa sababu utaratibu wa sasa wa kubakisha kishina katika kura katika *ballot papers* zile, inampa wasiwasi mpiga kura kwamba huenda baadaye uweze kufanyika uchunguzi kwamba nani na nani kampigia gani. Hapa kidogo kwa kweli mtu anakuwa hayupo huru katika kuchangua na ili aweze kuwa huru katika kuchagua, tunaomba katika utengenezaji wa *ballot papers* isibakie kishina. Yaani kinang'olewa chote. Kwa hiyo, pale uwezekano wa kujua nani kampigia nani unakuwa haupo na kwa hiyo mwananchi anakuwa na haki ya kuchagua pale ambapo ataona kuna maslahi, kama utaratibu wa sasa uliopita ulivyofanywa kwa upande wa uchaguzi wa Zanzibar *(ZEC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nichangie, ni hapo hapo kwenye marekebisho ya Katiba. Tunashukuru sana kusikia kwamba, Serikali inafikiria kuleta marekebisho ya Katiba, ni vizuri sana, lakini tunaomba iwe kweli ni marekebisho ya Katiba. Zaidi tungependelea marekebisho hayo yalenge katika kuendeleza Demokrasi ya Vyama Vingi Tanzania. Isiwe tunataka kufanya marekebisho ya Katiba lakini ikawa bado mfumo ni ule ule wa Chama Kimoja. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri, mfanye marekebisho ya Katiba ili ionekane kwamba, nchi hii imo katika mfumo wa Vyama Vingi na bado inaendelea zaidi katika mtandao mzima wa demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ninapenda kuzungumzia habari za Mahakama. Tunajua kwamba, Mahakama ya Rufaa tu ndiyo inayohusiana na suala la Muungano. Lakini tutakumbuka kwamba katika Muafaka, moyo wa tabia za Muafaka ilikuwa ni kuhusiana na marekebisho ya Katiba za Zanzibar na zirekebishwe kwa mujibu wa Mahakama za Jumuiya ya Madola. Suala hili walitafutwa wataalam wa *Commonwealth* wakafanya *write-up*, hawa wataalam na wakaipelekea Serikali kwamba tunafikiria utaratibu huu utafaa kufanya marekebisho ya Mahakama za Zanzibar ili ziweze kuwa huru zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la kusikitisha ni kwamba, hiyo *write-up* imepelekwa, imefunikwa na hadi sasa suala hili bado halijafanyiwa marekebisho. Tunajua kwamba, marekebisho yale hayahusu Muungano lakini tunajua kwamba huku ninyi ndiyo akina baba na wale ni watoto kama itakavyokuwa na bado ile ni Serikali yenu.

Kwa hiyo, tunapenda kushauri kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba wa Serikali ya Muungano, kushauriana na Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia na mambo hayo ya Sheria na Katiba kwa upande wa Zanzibar, ili kuona kwamba suala hili kwa mujibu wa Muafaka linatekelezwa ili kumjengea heshima Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa sababu yeye Mheshimiwa Rais alichukua ahadi mbele ya Watanzania na mbele ya dunia kwamba, atahakikisha Muafaka huu unatekelezwa. Naomba tusimwangushe Mheshimiwa Rais wetu, tunayempenda na amalize muda wake katika hali nzuri ili dunia iweze kumtumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. CHIFU ABDALLAH FUNDIKIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa si msemaji na nimesimama kukushukuru kwa kunipa dakika mbili, tatu, ambazo sidhani kama nitazimaliza na kutaka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haja yangu kubwa ilikuwa ni kutoa pongezi nyingi pia na kuonyesha *appreciation* yangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kwa sababu moja ama mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ninayoiona kwangu mimi ni kwamba, ninao uhusiano na yeye Mheshimiwa Waziri, namhesabu kwamba ni mwanangu. Si tu kwamba amekuja kushika Wizara ambayo niliianza mimi miaka tuseme kama karibu 40 sasa labda inakuwa, lakini pia ni kwa sababu ndiye amerithi mahala ambapo nilianza mimi na inanikumbusha na kunipa fahari kubwa kwamba anafuata nyayo zile zile za baba yake, ambaye alikuwa mtumishi wa nchi hii kwa muda mrefu na tulishughulika naye wakati tunaomba uhuru. Basi haya ndiyo yamenivutia na mimi mwenyewe *personally,* naona fahari kubwa sana kwamba kijana huyu anafuata nyayo zetu sisi wazazi wake za kufanya kazi nzuri katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa juu ya *debate* hii iliyoendelea, napenda kutoa ushauri mmoja tu nao ni kwa Mheshimiwa Mbunge wetu wa Sikonge, Mheshimiwa Said Juma Nkumba kwamba, haja ile aliyoomba kwamba Mheshimiwa Waziri apokee nyaraka kadhaa zinazohusu ile kesi ambayo ilihukumiwa huko ili yeye Mheshimiwa Waziri aingilie, ningependa asifanye hivyo kwa sababu ni waziwazi yeye Mheshimiwa Waziri hawezi kuingilia jambo lililohukumiwa Mahakamani hata kama ni Mahakama Ndogo ya sehemu yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa kama yeye anaona haki haikutendeka, basi awashauri wale ambao wanaona kwamba hawakupata haki, waombe rufaa, ndiyo njia iliyopo tu. Kwa hiyo, nataka nimwokoe yeye Mheshimiwa Waziri kwamba, asiwe na haja ya kumwambia kwamba aweze kupokea makabrasha yale na kwamba yeye si mahala pake pa kuweza kuingilia kesi ambayo imepita Mahakamani, ila wao kama wanaona hawakupata haki basi waombe rufaa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kumpa pole Mheshimiwa Zamda Bozzen, ambaye baba yake alikuwa rafiki yangu mkubwa, tukicheza mpira pamoja wakati huo. Yote yaliyompata hayo asahau na yeye aendelee tu kutumikia kama ilivyokuwa azma yake tangu hapo awali. Hayo yaliyompata yeye naamini kwamba yataondoka mara tu tutakapobadilisha Katiba labda na kusema kwamba, isiwe lazima kama ilivyo sasa ili mtu kugombea *public office* yoyote ya kura, awe mwanachama wa chama fulani.

Kikishabadilishwa kipengele hicho itakuwa sasa vyama vyenyewe vitaanza kuwaheshimu pia hata Wabunge na wanachama wao maana yake ikiwa watamtendea haki mwanachama, hana haja ya kusimama kwa tiketi ya chama kile, atakwenda katika chama kingine.

Lakini sasa haya yanatokea kwa sababu ukitaka kupata *public office* yoyote kwa njia ya kura ni lazima uwe mwanachama wa chama fulani. Hii nadhani ni *overdue* kabisa, ni heri iondoke mapema iwezekanavyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa dakika hizi chache labda nimezitumia kupita ukaribu ulionifanyia, naomba uniwie radhi kama nimefanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiunga mkono sana hotuba hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Fundikira. Nilikupa nafasi kwa sababu wale watatu walitumia muda mchache, nafasi zilibaki. Kwa hiyo, hatujapoteza muda. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze na mimi kuchangia hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu, ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kuhusu Makadirio ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2003/2004. Ni hotuba nzuri, ni hotuba yenye mwelekeo wa matumaini. Hivyo, napenda nitamke wazi kwamba, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu tangu Mkutano wa Bajeti uanze, naomba nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, waliochaguliwa na wananchi kupitia Chaguzi Ndogo, Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na Waheshimiwa Wabunge wa *CUF*. Pia napenda niwapongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Asha A. Ngede na Mheshimiwa Zamda S. Bozzen, Wabunge wa Viti Maalum kupitia Chama cha *CUF*. Napenda niseme kabisa kwamba, hawa ni Waheshimiwa Wabunge kupitia Chama cha *CUF* na wala siyo Wabunge wa Mahakama. Napenda kuwapongeza kwa kurejea humu Bungeni, hongereni sana kwa msimamo wenu. Naamini mna msimamo mmoja lakini mielekeo tofauti. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya ufinyu wa muda, mchango wangu utakuwa wa jumla jumla tu, utakaojielekeza katika maeneo machache na nitafanya hivyo kwa kifupi kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze na eneo moja lililochangiwa na Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, katika hotuba yake aliyoitoa kwa niaba ya Kambi nzima ya Upinzani, ni hili eneo la adhabu ya kifo. Kwa kifupi yeye anapendekeza adhabu ya kifo ifutwe na badala yake iwepo tu adhabu ya kifungo cha maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichonifanya nigusie kidogo hapa ni kwa sababu ameendelea kusema kwamba, Mheshimiwa Rais anapopunguza adhabu ya kifo kuwa adhabu ya maisha ni kinyume cha Sheria. Napenda niisahihishe kabisa kauli hiyo. Ukweli ni kwamba, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Jamhuri ya Muungano, kupitia ibara ya 45 ya Katiba, ana mamlaka ya kusamehe adhabu yoyote iliyotolewa na Mahakama yoyote ya nchi hii, ikiwemo adhabu ya kifo. Sasa hilo ni la msingi ni vizuri likaeleweka hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inakuja hoja yake ya pili, ucheleweshaji wa utekelezaji wa adhabu hiyo. Nashukuru kwamba Mheshimiwa Dr. Slaa, anakubaliana na Serikali na anaipongeza ingawa hakusema hivyo moja kwa moja. Naamini kwa wale ambao wamepatikana na hatia ya kunyongwa, ambao adhabu yao imefutwa na kubadilishwa kuwa kifungo cha maisha, nadhani wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Benjamin William Mkapa, wao na ndugu zao. Nadhani ni vizuri na hilo pia likaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kusema kwamba adhabu hii inafaa kufutwa kwa sababu ni mbaya, inatoa utu na inafanana na jino kwa jino. Nadhani kauli hiyo kama unataka kuiendeleza, ni vizuri Watanzania wote wakaungana na wewe. Kama kweli ndiyo mwelekeo wao wanaotaka kwenda huko kwa maana ya kuifuta adhabu ya kifo. Serikali imefanya tafiti zake mbalimbali katika eneo hili na matokeo ya tafiti hizo yanaonyesha wananchi walio wengi pamoja na dhana tofauti ambayo watu wanaweza kuwa nayo kuhusiana na matokeo ya adhabu hiyo, lakini wananchi walio wengi bado wanaunga mkono kuendelea kuwepo kwa adhabu hiyo. Kama tunataka kuelekea huko, tutahitaji mjadala mpana kwa kuwashirikisha wananchi wetu lakini hatuwezi tu kusema kama ilivyopendekezwa kwamba Serikali ilete marekebisho Bungeni haraka haraka ili kufuta adhabu ya kifo. Nimeona hilo niliseme kwa sababu ni suala la msingi sana na nchi ya Tanzania, ni miongoni mwa nchi ya makundi mawili. Yako makundi mawili, la kwanza, ni wale ambao wamefuta adhabu ya kifo na kundi la pili ambalo na lenyewe ni nchi nyingi sana ambao bado

adhabu hii inatekelezwa na wala haipingani na haki za binadamu. Kwa sababu ya muda nisingelipenda kujiingiza katika masuala yale ya *jurisprudence* kwa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niende kwenye eneo lingine. Ni kweli nashukuru sana kwa hoja za kuangalia maslahi ya Waheshimiwa Majaji, Mahakimu na Wanasheria wa Serikali. Hilo napenda nimwachie mwenye dhamana hiyo ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda niseme moja la kwangu kwa nafasi za Ujaji. Kuwa na sifa zilizotajwa na Katiba ya kuweza mtu kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu, Mahakama ya Rufani, hiyo siyo sifa pekee. Yapo masuala mengine ambayo lazima yanazingatiwa, mtu anaweza kuwa amebobea sana katika masuala ya Sheria lakini kimaadili hufai kabisa. Ndiyo maana kazi hizi na nafasi hizi huwa hazitangazwi. Wanawaangaliwa wale ambao wana sifa hizo za Katiba lakini pia wana zile sifa za ziada sasa. Maana kama ilivyoelezwa na wachangiaji wengi, kazi hizi ni ngumu, ni nzito na ni upweke sana. Lakini napenda kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa rai waliyoitoa ya kuiomba Serikali iendelee kuboresha maslahi ya watumishi wa Mahakama na watumishi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliulizwa hapa Bungeni kwamba Tume ya Kurekebisha Sheria ni kitu gani hasa, hiki chombo kina majukumu yepi na kimefanya kazi gani tangu kimeanzishwa? Chombo hiki cha Tume ya Kurekebisha Sheria kimeanzishwa kihalali kabisa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge, kilianzishwa na Sheria Na. 11 ya mwaka 1980. Katika kipindi cha uhai wake mpaka sasa, kimefanya kazi nyingi sana katika kuzirekebisha Sheria za nchi *either* kwa kutumwa au kuagizwa na Serikali au kwa Tume yenyewe kujituma. Tume imetoa taarifa zaidi ya ripoti 15 kwa masuala mbalimbali ambayo ilitumwa na Serikali na yale ambayo yenyewe iliona ijitume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume imeshughulikia masuala mengi na taarifa zake Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba huwa anaziwasilisha humu Bungeni. Kwa hiyo, ni chombo ambacho ni endelevu kwa maana ya kwamba kipo, hakina muda maalum ila tu viongozi wake hubadilika kama ilivyo kawaida ya kazi hizi. Lakini ni chombo cha kudumu kabisa na kitaendelea kuwepo na kimesaidia sana katika kazi ya kuhuisha Sheria zetu. Kwa wale watakaopenda kujua orodha ya kazi walizofanya, tunaweza kufanya hivyo lakini ni taarifa ambazo huwa zinawasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo liliulizwa, nadhani alikuwa ni Mheshimiwa Lekule M. Laizer, ilikuwa ni kuhusiana na adhabu, ndiyo ninayo hapa. Sasa tukasema hizi adhabu kwa wanafunzi wasichana, anasema Sheria ninavyoiona ni kwamba ina matatizo kidogo. Lakini tunasema kwa mujibu wa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana, msichana ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18, kama kwa bahati mbaya au nzuri, kwa kutegemea unataka kuliangalia vipi suala hili, atapata mimba, yule aliyehusika na kitendo hicho Sheria inambana na adhabu ya juu ni kile kifungo cha miaka 30. Kwa maana hiyo, sisi hatudhani kwamba hilo ni tatizo. Lakini kwa yule ambaye umri wake unazidi miaka 18, mimi nadhani hoja ya Mheshimiwa Lekule M. Laizer kwamba adhabu ni ndogo, ni hoja ambayo inazungumzika kuweza kuiona kama kuna haja ya kuiongeza adhabu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine linahusu haki za watoto na makundi maalum. Eneo hili liliguswa sana na upande wa Kambi ya Upinzani. Nataka niseme kwamba, haki za watoto na makundi maalum ni suala nyeti na linagusa maslahi ya makundi mbalimbali katika jamii yetu. Kwa sababu hiyo, ndiyo maana siyo kwamba Serikali inakuwa nzito. Masuala haya yanahitaji kufanyiwa utafiti wa kutosha. Tumeyafanya haya baada ya maandalizi ya muda mrefu kwenye eneo lile linalohusu haki za watoto na makundi maalum. Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imekamilisha maandalizi yote na kwa wakati muafaka Serikali itawasilisha Muswada Bungeni ili Bunge lako Tukufu lipate fursa sasa ya kuyatafakari mapendekezo yatakayoletwa na Serikali. Kwa hiyo, sidhani kama tumechelewa sana, naamini tumeifanya kazi ya uhakika. Ninyi Waheshimiwa Wabunge, ndiyo mtakaokuja kutusaidia pindi Muswada huu utakapowasilishwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine tuliulizwa kwamba, je, Serikali inaweza kueleza kwa kifupi aina ya Sheria zinazotawala maisha ya Watanzania hapa nchini pamoja na chimbuko lake? Ndiyo tunaweza tukaeleza, niseme tu zipo aina kuu nne hivi za Sheria zinazotawala maisha ya Watanzania, makundi manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la kwanza, ni Sheria zinazotungwa na mamlaka ya nchi, ambapo chimbuko lake ni Bunge hili. Sehemu kubwa tunayoifanya ya maisha ya Watanzania katika dunia ya leo hii pamoja na shughuli za Serikali na Dola kwa ujumla, zinatawaliwa na Sheria zinazotungwa na Bunge lako Tukufu. Kundi la pili, ni Sheria ambazo tulizipokea kutoka kwa Waingereza, walitutawala hawa Waingereza. Kuna Sheria ambazo za mila za Uingereza, kama zilivyokuwa tarehe 22 Julai, 1920 kule Uingereza, hizo ni *Common Law* na *equity*. Halafu lipo kundi la pili yaani ni Sheria za jumla zilizotungwa na mamlaka ya nchi kule Uingereza zilizokuwa zinatumika tarehe 22 Julai, 1920. Maana ya tarehe hiyo ya 22 Julai, 1920 ni tarehe ambayo wakoloni walianza rasmi kuitawala Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Sheria hizi Tanzania Bara ilipopata uhuru wake, ziliendelezwa hizi Sheria za Mapokeo kupitia Sheria nyingine ya nchi inayoitwa *"The Judicature and Application of Laws Ordinance* Na. 57 ya mwaka 1961".

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba, Sheria hizi zina nguvu hapa nchini isipokuwa kama Sheria hizo zitakuwa zimefutwa na Sheria iliyotungwa na Bunge lako Tukufu au kama zinapingana na mazingira ya nchi yetu.

Kundi la tatu, ni Sheria za Kiislam. Sheria hizi zinahusu masuala ya ndoa, mirathi na masuala ya wakfu na yote yale ya namna hiyo. Mimi siyo Muislam, lakini naamini kwa ufahamu wangu mdogo kwamba, chimbuko la Sheria hizo, ni imani ya waumini wa Dini ya Kiislam, ambao msingi wake ni Mwenyezi Mungu na kwa kuwa Katiba ya nchi yetu inatambua na kuthamini uhuru wa kuabudu, imani hiyo ya ndugu zetu waumini wa Kiislam inapaswa kuheshimiwa na vyombo vya Sheria na utoaji wa haki hapa nchini katika masuala yanayowahusu waumini hao. *(Makofi)*

Kundi la nne, ni Sheria za mila. Sasa chimbuko la Sheria hizi, ni jamii au kwa upana makabila mbalimbali ya Watanzania wenyewe. Sasa karibu asilimia takriban 80 ya Watanzania, shughuli zao za siku hadi siku za kimaisha zinategemea sana Sheria hizi za mila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo dhana hii ambayo imeanza kujitokeza kwamba, Sheria za mila zimepitwa na wakati. Ni kweli baadhi ya mila hizi zimepitwa na wakati lakini si sahihi kusema kwamba Sheria za mila hapa nchini zimepitwa na wakati kwa sababu msingi wa utamaduni wetu ni hizi mila na desturi, kwa Watanzania walio wengi katika nchi hii wanaishi kwa mujibu wa mila na desturi zao. Kama mila na desturi zao zimepitwa na wakati siku zote huwa nauliza hivi Sheria hizo zitapitwa vipi na wakati ambapo Watanzania wenyewe ambao ndiyo wengi zaidi ya asilimia 80 bado wapo na wanazitumia? Kwa hiyo, naomba tu kwa eneo hili tukubali kwamba, hakuna jamii hapa duniani ambayo haina mila zake. Tukubali kama Serikali inavyofanya kila wakati hapa kwamba mila hubadilika kadri jamii na mazingira yake yanavyobadilika, huo ndiyo msingi. Kwa hiyo, lazima tunaposema ziende na wakati ni kwa dhana hiyo. Lakini hatuwezi kusimama hapa na kusema kwamba, Sheria zote za mila hazina maana. Nimeona niyaeleze makundi hayo kwa maana niliyoyatoa ili wote tuyaelewe.

Eneo lingine ni Katiba. Imependekezwa, nadhani alikuwa ni Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha aliyesema, iundwe Kamati Maalum itakayowashirikisha wadau kupokea maoni na kuratibu na wengine wameniandikia kwamba kuwepo na Mkutano wa Katiba. Tumekwishapita huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme hili la Mkutano wa Katiba kwamba halipo. Zoezi hili la Katiba kwa maana ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu alilielezea juzi kwa taarifa, msingi wake ni kuendeleza yale ambayo Serikali ilipokuja hapa Bungeni mwaka 2000 ililieleza Bunge lako Tukufu kwamba: "Mheshimiwa Spika, tumeleta marekebisho haya ya 13 ya Katiba kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Jaji Kisanga".

Mheshimiwa Waziri, nashukuru kusema Mheshimiwa Jaji Kisanga na mwenyewe yupo hapa ananisikiliza, sasa ni Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu. Tulisema wakati ule yaletwe yale machache ambayo tuliona ni muhimu kwa wakati huo lakini furushi la maeneo mengine ya mapendekezo ya Kamati ya Jaji Kisanga yasubiri wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokisema Mheshimiwa Waziri Mkuu ilikuwa ni kuendeleza dhana hiyo. Hayo yaliyobaki ambayo sehemu nyingi ya mapendekezo ya Mheshimiwa Jaji Kisanga yalikubaliwa na Serikali na tulisema wazi hapa, sasa wenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano ni wananchi wenyewe. Sasa katika kupata maoni, Serikali iliona ni afadhali twende kwa wananchi wenyewe badala ya mikusanyiko hii ya warsha, makongamano na Mikutano ya Katiba, ambayo ni watu wachache tu wanajiteua waende kufanya kazi kwa niaba ya wengine. Haya ni maoni yaliyotoka kwa wananchi wenyewe wakasema ni kipi wanachotaka wakione katika Katiba yao kwa wakati tulionao. *(Makofi)*

Ufahamu wangu ni mdogo lakini ninavyofahamu jamii yetu ya Watanzania inawajumuisha pia Viongozi na Wanachama wa Vyama vya Upinzani na ndio maana fursa hiyo ilipotolewa ilitolewa kwa wote. Kama ulipewa fursa itumie huwezi kusema kwamba sisi ni kundi maalum mje mtuone sisi tuwape maoni yetu. Sisi tumeomba maoni kutoka kwa Watanzania na tunaendelea kuomba kama mapendekezo hayo yapo jamani yawekwe hadharani tuyaone. Huwezi ukaunda KAMAKA halafu mkajifungia kule KAMAKA, wakati haileti mapendekezo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu Viti Maalum, tumesikia ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. Alipolitoa hili nadhani ni rafiki yangu Karim Said Othman. Aah, kwanza niwapongeze sana, maana njia ya Viti Maalum mojawapo kwa upande wa akina mama kuingia Bungeni ambapo ni chombo cha juu sana katika uwakilishi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Nianze kwa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge Wanawake, ambao wametokana na njia ya wengi yaani kutokana na Majimbo ya Uchaguzi nao ni Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Hadija Kusaga, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Balozi Mongella, Mheshimiwa Fatuma Said Ali, Mheshimiwa Tatu Ntimizi na wengine wengi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ilivyokaa wala haiweki kiwango cha asilimia 30, tumesema kwa asilimia endelevu inaweza ikavuka hata hiyo ambayo tumeji-*commit* nayo. Naamini Mheshimiwa Rais, kwa busara yake eneo hili anaweza kulitekeleza.

Ndio Mheshimiwa Waziri alisema ukumbi nao ni *factor* moja lakini ukiniambia mimi nikakae kwenye *bench* kule aah mimi nakuachia Waziri sijui hawa wenzangu hawa nimesikiliza mchango wa Mheshimiwa Zamda Bozzen pale, huu upendo wa akina mama kwa upande wa *CUF* unaanza kutokea wapi? Wamewafukuza wale Wabunge Wanawake wa Viti Maalum halafu leo wanasema wako tayari kwenda kuketi nyuma kule! Aah sijui lakini nasema Waziri atalielezea suala hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Kuhusu Tume ya Uchaguzi, pendekezo la Mheshimiwa Karim Said Othman, kwamba Tume ya Uchaguzi isiwe na sura iliyopo sasa hivi, badala yake iwe na sura ya wajumbe wanaotokana na Vyama vya Siasa. Sababu gani? Kwa sababu wajumbe hawa wanaoteuliwa na Mheshimiwa Rais, wanawajibika mno kwa Rais. Mantiki yangu inanituma tu kuuliza hivi kama unasema kwa sababu wanateuliwa na Mheshimiwa Rais wanawajibika kwa Mheshimiwa Rais, hawa si ndio unataka wawajibike kwa Vyama vilivyowapeleka kwenye Tume? *Logic* hiyo nani ataikubali? Nasema jamani kidogo tuwe makini tunapojenga hoja hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Katiba inasema wazi kabisa jinsi Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi watakavyopatikana. Tumekuwa tunalielezea jambo hili na Kamati ya Jaji Kisanga imeelezea katika eneo hili wananchi walisema wana imani sana na uongozi wa Tume hiyo maana inaongozwa na Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa. Napenda tuelewane ninapowasikia wenzangu viongozi wa Vyama vya Upinzani na baadhi ya wanachama kwenye eneo hili wanasifu sana maamuzi yanayofanywa na Mahakama zetu kwa ngazi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani na ni Majaji wale wale, kwa sifa hizi ndio wanaenda kuongoza Tume. Sasa kama unakubali hukumu ni nzuri lakini inapofika Mwenyekiti anatoka Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa inakuwa haifai, sasa najiuliza nongwa iko wapi? Tunachotaka ni kuona *integrity, impartiality,* ya wajumbe wanaopelekwa kwenye Tume. Napenda kuipongeza sana Tume ya Uchaguzi kwa kazi nzuri ambayo imefanya, kwa kusimamia chaguzi tangu Mfumo wa Vyama Vingi urejee hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mchango mwingine wa Mheshimiwa Dr. Kamala, Mbunge wa Nkenge, yeye ana tatizo lake la siku nyingi kwenye Jimbo lake kuhusu masuala ya ushirika kuhusu kesi za watu waliotuhumiwa kufanya ubadhirifu na kufilisi Vyama vya Ushirika. Kwanza niseme jukumu la kwanza la kupeleka malalamiko ni la hawa ambao pesa yao mnasema imechezewa, imeibiwa kwa maana ya kwamba waende kulalamika Polisi, hilo sio suala la Serikali. Lakini la pili sasa kwa wale ambao walienda kulalamika Polisi na kesi zimepelekwa Mahakamani, suala la msingi pale ni ushahidi. Kuna baadhi ya kesi ambazo zilipelekwa Mahakamani katika Mikoa ya Kagera zimefutwa na Mahakama kwa sababu ya kutokuwa na ushahidi. Sasa tusiligeuze suala hili kuwa la kisiasa. Mahakama za nchi hii hazifanyi kazi kwa misingi ya kisiasa ni ushahidi tu na sheria. Kama ushahidi ukithibitika utapatikana na hatia lakini tunajua kesi hizi zipo zinaendelea.

Ningemwelewa sana Mheshimiwa Dr. Kamara kama angesema kwamba, jamani kesi zinaenda kwa kasi ndogo sana hamuwezi ku-*speed-up* kidogo kesi hizi, lakini kusema Serikali ichukue jukumu hilo, sio jukumu lake. Lakini najua Wizara ya Ushirika na Masoko wana taarifa zote za kesi zinazohusu ubadhirifu katika Vyama vya Ushirika Mkoa wa Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara wala sio kitu cha kificho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nimalizie kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, nimekaa muda mfupi sana Bungeni, lakini kila siku ninaposikia michango ya Wabunge kwenye eneo hili nafarijika na inanipa matumaini zaidi kwamba kuna viongozi wa nchi hii wanaojali sana mazuri yanayofanywa na sekta hii ya sheria hasa katika eneo la utoaji haki. Ndio mapungufu yataendelea kuwepo na ndio maana Serikali kupitia Bunge hili mnapotuongezea nguvu, tunapata faraja kubwa sana katika utendaji wetu wa kazi. Yale ya kwetu ambayo tunapaswa kuyasimamia tutaendelea kuyasimamia kwa kasi na kwa nguvu. Lakini pia bila kumwonea mtumishi yeyote katika utumishi wa vyombo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa nipigiwe kengele ya pili, lakini nimalizie kwa kukushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa usikivu wenu. Najua mmesema mengi ambayo kwa muda niliopewa nisingeweza kuwasaidieni sana, lakini nimwachie mtoa hoja ayaseme yale ya utekelezaji wa Sera za Chama kinachoongoza Serikali ya nchi hii ili tuweze kuhitimisha hoja yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache nasema tena naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kabisa, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maelezo mbalimbali kuhusiana na hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hii ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa mwaka 2003/2004. Pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mzee wangu, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, kwa dua ya kutuombea mema ili tuweze kukamilisha shughuli hizi za leo bila wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba uniruhusu kuwashukuru na kuwatambua Waheshimiwa Wabunge, ambao wamechangia kwa njia ya maandishi na kwa kuzungumza ndani ya Bunge. Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa niaba ya Mwenyekiti Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Asha Ali Ngede, Mheshimiwa Dr. Ibrahimu Marwa, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Karim Said, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Zamda Bozzen, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Mzee wangu Chifu Abdallah Fundikira na mwisho Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa Alhaji Mpeme, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Mwanaidi Jecha, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Janeth Mashele, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Christopher

Wegga; Mheshimiwa John Mwakipesile; Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Salim, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Feteh Mgeni, Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Athumani Kapuya, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao yote iwe ni kwa njia ya maswali au kwa njia ya kutoa maoni. Nawashukuru zaidi kwa sababu michango yote hiyo kwa kweli imelenga katika kuboresha na kuimarisha utendaji kazi wa Wizara yetu ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Hoja zilizotolewa ni nyingi na muda tulionao kama alivyosema Mwanasheria Mkuu ni mfupi kwa hiyo sitaweza kujibu hoja moja baada ya nyingine. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, mimi mwenyewe, Mwanasheria Mkuu na wataalam wangu wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu, ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Wizara, tumezipokea hoja hizo, tutazifanyia kazi na kabla ya Bunge hili kufungwa tutakuwa tumewajibu wote hao kwa maandishi. Hoja nyingine zilizotolewa zilizungumziwa na Waheshimiwa Wabunge zaidi ya mmoja. Naomba mniwie radhi kwa kuwa pengine sitataja jina la kila Mbunge aliyechangia katika hoja hii. Naomba kwanza uniruhusu nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu, ambaye amenisaidia sana katika mchango wake, ameweza kujibu masuala mbalimbali ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuishukuru Kamati ya Mheshimiwa Athumani Janguo, wamekuwa karibu sana na Wizara, wametupa ushauri mwingi, wameweza kutembelea maeneo mengi ya shughuli zetu na wameweza kujionea wao wenyewe matatizo na mafanikio yetu na kutushauri. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kwa hotuba yake nzuri, nzito na imekuwa ni mchango mkubwa katika shughuli zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaomalizika, nilifanya ziara katika Wilaya takribani 16 mbalimbali hapa nchini. Katika ziara zangu hizo, nimejionea mwenyewe na kushuhudia matatizo tuliyonayo. Matatizo hayo yapo katika viwango vinavyopishana kati ya Wilaya moja na nyingine. Kwa kweli Waheshimiwa Wabunge, hawakuongeza hata chembe ya chumvi katika kuyaelezea matatizo yanayoikabili sekta ya sheria kama walivyozungumzia katika hoja zao. *(Makofi)*

Chimbuko kubwa la matatizo haya ni ukosefu wa raslimali. Suala hili limezungumziwa na Kamati yetu ikiongozwa na Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na Wabunge wengine. Kwa kipindi kirefu sana tangu tulipojipatia uhuru sekta ya sheria haikuwa inapewa raslimali ya kutosha. Katika vita vyetu dhidi ya maadui wakubwa yaani umaskini, ujinga na maradhi, sekta ya sheria katika ujumla wake haikuonekana kuwa mmoja wa askari wapiganaji wa mstari wa mbele katika vita dhidi ya maadui hao.

Raslimali zilizotengwa kwa madhumuni ya sekta hii zilikuwa ni kidogo hazikutosha kukidhi mahitaji yake. Kutokana na sekta ya sheria kukosa raslimali kwa muda mrefu, sekta hii ilishindwa kuendelea kwa kasi sawasawa na sekta nyingine. Kwa hiyo, matatizo ambayo yamekuwa yakitukumba kama vile ya usafiri, uhaba wa vitendea kazi, kutokuwa na ripoti za hukumu za Mahakama, kutokuwa na marupurupu ya kutosha, haya yote kwa ujumla yametokana na uhaba wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matatizo hayo, katika miaka ya hivi karibuni kwa kweli Serikali imetambua umuhimu wa sekta hii na hivyo kuipatia fedha za kujaribu kutatua baadhi ya matatizo tuliyonayo. Kama Waheshimiwa Wabunge walivyoona katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara imeweza kupatiwa Bajeti kubwa zaidi na hasa kwa upande wa Mahakama. Kwa hiyo, hii ni faraja kubwa kwa upande wetu kuona kwamba, Serikali inaipa sekta hii umuhimu unaostahili na kuwa ni askari wa kutegemewa katika vita vyetu dhidi ya umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo ya jumla, napenda nijibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Yale ya Kamati yetu tumeyachukua na tutayafanyia kazi. Lakini nimeona ni vizuri nichukue nafasi hii kuyazungumzia yale ambayo yamezungumzwa na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa katika hotuba yake.

Kwanza niseme tu kwamba, baadhi ya mambo haya yamejibiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mimi nitapitia machache tu. Katika ukurasa wa tatu kuhusu haki za binadamu, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa kwamba, Tume hii imeundwa barabara. Ni sisi wenyewe ambao tulizungumzia na kuweza kuchomeka sura ambayo inahusu haki za binadamu na pia katika utaratibu wa kutafuta viongozi wenyewe tuliona kwamba watakaowatafuta viongozi wetu hao ni lazima wawe watu wazito. Kwa hiyo, hiyo *Appointment Committee* ikawa ni ya watu wazito, Maspika wa pande zote mbili za nchi yetu, Majaji Wakuu wa pande zote mbili za nchi yetu na Katibu wao akiwa Katibu Mkuu, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, ambaye pia ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, kwa kweli tuna imani kwamba, tumeanza vizuri na hatuna haja ya kuwa na wasiwasi katika eneo hilo. Viongozi wote hao sio viongozi mashuhuri tu lakini ni watu wenye uwezo ambao wamelitumikia Taifa letu kwa muda mrefu na ambao tunawaamini katika shughuli zao ambazo wamezifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, alizungumzia Sera ya Watoto. Kama alivyozungumza *AG*, sheria hii tutaileta hivi karibuni pia itazungumzia *children in the street* na *street children* na haki zao. Kwa hiyo, namwomba avute subira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mirathi, sasa hivi *draft* ya Muswada iko tayari itakwenda Serikalini na baada ya hapo tutawasilisha Muswada katika Bunge hili ili tuweze kuuzungumzia. Pia kazungumzia sheria za watoto ambazo zinahitaji kuangaliwa upya. Katika Sheria hiyo ya Watoto mambo haya pia yamezungumziwa kuhusu *definition* ya mtoto, kazi ambazo wanatakiwa wafanye katika umri mbalimbali, yote haya yamo katika Muswada ambao tunatazamia kuuleta.

Suala lingine ambalo amezungumzia Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, lilihusu mikataba mbalimbali. Ni kweli baadhi ya mikataba ya Kimataifa bado hatujaiwasilisha. Tunazungumza na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili iweze kufikishwa Bungeni kujadiliwa na kuridhiwa. Lakini mingi ya mikataba hii imekwishawasilishwa mingine bado tunaichunguza kuona kama inatufaa maana si lazima kwamba mikataba hii ya Kimataifa tuingize katika sheria zetu. Kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa kuwa, *domesticated*, ni lazima tuangalie ni vipi zinalingana vipi na mila na desturi zetu.

Sasa hivi katika nchi za Ulaya na sehemu nyingine katika dhana ya haki za binadamu, mwanaume na mwanaume kuoana ni suala ambalo linakubalika. Sasa likiingizwa katika tamko la haki za binadamu la Kimataifa, haitakuwa na maana kwamba sisi tutaliingiza hilo! Au tunataka baada ya kuwa na Viti Maalum vya Wanawake tuwe na Viti Maalum vya Mashoga, hii itakubalika? Kwa hiyo, inabidi masuala haya tuyatizame kabla ya kufikiria kuyaingiza katika sheria zetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Majaji, Mwanasheria Mkuu amelizungumzia, ripoti ya Jaji Mroso, tumeshaipokea na tunaifanyia kazi ikiwa ni pamoja na marupurupu na mishahara yao. Masuala mengine yanahusu utaratibu tu wa kiutawala mengine yanahusu masuala ya kisheria na mengine ya kikatiba. Lakini kwa ujumla yote haya tunayafanyia kazi. Masuala ya rushwa yapo lakini kama Wabunge wengi walivyozungumza ni kwamba, kwa kiasi kikubwa tumejaribu hasa *Chief Justice* mwenyewe, kuyafuatilia masuala haya, amekuwa akitembelea Mahakama na kuzungumza na wafanyakazi, amekuwa akiwachukulia hatua mbalimbali za kinidhamu na Mahakimu wengi wameachishwa kazi.

Kuhusu Bodi za Mahakama, nasema suala hili linakwenda vizuri. Nimetembelea Wilaya nyingi na pote nilipopita kwa kweli nimekuta Ma-*DC* wanalifuatilia suala hili na kwa sasa hivi wana Bajeti ya kutosha na wanakutana kuweza kuyatatua matatizo haya. Juzi nilipokuwa Karatu, *DC* wa pale alinipa ripoti kwamba wamekuwa na vikao kuhusu Bodi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo yalikuwa masuala makubwa ambayo Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ameyazungumzia. Kuna mengine ambayo yamezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengine kuhusu posho za wazee, nasema haya ni matatizo ya muda, tumo mbioni kuyatatua na madeni ambayo wazee hawa wanadai yatalipwa. Utaratibu tulionao sasa hivi wa kuwalipa Sh.1,500/= kwa kesi ambazo wanaanza na kuzikamilisha wengi wa wazee pamoja na Mahakimu wanaupenda utaratibu huu. Kweli kuna matatizo ya posho hizi kufika kwa wakati lakini tunafuatilia masuala haya kwa kushirikiana na

wenzetu wa Hazina. Ni hizi *warrant funds* ambazo hazifiki katika *sub-treasury* kwa wakati. Kwa hiyo, tunazungumza na wenzetu wa Hazina ili kuweza kutumia utaratibu wa *fax.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usafiri wa Mahakimu limezungumziwa na ni kweli ni tatizo. Lakini kama nilivyozungumza katika hotuba yangu asubuhi, tumeweka Bajeti ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya usafiri. Kwa hiyo, angalau mwaka huu Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 25 wanaweza kupata usafiri ili kuboresha ukaguzi wa Mahakama zetu mbalimbali.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA**

**FUNGU 40 - MAHAKAMA**

Kif. - 1001 - *Administration and General ...* Shs. 2,492,405,400/=

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kupata ufafanuzi kwa sababu nilipochangia niliulizia kwamba kuna watu waliofungwa miaka arobaini, sasa wameshatumikia kifungo cha miaka minne. Walipofungwa hawakujua kosa kwa sababu kwanza hata Kiswahili hawajui.

Kwa hiyo, wameshindwa hata kujitetea na mpaka sasa wanaendelea na kifungo. Sasa ningependa tu kuiuliza Serikali pamoja na kwamba hawa watu wamefungwa katika mazingira ambayo wao wenyewe wameshindwa kuelezea na hakuna mkalimani. Je, Serikali itasemaje juu ya hawa watu waliokaa muda mrefu hivyo Mahakamani na itatoa msaada gani kwa hao watu?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limekuwa ni la muda mrefu, limekwishafika mbali na kwa kweli hatuoni ni vipi tutaweza kusaidia. Lakini pamoja na hayo nashangaza kuona kwamba hakuweza kupatikana mkalimani wa Kimasai akazungumza Kiswahili, ahaa mimi Mmasai bwana, wako wengi wa namna hiyo ambao wangeweza kusaidia katika suala hilo. Lakini pia namwomba Mheshimiwa Mbunge basi tukutane tuweze kuona nini kilitokea na vipi tunaweza kusaidia, kama tukishindwa basi tutakuwa tumeshindwa.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kusema kwamba nadhani tumekwishakutana na *AG* na tumekutana na Waziri mwenyewe. Kwa hiyo, wote wanalielewa hili jambo. Lakini kinachonisikitisha anaposema kwamba jambo hili limekuwa la muda mrefu. Miaka 40, wametumikia miaka minne, ukitoa bado inabaki miaka 36 na ukisema ni jambo la muda mrefu kwa watu waliofungwa bila kujua, haieleweki. Walihukumiwa Meatu, sasa sijui kama kuna Wamasai walioko Meatu ambao wanaweza wakatafsiri lugha ya Kimasai, labda kama kuna wakalimali ni wakalimani wa Kisukuma siyo wa Kimasai kwa sababu Meatu hakuna Wamasai. Kwa hiyo, kama mimi sioni kwamba hili jambo kama ni la muda mrefu. Ningependa kusema kwamba naomba Serikali iwasaidie kwa sababu ni Watanzania, ni watu wetu, iwasaidie kwa sababu wamekwishapata adhabu. Hiyo adhabu ya miaka minne bila kujua kujitetea au bila kosa ni kubwa sana na ingetosha tu kusema kwamba wasamehewe. Kwa hiyo, tumekwishakutana na Mheshimiwa Waziri sasa sijui tukutane tena?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niseme tu kwamba sijui kama suala hili kwa kweli limenifikia mimi, labda *AG* analo. Lakini kama mmojawao yupo hapa Dodoma, basi mimi niko tayari kwenda naye huko Gerezani kwenda kuwaamkia hawa jamaa na kuzungumza na kuweza kupata ukweli wenyewe wa suala hili likoje na kuzungumza na vyombo vyetu vya Kimahakama. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechangia kwa maandishi kuhusu tatizo la ofisi yake ya Kabidhi Wasii kwamba ofisi hii iko kwa huduma ya wananchi, lakini ni ofisi yenye kero sana maana huwezi kupata simu ya ofisi hiyo wala barua ya fomu zako unazopeleka.

Katika kufuatilia imeonekana ofisi hii simu zake zimekatwa, kwa hiyo hazifanyi kazi, inaonekana ofisi hii haina hata hela za stempu. Sasa nilitaka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, sina haja ya kushika shilingi ila ninaomba kwa kweli kama hili ni kweli na kama limefanyika huko, je, ana utaratibu gani wa kuondokana na aibu hii ambayo kwa kweli itakuwa ni ya kidunia katika ulimwengu wa leo?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, analozungumzia Mheshimiwa Halinga ni kweli, tuna matatizo na ndiyo maana katika hotuba yangu nimeorodhesha matatizo mengi ndani ya sekta ya sheria ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Mahakama zetu na asasi mbalimbali. Hii Ofisi ya Kabidhi Wasii ina matatizo makubwa na Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala ilitembelea ofisi zile na imekuta kweli tunayo matatizo makubwa na sasa hivi mapato yao yanaelekea kuifanya ofisi hiyo kuwa ni *Executive agency. (Makofi)*

Kwa hiyo, inayo matatizo ya kifedha na nisingependa nikatae moja kwa moja kuhusu matatizo ambayo yamemkabili Mheshimiwa Halinga, lakini naomba basi tukae, tuzungumze na kama kuna matatizo ambayo ni *specific* basi tutafute njia ya kuweza kuyatatua.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *High Court* ... ... ... ... ... ... ... Shs. 359,369,900/=
Kif. 2002 - *Court of Appeal Dar es Salaam* ... ...Shs. 382,661,600/=
Kif. 2003 - *Arusha Zone* ... ... ... ... ... ... ... Shs. 483,048,900/=
Kif. 2004 - *Dar es Salaam Zone* ... ... ... ... Shs. 1,106,179,300/=
Kif. 2005 - *Dodoma Zone* ... ... ... ... ... ... ... Shs. 478,274,000/=
Kif. 2006 - *Mbeya Zon*e ... ... ... ... ... ... ... Shs. 801,018,600/=
Kif. 2007 - *Mtwara Zone* ... ... ... ... ... ... ... Shs. 439,553,800/=
Kif. 2008 - *Mwanza Zone* ... ... ... ... ... ... ... Shs. 724,525,400/=
Kif. 2009 - *Tabora Zone* ... ... ... ... ... ... ... Shs. 927,6833,700/=
Kif. 2010 - *Tanga Zone* ... ... ... ... ... ... ... Shs. 352,173,900/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2011 - *Primary Courts* ... ... ... ... ... ... Shs. 3,554,219,400/=

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia hicho kifungu cha 2011, nikilenga katika Mahakama ya Mwanzo ya Mjini Tarime. Katika hiyo Mahakama ya Mwanzo Ndugu I.M.F. alivamia kiwanja hicho na kujenga nyumba yake.

Baada ya kujenga nyumba yake Mheshimiwa Waziri alipotembelea Jimbo la Tarime badala ya kumhamisha walimwachia hiyo Mahakama wakimwomba awajengee nyingine na hiyo Mahakama ndiyo Mahakama iliyoko Mjini na ndiyo iliyo karibu na wananchi. Huyu ndugu *I.M.F.* amejenga Mahakama nyingine sehemu tofauti na hiyo ya Mjini na ameijenga kwa kiwango duni kuliko hiyo Mahakama iliyoko Mjini kwa maana msingi wake umejengewa msingi wa mawe na matope, mabati *gauge 30,* ukuta inchi sita na mbao ambazo hazikuwa *treated.* Kwa hiyo, hatutegemei kwamba hata kama hii wataichukua itadumu.

Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo napenda kuzungumzia ni kwamba hisia za wananchi kwamba Mahakama inauzwa kwa raia. Sasa ningependa nipate maelezo toka kwa Waziri kwa nini huyu mtu aliyevamia eneo la Mahakama badala ya kumwadhibu atoke aliamriwa kwamba apewe Mahakama. Sasa kama ndiyo huo mtindo basi itakuwa ndiyo mwanzo kwamba mtu akitaka eneo la Mahakama basi anajenga na akijenga Mahakama nyingine anaachiwa hilo eneo. Kwa hiyo, ningependa kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu suala hilo.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kumbukumbu zangu hazinifikishi mahali ambapo naweza nikasema nilishiriki katika suala hilo. Pengine tulikuwa tuna majibiano baina ya mimi pamoja na uongozi wa mahali pale, labda ni hilo walinishirikisha

lakini kwamba nilifikia hatua ya kusema kiwanja hiki apewe mtu fulani, ama kwamba Mahakama ijengewe nyumba na nini hayo mambo hayapo katika uwezo wangu kama Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba. Masuala haya yanahusu moja kwa moja Idara ya Mahakama siwezi nikaingilia katika masuala ya namna hiyo.

Lakini pamoja na hayo nitamwomba Mheshimiwa Chambiri tukumbushane ili aweze kunipatia mambo hayo kimaandishi ili niweze kulifuatilia suala hilo la Idara ya Mahakama. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilichangia kwa maandishi na katika mchango wangu nilijielekeza zaidi kwenye upungufu wa Mahakimu kwenye Mahakama za Mwanzo. Mheshimiwa Waziri alisema kwamba atatembelea Wilaya, ni kweli ametembelea na Babati ametembelea na nakumbuka kwamba alipewa ombi maalum la upungufu mkubwa wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Wilayani Babati.

Sasa nilitaka tu Waziri anihakikishie ni namna gani atatatua tatizo la upungufu mkubwa wa Mahakimu Wilayani Babati ikizingatiwa kwamba kuna mashauri mengi sana katika Wilaya hiyo kwenye Mahakama za Mwanzo. Naomba anisaidie maelezo ili nijue kwamba atatatua namna gani na nina hakika Mheshimiwa Waziri anafahamu hivyo.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Ni kweli nilitembelea Mkoa wa Manyara ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Babati kwenye Mahakama za Mwanzo nyingi tu zilizopo katika Wilaya hiyo na ni kweli pia kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu. Sasa kitu ambacho tumefanya mpaka sasa hivi ni kuorodhesha zile Mahakama ambazo zina upungufu mkubwa sana wa Mahakimu na tumekuwa tunapata maombi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wenzetu Serikalini ili tuweze kupanga hao wachache ambao tumepewa katika Mahakama hizo ambazo zina upungufu mkubwa wa Mahakimu.

Kwa hiyo, hiyo orodha sinayo, lakini katika haya maeneo mengi ambayo nimetembelea basi tunaweza kuwapa kipaumbele kinachostahili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kwaangw' basi tutazame ile list kesho.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2012 - *District Courts* ... ... ... ... ... ... ... Shs. 2,988,660,000/=

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Simanjiro ina miaka tisa sasa toka ianzishwe. Hatuna Mahakimu wa kutosha wa Mahakama za Mwanzo, Mheshimiwa Kwaangw' alieleza na wala hatuna Hakimu wa Mahakama ya Wilaya.

Nashukuru Serikali kwamba imetuweka kwenye huo mradi wa *Quick Start* lakini Mahakama ya Wilaya iliyo karibu ni Kiteto ambayo ni kilomita 150. Kwa hiyo, kwa Wilaya nzima hatuna Mahakama ya Wilaya, hatuna jengo wala Hakimu. Pamoja na huu mradi wa *Quick Start.*

Je, Waziri anaweza kunieleza kwamba tutakaa bila Hakimu wa Mahakama ya Wilaya mpaka hilo jengo lijengwe?

Je, ameshindwa kutafuta jengo lingine la kuazima hasa kwenye majengo ya Halmashauri ili kutupatia Hakimu kwa sababu wao wenyewe ndiyo wanatuambia *justice delayed, justice denied.*

Sasa kama ndiyo hivyo anataka kutuambia kwamba kwa Wilaya ya Simanjiro hilo halina maana au Waziri anatukubalia tuanzishe sheria za kimila na waziheshimu tukitoa hukumu ili kupunguza gharama kwa wananchi wa huko?

Lakini siyo jamii moja tu iliyoko pale, kwa hiyo wengine waliopo wataona hizi sheria ambazo hawazijui. Sasa tunaomba Waziri atuhakikishie lini na sisi tutapata haki yetu hii ya kupata Hakimu wa Wilaya huku wakijenga Mahakama ya Wilaya? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba na Idara ya Mahakama inatambua umuhimu wa kuipatia Mahakama ya Wilaya, Wilaya ya Simanjiro ikiwa ni pamoja na Mahakama za Mwanzo katika maeneo muhimu ambayo yana wawekezaji wakubwa kama pale Mererani.

Nilitembelea Mererani na sasa umekuwa ni Mji mdogo, lakini mpaka sasa hivi pale hawana Mahakama ya Mwanzo. Nimeona pale kuna watu wengi, biashara inakwenda kwa kasi na kuna wajuaji wengi. Kwa hiyo, hili tunalitambua kama ni tatizo kubwa ambalo tunalo, lakini sasa limeingizwa katika huu mradi wa *Quick Start* na ambao unatuhusisha sisi, Halmashauri zenyewe na wananchi. Kwa hiyo, ninachoomba kwa Mheshimiwa Kone ni kwamba tusaidiane kuhamasisha Halmashauri yetu pale na wananchi na sisi tutaendelea kuzungumza na wafadhili na Serikali yetu ili tuone ni vipi tunaweza kujenga kwa haraka Mahakama ya Wilaya ya Simanjiro na Mahakama za Mwanzo katika maeneo mengine.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hajajibu swali langu aniambie kwa kifupi hawatapata huduma ya Mahakama ya Wilaya mpaka jengo likamilike au tushirikiane kutafuta jengo ili wananchi wapate huduma hiyo? Ajibu moja kati ya hayo mawili.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua umuhimu wa Wilaya hiyo, atafute jengo na kesho asubuhi tutampa huyo Hakimu. *(Kicheko)*

Kif. 2013 - *Kagera Zone* ... ... ... ... ... ... ... Shs. 378,586,600/=
Kif. 2014 - *Ruvuma Zone* ... ... ... ... ... ... Shs. 433,815,900/=
Kif. 2015 - *Moshi Zone* ... ... ... ... ... ... ... Shs. 371,559,900/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Fungu la 41, lipo katika ukurasa wa 109 imeandika *Ministry of Justice and Constitutional Affairs.* Yale maneno yanafutwa inakuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, tumeyaweka kwenye *Hansard.*

**Fungu 41 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... ... Shs. 880,029,600/=

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza machache. Napenda nianze kwa kusema majibu yaliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba hayakuniridhisha. Ingawa amesema si vizuri kuingiza mambo ya siasa katika masuala ya kesi Mahakamani. Lakini napenda niseme mimi ni mwanasiasa na siku zote lazima nilete siasa katika masuala ya utendaji, na katika hilo sioni aibu ndizo kazi zetu. Na watendaji wajue kwamba watafanya kazi zao kwa kusikiliza matakwa ya wanasiasa na si vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu ni kwamba kuna ubadhilifu uliotokea katika Vyama vya Ushirika zaidi ya mabilioni ya fedha yalipotea. Sasa kuhusu *KCU* ni zaidi ya bilioni 2 na zaidi. Na ukienda kwenye mikutano ya hadhara wananchi wanakuuliza kwamba tulikatwa shilingi tatu kwa kila kilo ya kahawa na sasa tumebaki na stakabadhi fedha ziko wapi. Sasa hiyo siyo siasa. Issue ni kwamba wananchi walichanga fedha zao na fedha hazijulikani ziko wapi siyo siasa hiyo hata kidogo. Ni dhambi kubwa kusema hiyo ni siasa. Sasa mimi nataka majibu ya uhakika na ya kitaalam. La kwanza, kuna Kamati ziliundwa zikachunguza, *COASCO* chombo ambacho ni cha Serikali kilipitia katika mahesabu ya Vyama vya Ushirika kikasema kwamba kuna ubadhilifu, na *COASCO* ikishasema huwezi ukasema tena kwamba ni siasa, ni ama waliohusika wanapelekwa kwenye Vyombo vya Sheria ama hawapelekwi. Sasa

mimi nataka kusema *COASCO* ikishagundua kuna ubadhilifu Serikali inasubiri nini tena iambiwe na nani kwamba hao wapelekwe kwenye Vyombo vya Sheria. *(Makofi)*

Lakini vilevile nashangaa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaposema zipo kesi zilizopelekwa Mahakamani zikafukuzwa, ni zipi kesi hizo atoe orodha ya kesi hizo na kesi namba ngapi, akinipa orodha kwamba ni kesi namba hii ya ubadhilifu wa bilioni 2/= ilipelekwa ikakosa ushahidi Mahakama ikaifukuza nitakuwa sina matatizo hata kidogo. Lakini si kusema tu hapa halafu ukatumia neno siasa siyo sahihi hata kidogo.

Lakini vile vile napenda niseme Kamati ya kumshauri Mheshimiwa Rais iliyafanyia kazi haya mambo kitaalam ikatoa na ratiba ya kwamba kuanzia tarehe hii mpaka tarehe wahusika watafikishwa kwenye Vyombo vya Sheria na ikasema mhusika ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wengine. Sasa leo hii anaposema ni siasa maana yake ni nini hii. Si kweli hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa niseme mimi kama Mbunge nisingependa kulivalia njuga suala hili, kwa sababu linanijengea maadui zaidi kuliko kunijengea marafiki. Lakini wananchi walionipa kura niliahidi kwamba nitalisimamia suala hili siwezi kuja hapa nikaanza ubabaishaji. Nataka majibu ya uhakika siyo ya ubabaishaji. Sisi ni wanasiasa na tutaendelea kuwa wanasiasa ninataka mambo ya uhakika.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namuelewa sana Mheshimiwa Diodorus Kamala kuhusu utumishi wa wananchi, hasa tunapoongelea kwa masuala ambayo yanahusu taratibu za kisheria ni vizuri tukakubali kwamba Mahakamani hakuna siasa. Nimesema na ninapenda nirudie kusema kwenye Kamati yako kwamba Mahakamani ni suala la ushahidi na jinsi sasa Mahakama itakavyotumia ushahidi huo kutekeleza sheria ya nchi inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ombi lake la kupewa orodha ya kesi ambazo zilifikishwa Mahakamani na baadhi yake zikafukuzwa na Mahakama kwa kukosa ushahidi. Mimi napenda nimhakikishie kwamba kama angelikuwa amenipa taarifa kabla ya kurudi hapa saa 11.00 jioni tungelimpa orodha yote ya kesi. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama ilivyo Serikali nzima haifanyi kazi ya kubabaisha. Tunazo orodha ya kesi kama nilivyosema Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Mara, Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Mwanza. Tutampa orodha hiyo na orodha hiyo Ofisi yangu iliikabidhi pia kwenye Wizara ya Ushirika na Masoko.

La tatu, Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikusema tunaingiza siasa. Nilisema yeye aendelee kuwasaidia wanapiga kura wake. Lakini la msingi sasa ni kwamba unapolalamika kwamba kuna ubadhilifu kupitia hesabu zilizokaguliwa na *COASCO* sasa tusaidie basi wewe kwenda kusimamia kesi hiyo katika kutoa ushahidi, huwezi tu ukatwambia kwamba eti kwa sababu zimekaguliwa na *COASCO* basi tuwakamate watu tuwapeleke jela. Mimi nadhani tuwe watulivu kwa masuala haya. Mimi napenda nimwombe tu Mheshimiwa Diodorus Kamala kama *concern* yake ni kwamba kesi haziendi kwa kasi ambayo wote tunapenda kesi zimalizike nakubaliana naye moja kwa moja. Lakini siyo kwamba tunafanya kazi ya kulinda wabadhilifu wa kesi za wakulima wanachama wa Vyama vya Ushirika.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *Attorney General* ameanza kuongea lugha ambayo naweza nikaielewa kwa mbali. Lakini napenda niseme hapa Mheshimiwa *Attorney General* anaposema ningemueleza kama anataka orodha hiyo angekuja nayo si kweli, kwa sababu nilichoandika ni kwamba nataka maelezo ya kina na maelezo ya kina alitakiwa hata kama vitabu hivyo vinabebwa na *pick up* kwa ajili ya ushahidi aje navyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge ni mahali patakatifu na ni mahali ambapo Waheshimiwa Wabunge wanapokuwa hapa wanaweza wakataka chochote kwa wakati wowote. Tunamshauri Mheshimiwa *Attorney General* siku nyingine akisikia tunataka ushauri wa kina maana yake aje amejiandaa. *(Makofi)*

La mwisho, Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kesi kwenda taratibu hilo ni suala lingine. Lakini ningependa nisisitize hata Viongozi Wakuu sina haja ya kuwataja hapa walishaagiza vilevile kwamba

wahusika wahakikishe wanafanya kazi yao. Sasa napenda hapa nimkumbushe tena Mheshimiwa *Attorney General* kwamba afanye kazi yake na wasaidizi zake na akishindwa kufanya kazi yake na sisi tutafanya kazi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wabunge wakati wa Kamati ya Matumizi Mbunge anaweza kuzungumza kwa dakika tano hakuna dakika ya warning hapana, ni dakika tano kamili kengele ndiyo itagongwa.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hilo Fungu la 41 kitu ambacho anataka kupata maelezo ni kile ambacho umezungumza kwanza wewe kwamba sasa hili Fungu hapa lisomeke Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Lakini kwa kumbukumbu ukiangalia Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria wameshughulikia Wizara ndiyo waliopitisha bajeti ya Wizara hii. Sasa kama ni badiliko nadhani siyo wakati huu lingekuja baadaye, kwa sababu mabadiliko ya namna hii yamefanywa vilevile na Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Utumishi. Lakini *record* zimebaki hivyo hivyo kama zilivyokuwa *printed* watakuja kuleta mabadiliko baadaye. Kwa sababu vitabu vyote hivi sasa hivi vimekuwa *printed Ministry of Justice and Constitutional Affairs.* Kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba yeye aliomba fedha kwa ajili ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiyo nilitaka kuuliza mbona ameomba fedha kwa ajili ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini hakuomba fedha kwa ajili ya Wizara yake. Ndiyo nililotaka kuuliza hilo.

Lakini sasa Mheshimiwa Mwenyekiti umelirekebisha. Sasa mimi napendekeza na nashauri hivi vitabu vingebaki hivyo hivyo haya mabadiliko yaje baadaye kuliko kuanza kufumua hivi vitabu sasa hivi kwa sababu inaonekana tu katika Kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri. Lakini katika kitabu hiki pamoja na Kitabu cha Mipango ya Maendeleo Wizara ndiyo inaonekana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hili suala ni la Mwenyekiti. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameomba jumla bilioni 31,846,939,583/=, sasa hizi ni *break down* za mafungu. Lakini katika *documentation* ndiyo maana nimesema mimi na sikuomba majibu ya mtu yeyote. Kwa sababu hilo fungu la 41 siyo *Ministry of Justice and Constitutaional Affairs* ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali *like* katika mafungu mengine yoyote yale. Sasa mabadiliko mengine watafanya huko. Lakini kwa ajili ya *record* ya *Hansard* yetu tunataka hii ionekane ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na tumepitisha Fungu la *Attorney General.*

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kuhusu hiyo *Sub-Vote 1001.* Mheshimiwa Waziri katika kujibu hoja yangu moja alielekea kukubali kwamba kwa jumla Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba imekuwa inapata fedha kidogo tangu wakati wa uhuru. Na amesema kwamba atafanya mazungumzo na Wizara ya Fedha (Hazina) kuona kwamba hili jambo linabadilika. Nafikiri alikuwa anajibu ile hoja ya kiwango cha juu cha Bajeti.

Lakini mimi nilikuwa nafikiria hili suala siyo suala la kuahidiwa mazungumzo. Nilikuwa naomba nipate *commitment* ya Mheshimiwa Waziri kwamba bajeti ijayo kiwango cha juu cha Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa ujumla kitaongezwa ili waweze kufanya kazi zao sawasawa. Siyo suala la mazungumzo ni suala la commitment kwamba hili suala litatekelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai inawezekana Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba akaongeza.

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi kwamba ataongeza. Nasema kwamba siyo suala la mazungumzo ni kwamba ajitahidi a-*influence* hilo fungu liweze kuongezewa iwe *commitment* isiwe tu suala la mazungumzo.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumujibu swali lake Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai kama ifuatavyo. Kwanza kwa ujumla nasema tunaishukuru sana Kamati ya Mheshimiwa Athumani Janguo na Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai akiwa ni Mjumbe katika Kamati hiyo wametusaidia sana katika miaka hii miwili iliyopita katika kusukuma shughuli zetu na tukaweza kufikia katika bajeti hii.

Lakini pia niseme kwamba mambo haya yanakwenda na wakati. Tulikotoka huko tuliwekeza fedha nyingi katika masuala ya Kilimo, Mashirika ya Umma na mambo kadhaa, na sasa imefikia wakati ambapo sera yetu ya kuhodhi uchumi kupitia njia ya Vyombo vya Umma tunaibadilisha, tunabinafsisha na shughuli nyingi za kiuchumi zinajiendesha zenyewe.

Sasa kazi kubwa iliyopo ya Serikali ni utawala. Yaani *the Rule of Law* na kuona kwamba hizi *law enforcement unit* zetu zinapata fedha za kutosha. Kwa hiyo, Serikali imeanza kuweka fedha nyingi zaidi katika vyombo vyetu vya Kisheria *PCB,* Magereza, Polisi sasa hivi Serikali imetupia macho Mahakama pamoja na vyombo vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo, mimi nina imani chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais wetu ambaye anasisitiza mambo ya uwazi, ukweli na uwajibikaji ni kwamba Wizara hii itapewa fedha nyingi zaidi ikiwa ni pamoja na kupewa kipaumbele chini ya mradi huu au Mkakati wa Kuondoa Umaskini. Kwa hiyo, tushirikiane na Kamati na tushirikiane na Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai katika mazungumzo, lazima tuzungumze. Ili tuweze kufika mahali ambapo tunasema tunakubaliana kuongeza Bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 *Finance Accounts ... ... ...* Shs.217,422,700/=

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu wa maandishi nilimwomba Mheshimiwa Waziri anipe tamko kutokana na tatizo la wazee wa Mahakama ya Mwanzo Mtwara ambao wana miaka minne sasa wanadai posho zao na wazee wale sasa wameondolewa Mahakamani si wazee wa Mahakama tena. Anipe maelezo kwamba ni lini wanaweza wakalipwa fedha zao.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme kama ifuatavyo. Ndiyo nakiri kupokea taarifa hiyo. Lakini katika kuyazungukia maeneo ya Mkoa wa Mtwara kwa kweli kwa ujumla nimekuta kwamba wazee hawa wa baraza wanalipwa. Tatizo pengine ni fedha zile kutokufika kwa wakati. Lakini kama anayo matatizo kama alivyoyaorodhesha katika hoja yake kimaandishi basi tutayashughulikia na tutatafuta njia ya kuweza kulitatua tatizo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge lakini hii ni Idara ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambayo inahusika na suala lako ni Idara ya Mahakama. Lakini umepata faida ya majibu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Information Services ... ...* Shs. 489,863,000/=

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia nilikuwa nimetoa mapendekezo kadhaa yanayosaidia katika kujenga *Policy* ya Sheria katika nchi yetu ikiwemo *Constitutional College* na pia ikiwemo kubadili sheria zilizopitwa na wakati kama ile ya uchawi na sikuelezwa na Mheshimiwa Waziri sijui anaeleza kunieleza.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba niseme kitu kimoja hapa. Kwamba kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba muda wenyewe haukuturuhusu kuwajibu Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hasa wale waliochangia kwa maandishi, na ndiyo maana tumesema kabla ya mwisho wa Mkutano huu wa Bunge yote hayo yakiwemo haya mawazo mazuri ya Mheshimiwa Getrude Mongella na yenyewe yatajibiwa kwa maandishi. Naomba tu akubali ahadi yetu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*

*bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Administration General* ... ... ... Shs. 483,193,000/=
Kif. 2002 - *Public Prosecution* ... ... ... .... Shs. 1,451,624,400/=
Kif. 2003 - *Legislative Drafting* ... ... ... ... Shs. 348,023,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 *Civil International Affairs* ... ... Shs. 419, 485,200/=

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia nilitoa pendekezo kwamba kufanywe uchunguzi kwa nini madai dhidi ya Serikali yaongezeka. Nafikiri sikusikia *comment* kutoka upande wa Serikali juu ya hilo. Pia, pamoja na hilo kuna *concern* juu ya hii Idara inavyofanya kazi.

Katika Bunge lako Tukufu kumekuwa na *debate* kubwa juu ya Mikataba ambayo imeleta matatizo kama Mkataba wa *IPTL,* kama hii Mikataba ya Serikali ya kuuza Mashirika ya Umma na nini. Naomba tupate maelezo juu ya hii Idara inafanyaje kazi, Serikali ina-*consult* halafu wanatoa ushauri ambao siyo ama Serikali hai-*consult,* halafu wao wanakuja kufanya kazi ya kufunga vidonda.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimjibu kwa kifupi Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai kama ifuatavyo. Kuhusiana na wazo lake la utafiti, ni wazo lolote linapokelewa na sisi tutalifanyia kazi. Lakini nitasema moja la wazi. Jamii yetu ya Watanzania sasa imepata mwamko sana katika kutafuta haki na ni tofauti na miaka ya nyuma na ukiangalia kesi nyingi kwa sababu huwezi ukamkataza mtu asikupeleke Mahakamani basi Serikali inashitakiwa kama mtu mwingine ndiyo utaratibu wa sheria za nchi yetu. Kesi nyingi ni zile ambazo Serikali inapelekwa Mahakamani na wananchi au vyombo vya wananchi. Sasa ni vizuri tukafanya utafiti. Lakini lazima kuna mgogoro kwamba mimi nimetoa huduma Serikalini, mathalani lakini sijalipwa, sasa kama sijalipwa *solution* yangu nasema ni kwenda Mahakamani.

Lakini sisi upande wa Serikali kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiyo moja ya kazi zetu unapopata taarifa hiyo kwamba kuna kusudio la Serikali kupelekwa Mahakamani ndiyo lazima uwasiliane na chombo husika ili ujue kulikoni. Kama kuna Mkataba halali ndiyo unawashauri kwamba jamani hapa hata tukienda Mahakamani hamtasaidia mtashindwa.

La pili, hata Mikataba anayosema ya *IPTL* tungelikuwa na muda mimi siko hapa kujitetea. Kwanza naipongeza sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inayosimamia Mikataba ni vijana wazuri na wameiva katika maeneo yao na wataendelea kuivishwa.

Mkataba wa *IPTL* kama chombo cha Mataifa kilichosema Mkataba wenyewe misingi ya kisheria haina matatizo. Tatizo ni ile *capacity charge* kwamba kwa sababu misingi yote ya Mikataba hii *independent power agreements* ni kwamba unatumia ule umeme wakati ambapo unauhitaji lakini lazima uulipie. Sasa hilo siyo suala la kisheria, hiyo ni *technical accept* ya ma-*engineer* ambao wanapaswa sasa washauri hiyo. Mwanasheria anakwambia msingi huu ndiyo unaopaswa ukae kwa Mkataba.

Mimi nasema kwa hilo ni maneno tu unakuta watu wote na Mwanasheria Mkuu kwa maeneo ya Mikataba na kama nilivyosema siku ile nachangia Bungeni hapa. Kuna Mikataba mingi sana siyo wa *IPTL* tu, siyo mikataba inayosemwa ya ubinafsishaji. Maana lazima tulenge ni mkataba upi. Lakini hoja ya Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai tunasema ni nzuri kama ni kutafuta kiini cha tatizo tuweze tukajua tutafanya nini. *(Makofi)*

Lakini niseme tu la mwisho kuhusu swali lake la pili. Ni kwamba kwa utaratibu sisi hatwendi kutafuta kazi katika Wizara na Idara za Serikali. Ofisi yangu haiendi kupiga hodi jamani mna kazi hapa ya

kutupa na mnaomba ushauri hapana. Wao ndiyo wanatuletea na tumekuwa tunaishauri Serikali kwamba kwa masuala kama haya mazito ya Mikataba ni vizuri sana mkawahusisha Wanasheria tangu mapema msije tu mkafika mwishoni mkasema hapo ndiyo mnataka m-*involve* Wanasheria hapana, lazima uwe nao mwanzoni watakwambia *no* msiende namna hii, nendeni namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bila kuchukua muda wako nasema Ofisi yangu itaendelea kuisaidia Serikali katika kutoa ushauri na tunashukuru sana katika kuendelea kutunga mkono kwa kutoa mafunzo kwa Wanasheria waliopo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ahsante sana.

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa majibu aliyonipa. Lakini *statement* ya mwisho aliyosema kwamba Ofisi yake haifuati kazi wanaletewa kazi.

Je, ina maana kwamba kuna baadhi ya Mikataba au kuna baadhi ya sehemu nyingine ambazo Serikali imejikuta inadaiwa Mahakamani na wakati ambapo Serikali haikuuliza ushauri kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiyo anataka kusema hivyo. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi huwa tunaenda kwa kesi mahsusi, hatuendi hii ya kwenda kwa nadharia.

Mimi nimeeleza na ninaendelea kusema Serikali katika ujumla yake tunajua inaongozwa na watu ambao wanapenda kufuata taratibu za namna Serikali inavyopaswa kuingia katika Mikataba, kwa maana hiyo kwamba wanapaswa waende wakatafute ushauri wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa masuala ya kisheria.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *Constitutional Affairs* ... ... ... Shs. 288,851,500/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... Shs.2,007,585,400/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... ... Shs.482,737,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 64 - Mahakama ya Biashara**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... Shs.587,332,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 90 - Mahakama ya Ardhi**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... Shs. 460,814,800/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA**

**Fungu la 40 - Mahakama**

Kif. 2001 - *High Court* .......................... Shs.4 00,000,000/=

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub Vote 2001* makisio ya mwaka 2003/2004 isomeke *Rehabilitation, Renovation and Replacement of Equipment shs. 400,000,000/=.* Na *Total shs. 400,000,000/=.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Court of Appeal Dar es Salaam* ..... Shs. 1,000,000,000,000/=

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Masahihisho *Vote 2002 - Court of Appeal Dar es Salaam Rehabilitation of Appeal Building* badala ya shs. 500,000,000/= iwe ni 1,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2012 - *District Court* ... ......... ...... Shs. 150,000,000/=

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Kwa hiyo, kwenye *District Court* badala ya zile shs. 800,000,000/= iwe ni Shs. 150,000,000/=

**MHE. IBRAHIM W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani naona tumekwenda kifungu 2012 sikusikia kikitajwa kile kifungu 2011.

**MWENYEKITI:** Kinachofuata ndicho hicho. Kulikuwa na *printing error.* Kwa hiyo, hapa ni *District Courts* halafu kinakuja hicho 2011.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**MHE. ELIACHIM S. SIMPASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hatujakiona sawa sawa hapa. *District Court* hatujapaona. *Page* gani sijui?

**MWENYEKITI:** *Page 49*. Waheshimiwa Wabunge katika *Judiciary* eneo hili lote lilikuwa na matatizo. Sasa Waziri ana uwezo kufuatana na kanuni zetu kuweka mabadiliko kwenye Kamati ya Matumizi. Sasa haya anayoyasema Waziri ndiyo mabadiliko yenyewe katika kifungu hicho. Kitabadilishwa kurasa nzima lakini kwa sasa hatuwezi kufanya hivyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2011 - *Primary Court* .............Shs. 100,000,000/=

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, masahihisho tumeongezea katika ile *Public Buildings Project 6211. Public Buildings 50,000,000/=* kwa ajili ya Ujenzi wa Mahakama ya Manzese. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wakati nikichangia asubuhi kwenye hoja hii nilizungumzia tatizo la Mahakama ya Kitaji Mjini Musoma kutokuwa na vyoo. Na nikasema hii ni hali ambayo inatisha na tungehitaji hatua za dharura zichukuliwe na nikawa nime-*cite* hiki kifungu kwa maana kwamba kuna fedha pale ambazo zimeonyeshwa kwenye *projects* kifungu 6211 *Public Buildings 100,000,000/=* na hazikuelezwa fedha hizi zinakwenda wapi. Kwa hiyo, nikawa nimemwomba Mheshimiwa Waziri kwamba atakapokuwa ana-*wind up* basi atuhakikishie kwamba fedha zitatengwa kwa ajili ya kwenda kujenga choo ili hawa watumishi wa Mahakama wasiendelee kwenda kuomba hii huduma kwenye nyumba za jirani.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi 100,000,000/= ambazo anazizungumzia Mheshimiwa Dr. Ibrahim Marwa ni kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama Kuu ya Bukoba. Kwa hiyo, ni mradi mahsusi na umekuwa hapa kwa muda mrefu na hatujaweza kuutekeleza. Ili suala la vyoo ningeomba kwa kweli hawahamasishi wananchi ili wasaidiane kukusanya hivyo vitu ambayo ni mali yao. Eeh!!. Sasa hii mpaka twende Serikali Kuu tutafute mfadhili kwa kutufanyia masuala kama haya. Mimi nadhani yamo ndani ya uwezo wetu. Yeye kwa kushirikiana na Halmashauri na wananchi wangeweza kujenga hivi vyoo.

**MHE. IBRAHIM W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba. Nadhani kauli ya kusema kwamba kuna miradi ambayo wananchi wanatakiwa washirikishwe si kazi ya Serikali Kuu maana yake anatueleza hata hii miradi mingine basi wananchi wangeibeba moja kwa moja bila msaada wa Serikali Kuu. Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri aseme kwamba hili ni jukumu la Serikali kwa sababu Mahakama ile ni ya Serikali iko pale kwa muda mrefu na anihakikishie tu kwamba atatenga fedha kiasi kidogo kwa ajili ya ujenzi wa hii huduma ya msingi kabisa kwenye hii Ofisi ya Serikali.

Katika majibu yake anazungumzia hizi 100,000,000/= ni kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama Kuu Bukoba. Lakini hapa imeandikwa ni *Primary Court Budget Fund* kwa ajili ya majengo. Sasa haya majengo ni yapi ambayo hayakutajwa kwenye kitabu hiki cha Bajeti. Lakini Waziri anaeleza kwamba fedha hizi zinakwenda Bukoba sasa labda atusaidie. Lakini kama ni fedha za Mahakama za Mwanzo nilikuwa namshauri na kumwomba kwamba fedha kiasi zitolewe kwenda kujenga choo katika Mahakama ya Mwanzo Mjini Musoma. Ahsante Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Kwanza kabisa Waheshimiwa Wabunge mabadiliko aliyofanya Mheshimiwa Waziri fedha ni shs 50,000,000/= zinakwenda kujenga kama tumemsikia Mahakama ya Manzese. Kwa hiyo, kama kuna suala ambalo unajua kabisa katika kifungu halina neno hilo ndiyo maana tunatumia kifungu cha *Administration* katika eneo lile. Kwa hiyo, huku kwa kweli halihusiani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2013 - *Kagera Zone* ... ... Shs. 100,000,000/=

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Kagera Zone Sub Vote 2013* badala ya Shs. 50,000,000/= marekebisho ni Shs.100,000,000/=.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 41- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali..Shs. 4,458,241,090/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na
Utawala Bora ................................ Shs. 1,147,920,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria ............ Shs. 220,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 64 - Mahakama ya Ardhi ........................... Shs. 250,800,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kesi ile aliyetoa Mheshimiwa Marwa kama kuna jambo ambalo katika kile kitabu cha 4 unataka maelezo tu. Ndiyo maana tunauliza kwenye *Administration General.* Ukiuliza kwenye eneo la kifungu cha maendeleo kama sio yenyewe, Waziri anafanya nini. Kwa hiyo, ndiyo maana tukasema suala lako lilikuwa *irrelevant* ungeuliza kwenye Utawala kule angeweza kukueleza vizuri zaidi kuliko katika kifungu ambacho hakihusiki.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha pamoja na marekebisho. Hivyo naomba kutoa taarifa kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba Yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 01.41 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 18 Julai 2003 Saa Tatu Asubuhi)*